ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Farida Amour Mohammed Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Fatma Mbarouk Said Jimbo la Amani

42.Mhe. Hamza Hassan Juma Jimbo la Kwamtipura

43.Mhe. Hassan Hamad Omar Jimbo la Kojani

44.Mhe. Hija Hassan Hija Jimbo la Kiwani

45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu Jimbo la Mji Mkongwe

46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub Jimbo la Muyuni

47.Mhe. Kazija Khamis Kona Nafasi za Wanawake

48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

50.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 16 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 46

Tatizo la Dawa za Kulevya Zanzibar

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Kny: Mhe.Ismail Jussa Ladhu) – Aliuliza:-

Tatizo la utumiaji wa dawa za kulevya ambalo mara baada ya kuingia madarakani Serikali ya Awamu ya Saba lilionekana kupungua kwa kiasi kikubwa, hivi sasa linaonekana limerejea upya katika mitaa mbali mbali ya Mji wa Zanzibar.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea kurudi nyuma kwa hatua zilizochukuliwa katika miezi ya mwanzo ya Serikali ya Awamu ya Saba kupambana na janga hili la taifa?

(b) Mikakati gani imeandaliwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika kukabiliana na changamoto ya kurudi upya kwa uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya katika mitaa ya Mji wa Zanzibar?

(c) Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imechukua hatua gani kuunga mkono kazi kubwa inayofanywa na taasisi binafsi kupitia nyumba za '*Sober Houses*' katika kuwasaidia waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya kuachana na matumizi hayo huku ikitambua kuwa taasisi hizo zinatekeleza jukumu ambalo lilipaswa kufanywa na serikali?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, napenda kumtoa wasi wasi Mhe. Mjumbe kama kamwe juhudi hazikurudi nyuma za kupambana na dawa za kulevya, hasa tukizingatia kwamba janga la dawa za kulevya halina mipaka na huathiri kwa ujumla mustakbali wa rasilimali na nguvu kazi ya taifa ya vijana. *(Makofi)*

Juhudi zinaendelea na zipo kesi kadhaa zimekamatwa katika kipindi hichi. Katika mwaka wa 2010 kuanzia Novemba hadi Disemba ni kesi 67 zilizokamatwa, Januari hadi Juni, 2011 ni kesi 168 na kuanzia Julai, 2011 hadi Juni, 2012 ni kesi 104.

(b) Mhe. Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya Zanzibar, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad alikutana na wadau mbali mbali wanaohusika na udhibiti wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya, ili kupata maoni yao juu ya namna bora ya kulikabili tatizo hilo.

Shughuli hiyo ilifuatiwa na mkutano, ili kuzungumzia kwa kina changamoto zilizoibuliwa na wadau hao na kuwa na mikakati ya pamoja ya kukabiliana na janga hilo, kwa ajili ya kufikia lengo la kuifanya Zanzibar kuwa bila ya dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, iliandaa Kikosi Kazi kilichojumuisha taasisi tofauti za dola zilizomo katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kuandaa *Road map* ya utekelezaji wa Sheria ya Dawa za Kulevya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mjumbe pamoja na Wawakilishi wa Baraza lako hili Tukufu kwa jumla wawe na subra katika kipindi hichi ambapo mchakato wa ukamilishaji wa *Road map* hiyo unaendelea. Kwa hivyo, naamini kukamilika kwa mchakato huo kutatoa dira kwa taifa letu katika kukabiliana na vita hivi vya mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

Aidha niendelee kuvitaka vyombo vya dola vilivyopewa jukumu la kukabiliana na tatizo hilo kuongeza kasi ya utendaji kazi zao, ili kunusuru vijana wa taifa letu ambao ni wahanga wakubwa katika janga hili.

(c) Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kutanguliza shukurani za dhati kwa juhudi zinazochukuliwa na taasisi hizo za kijamii, katika kuunga mkono juhudi za serikali yao tukufu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutambua mchango wa taasisi zisizo za kiserikali katika suala zima la mapambano dhidi ya dawa za kulevya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, ilizipatia jumla ya shilingi milioni 9,900,000/= Nyumba 9 za Makaazi ya Vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya maarufu kama '*Sober Houses'* kwa Unguja na Pemba, ambazo zimetumika katika malipo ya kodi za nyumba, kununua baadhi ya vyakula na vifaa vidogo vidogo vya nyumbani.

Aidha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imetoa msaada wa vifaa vya *electronic* ikiwemo *television* na *radio* kwa *Sober Houses* za Unguja na Pemba. Mafunzo juu ya uongozi, utunzaji wa kumbukumbu na fedha yameweza kutolewa kwa viongozi wa makaazi hayo. Kwa kutambua umuhimu wa kuwa na uwiano mzuri na huduma zenye kuleta ufanisi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imetayarisha muongozo maalum kwa ajili ya makaazi hayo.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, itaendelea kuunga mkono juhudi hizi. Pia napenda kutoa wito kwa taasisi nyengine mbali mbali na jamii kwa jumla kuendelea kutoa msukumo na michango yao katika kuendeleza mbele harakati hizo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru pia nimshukuru swahibu yangu Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa kuuliza swali hili kwa niaba yangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ninataka nikiri kwamba wakati ninaandika swali hili na kulileta hadi sasa kuna mabadiliko ambayo tumeyaona kwamba udhibiti umerudi upya.

Lakini pamoja na maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, wakati hali ya mitaani kwa watumiaji kiasi kikubwa inadhibitiwa, bado udhibiti wa waingizaji na wauzaji wa dawa za kulevya katika mitaa yetu hili linaonekana kuwa bado kero kubwa kwa wananchi.

Mhe. Waziri kwa sababu yeye mwenyewe ni mkaazi katika Jimbo la Mji Mkongwe analielewa hilo, kwamba hali ndani ya Jimbo la Mji Mkongwe na majimbo mengine kuna malalamiko ya wananchi kuwa wanatakiwa kila wakati kushirikiana na serikali kwa kutoa taarifa kwamba wao ndio wanaokaa na hao wananchi wenzao wanawajua.

Kwa kweli wanatoa taarifa lakini kinachowavunja moyo ni kuona kwamba wanatoa taarifa watu wanakamatwa na mambo haya yanafanyika wazi wazi

wanajulikana kabisa na yako maeneo. Kwa mfano, katika Jimbo la Mji Mkongwe Mhe. Naibu Spika, kwenye eneo la Kanisa la Minara Miwili na karibu na Msikiti wa Bwana Udi maarufu pale, lakini baadaye watu hawa wanaonekana wanarudi mitaani na kuendelea na shughuli zao.

Sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba wamechukua juhudi gani katika kulibana Jeshi la Polisi ambalo ndilo linalohusika kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha kwamba kesi hizi zinapofanyiwa kazi zinafika hadi mwisho na wale wahusika wanachukuliwa hatua? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba nikubaliane naye kwamba ni kweli pamoja na juhudi ambazo zinachukuliwa na ofisi yangu na taasisi mbali mbali za kupambana na dawa za kulevya, bado suala la udhibiti wa uingizaji na uuzaji mdogo mdogo wa dawa za kulevya katika mitaa yetu bado ni tatizo sugu.

Naomba nimrudishe Mhe. Mwakilishi katika jibu langu mama, kwamba ofisi inaandaa *Road map* na sijui kwa Lugha ya Kiswahili kama nitapata neno zuri la kulitafsiri, lakini ni njia bora ya kuweza kujipanga vyema, ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi awe mstahamilivu, mikakati hii ni ya kiulinzi na usalama pia na inahusisha vyombo vya dola na wala si vyema tukaitoa hapa, kwa sababu itatufunga katika kuleta mafanikio kwenye kazi zetu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri wenzetu upande wa pili wa Muungano mara nyingi sana panapotokezea matatizo kama haya hutumia utaratibu wa kupiga Kura za Maoni za Siri, ili waweze kuwaadhibu wale wahusika katika masuala kama haya. Je, wizara yako ina mpango gani katika kukabiliana na suala hili kwa utaratibu ambao wenzetu wanautumia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwa upande wa Tanzania Bara kumewahi kutokea matatizo na ambalo ninalolijua zaidi ni uuaji wa ndugu zetu ambao wanaishi wakiwa na ulemavu wa ngozi (*Albino*), ili kutoa taarifa kwa wale ambao wanahusika na vitendo hivyo. Kwa kweli ofisi yangu imelifuatilia kwa kina na tumeona kwamba kuna matatizo katika mfumo mzima ule wa kupiga kura za siri katika kuwataja wale wahusika.

Mhe. Naibu Spika, tunaendelea kulifanyia kazi, lakini tumegundua kwamba utaratibu ule kwa Tanzania Bara ulizaa matatizo makubwa na kuleta fitna miongomi mwa wananchi wenyewe kwa wenyewe kwa kisingizio tu cha

kuona kwamba mimi nikimtaja huyu kwa kupiga kura ya siri kuwa anahusika na tatizo hili, basi vyombo vya dola vitamshughulikia. Vile vile wananchi wengi wana sababu zao wenyewe, visa vyao wenyewe vya mitaani, basi waliwataja watu wengi ambao hawahusiki kabisa na suala lile.

Mhe. Naibu Spika, ofisi yangu bado linalitafakari kwa kina kuona kwamba hili litakuwa ni moja katika mikakati ambayo itaweza kushughulikiwa katika utaratibu wetu mzima wa kulishughulikia suala hili kama itaona litaleta faraja katika jamii.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri ametueleza kwamba juhudi za kupambana na dawa za kulevya bado zinaendelea na ametueleza takwimu ambazo katika kipindi hichi wameweza kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Lakini Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo muonekano unaonesha kuwa hivi sasa suala la uuzaji wa dawa za kulevya limerejea upya mitaani.

Je, Mhe. Waziri anataka kulieleza Baraza hili kuwa wale wafanyabiashara ya dawa za kulevya wameongeza kasi ya kuingiza dawa hizo nchini?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naogopa sana kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kasi kubwa imeongezeka ya uuzaji.

Kwa kweli ofisi yangu inachofahamu ni kwamba bado Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinafanya kazi kubwa vikishirikiana na Vikosi vya Ulinzi Shirikishi vya katika maeneo mbali mbali ndani ya miji yetu hii na hata nje ya mji wetu kuhakikisha kwamba suala hili linadhibitiwa. Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa nilizonazo ni kwamba kasi imepungua na sio kuongezeka.

Kwa hivyo, inawezekana kwamba katika maeneo ambayo vyombo hivi vya ulinzi kwa kiasi fulani itakuwa imepunguza kasi yake ya kufanya *patrol*, lakini pia kupata mashirikiano ya Vikosi vya Ulinzi Shirikishi, basi watu hawa wabaya nao wakarudi kwa kiasi fulani. Lakini kwa ujumla hali sio ya kuzidi, isipokuwa kasi ya kupambana ni kubwa kuliko ya hawa wauzaji.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 95 naomba uniruhusu kwa heshima na taadhima ya hali ya juu kabisa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pia ni mtarajiwa Makamo Mwenyekiti wa CCM, kwa kazi nzito

na kubwa aliyoonesha ya kuwajali wananchi wake na kuwafikiria kupunguza vifo vya mama wajawazito. (*Makofi*)

Baada maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba swali langu lipate jawabu.

Nam. 95

Upatikanaji Huduma za Uzazi kwa Mama Wajawazito

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo mwezi wa Mei mwaka huu amemaliza kilio cha muda mrefu sana cha mama wajawazito cha kutozwa Ada ya Uzazi, jambo ambalo linamfanya astahiki pongezi kubwa.

(a) Je, wizara imejitayarisha vipi kuziba pengo la mapato yake?

(b) Wizara ya Afya imechukua hatua gani mpaka sasa kuhakikisha akinamama wanaojifungua katika hospitali zote za serikali wanapata huduma bure kama alivyoagiza Mhe. Rais?

(c) Wizara ina mpango gani wa kuongeza madaktari wa kutosha wanawake, ili kuondoa kilio cha pili cha mama wajawazito kusaidiwa kujifungua na madaktari wanaume baada ya wanawake?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 95 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wizara ya Afya pamoja na mimi binafsi nichukue fursa hii kumpongeza pia kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuamua kutangaza rasmi kwamba Huduma za Akinamama Wajawazito na Kujifungua zifanyike bila ya malipo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kupitia bajeti yetu ya wizara ya mwaka 2012/2013 serikali itaongeza fedha zaidi, ili tuweze kukidhi mahitaji ya huduma hizo.

Hatua ambazo Wizara ya Afya imezichukua, serikali imeturuhusu kutiliana mkataba wa muda mrefu na wanunuzi na wasambazaji wa dawa watakaopata *tender* au waliopata *tender*, kwa sababu shughuli zimeshaanza. Wizara itahudumia Hospitali ya Rufaa na mikoa, lakini *DANIDA* itahudumia Vituo

vya Afya na Hospitali za Wilaya. Mpango wa Huduma na Akinamama na Watoto nao utachangia vifaa muhimu, kwa ajili ya kusaidia kutekeleza agizo hilo.

Suala la kuongeza madaktari wanawake, kuchukua fani ya utaalamu kwa maradhi ya kike (*Gynaecologist*) halina uhusiano moja kwa moja na wizara, kwa sababu hii ni hiari na hamu ya daktari mwenyewe anataka kusoma nini. Kwa bahati mbaya madaktari wanawake hawako wengi na hao kidogo waliopo si aghalabu kuipenda fani hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana madaktari wengi wa maradhi ya wanawake ni wanaume. Mhe. Naibu Spika, kwa hivi sasa katika hospitali zetu hakuna hata daktari mmoja wa kike. Kwa hiyo akinamama *hatupati tukitakacho, isipokuwa tutapata tukijaaliwacho*. Kwa maana hiyo, tuvute subra na tuwahimize watoto wetu wanawake wasome masomo ya *science* na tuwahimize wachukue udaktari wa wanawake. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

(a) Kwa kuwa vituo vingi vya afya vijijini havina wakunga wa mama wajawazito, maamuzi yake yatasaidia vipi kupunguza vifo hivyo vya mama wajawazito baada ya kufukuzia kwa wakunga wa kienyeji, hivi anatoa wito gani?

(b) Kwa kuwa mama wajawazito wengi wanajifungua kwa upasuaji na wala hawana uwezo. Je, serikali imejipanga vipi katika mwaka huu wa fedha na kuhakikisha vifo vya mama wajawazito vinapungua au kwisha kabisa katika hospitali za serikali. Kwa nini serikali isitoe tamko lini utaratibu wa matibabu bure utaanza kwa vitendo wakati Mhe. Rais hakupata kigugumizi katika suala hili, ili wananchi wapate kujua lini wananchi wataanza kuhudumiwa kwa huduma hii, wakati tukizingatia kwamba bajeti ya Wizara ya Afya tayari imeshapita?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie maswali yake na yawe mafupi, ili niweze kufahamu, maana naona kama lugha inapandana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, rejea maswali kwa ufupi tena kwa utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante.

(a) Kwa kuwa vituo vingi vya Afya vijijini havina wakunga wa mama wajawazito, wanalazimika kujifungua kwa kutumia wakunga wa jadi. Je, serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa mama wajawazito wengi wanajifungua kwa upasuaji na hawana uwezo. Je, serikali imejipanga vipi kwa mwaka huu wa fedha kwa kuhakikisha vifaa vyote vya uzazi vinapatikana katika Hospitali za Serikali. Hivyo, kwa nini serikali isitoe tamko lini utaratibu wa matibabu bure utaanza kutekelezwa kwa vitendo kama alivyoamua Rais wa Zanzibar na kwa vile ukizingatia bajeti hii tayari imeshapita, wananchi wanataka kujua ni lini wataanza kupatiwa huduma hiyo bure?

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri umeyafahamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kiasi fulani.

(a) Kuhusu suala la wakunga vijijini ingawa tunasema tunao upungufu wa wafanyakazi, lakini katika mgao wa mwaka huu hakuna Kituo hata kimoja ambacho hakitokuwa na mkunga. Kwa hivyo, vituo vyote vinavyo wakunga.

(b) Suala la upasuaji, nafikiri katika kuzaa iwe kwa kupasuliwa au kuzaa kwa hiari ama Mwenyezi Mungu akikujaalia yote hayo yamo katika mpango huo wa kuzaa bila ya malipo. Kwa hivyo, hayo tumeyazingatia na tayari tumeshayafanyia kazi na tuna uhakika kwamba wazazi watazaa kwa hiari zao, uwezo wao na kupasuliwa bila ya kulipa.

(c) Mhe. Naibu Spika, nafikiri mwenye uwezo wa kutoa tamko nchi hii zaidi ni Rais kuliko wizara. Kwa maana hiyo, kama Rais amesema wazae bure ina maana watazaa bure na kwenye Hotuba ya Wizara ya Afya hilo lilitamkwa wazi na mimi sina la ziada hapa kusema. *(Makofi)*

Nam. 159

Mradi wa Ujenzi wa Bandari Huru

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilijibu swali katika Kikao cha Aprili, 2012 na kueleza taratibu za kujenga Bandari Huru zimeanza kufanyika baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya China.

(a) Je, utekelezaji wa mradi huo umefikia hatua gani?

(b) Kwa kuwa eneo la Mkumbuu na Mpigaduri Kisiwani Unguja yamefungwa kwa mradi huo, ni sababu gani zinazopelekea mradi huo kushindwa kuonekana maendeleo yake?

(c) Kwa kuwa Jumuia ya Afrika ya Mashariki umesharuhusu Soko la Pamoja, Zanzibar imejitayarisha vipi na kushindana na Bandari Huru Bagamoyo Tanzania Bara, ambayo imefikia hatua kubwa ya utekelezaji wake?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 159 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifutavyo:-

(a) Kwanza kabisa naomba nikiri juu ya kukubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kuhusiana na Kauli za Serikali juu ya azma ya kujenga Bandari Mpya ya Kisasa na Kubwa yenye Hadhi ya *Harbour Port* katika eneo la Maruhubi. Katika hatua za utekelezaji wa mradi huo ni kama tulivyoeleza wakati tukijibu swali Nam. 57 katika kikao hichi kinachoendelea.

Aidha kwa kumkumbusha tu Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, hatua iliopo ni kwamba uchambuzi umefanyika na suala la gharama ndio kikwazo kwetu, kwani serikali imeona ni vyema tukaangalia tena na kujiridhisha juu ya gharama iliyopendekezwa na Mkandarasi aliyefanya kazi hiyo ya uchambuzi yakinifu.

(b) Mhe. Naibu Spika, hakuna kitu kilichozuia maendeleo hayo hasa kwa upande wa Maruhubi, isipokuwa suala la gharama kama tulivyoeleza hapo awali.

(c) Ni imani yangu kwamba kutokana na faida za kimaumbile ya ki-*geographies* na mkondo wa bahari yetu, pindi kukikamilisha zoezi hilo, basi bandari zote hizo alizozitaja Mhe. Mjumbe ikiwemo pia pamoja na ile ya Mombasa, basi haziwezi kuwa tishio kibiashara dhidi ya Bandari yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, matarajio yetu bandari hii itakuwa ndio *Herb* kwa *East Africa and Central*. Kwa hivyo, tunaweza kutumia Soko hilo la

East Africa kwa huduma na shughuli nyengine zinazozalishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu yanayokatisha tamaa ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Je, katika mwaka huu wa fedha serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kufanikisha hatua za awali za ujenzi wa Bandari Kuu ya Zanzibar?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, juzi wiki mbili zilizopita tulizungumza katika swali Nam. 57 hatua ya serikali iko wapi na mradi huu unakwenda vipi na leo tunarejea tena, kwamba serikali tulichokifanya ni kufanya uchambuzi yakinifu, hivyo baada ya kufanya uchambuzi yakinifu tunachofanya ni kutafuta fedha. Kwa hivyo, katika bajeti ya mwaka huu hazimo hizo fedha za kujengea Bandari Huru.

Vile vile tumesema gharama yake inakisiwa iwe zaidi ya *Dollar* milioni 500 na katika bajeti hii hazimo, kwa sababu jambo lenyewe hatuwezi kusema kwamba tutajenga wenyewe kwa kupitia bajeti yetu ya wizara tunajidanganya.

Kwa maana hiyo, ukweli ni kwamba sisi tulichokifanya ni kukamilisha uchambuzi yakinifu na halafu tuendelee na utaratibu wa kutafuta fedha kwa kushirikiana na wahisani pamoja na washirika wa maendeleo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Nam. 160

Kufungwa kwa Barabara ya Forodhani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Oktoba mwaka jana serikali ilisema ilikiri kupitia swali Nam. 6 na Nam. 2 katika Kikao cha Aprili, 2012, kwamba hakuna sababu za msingi kufunga barabara ya kuanzia Malindi Round About hadi Nyumba ya Kulelea Watoto Forodhani na kuahidi kufungua barabara hiyo.

(a) Ni sababu gani zilizopelekea kufungwa njia hiyo hadi sasa na kupelekea msongamano wa magari?

(b) Kwa kuwa Sheria za Uhifadhi Mji Mkongwe zimekuja kulinda majengo yaliyomo katika Hifadhi ya Mji Mkongwe pamoja na

maeneo ya wazi. Je, ni sheria gani inayozuia gari kupita katika Uhifadhi wa Mji Mkongwe?

(c) Kwa kuwa serikali ilikubali kuifungua na kuondoa matofali ya zege yaliyofunga kipande cha barabara hiyo, ni lini itatimiza ahadi hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 160 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Sera ya Mji Mkongwe ni kuwa *Free Traffic Zone* na suala hili serikali imekuwa ikienda nalo hatua baada ya hatua. Kwa muda mrefu wananchi walizoea kutumia huduma za magari katika eneo hilo la Mji Mkongwe.

Aidha baada ya serikali kufanya maamuzi ya Mji wetu huu kuingizwa katika Orodha ya Miji Mikongwe na kutunga sheria mwaka 1994, basi tunalazimika na sisi kufuata na kuzitii sheria husika zile zinazosimamiwa na *UNESCO*.

Miongoni mwa mambo ya msingi kwa miji kama hii ya kihistoria ni pamoja na kudhibiti matumizi makubwa ya magari katika maeneo husika. Sambamba na mpango mkuu wa usafiri wa Zanzibar (*Zanzibar Transport Master Plan*), imeonekana ni vyema tukalifanyia eneo hili lisitumiwe na magari kiasi kikubwa.

Katika kufanikisha azma hiyo ndio maana serikali, ili tutekeleze vizuri na kwa kuzingatia mazoea yaliyojengeka kwa wananchi wetu, serikali imechukua hatua kwa kuanza kufanya *one way traffic* kwa eneo maalum, ili kubaini athari zake kabla ya kulisimamia eneo lote la Hifadhi ya Mji Mkongwe kulifanya kwamba lisiingie magari.

Mhe. Naibu Spika, baada maelezo yangu hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, barabara kutoka mzunguko wa Malindi hadi Nyumba ya Kulelea Watoto haikufungwa, isipokuwa imefanyiwa marekebisho ya matumizi kuanzia Baniani *Tree* hadi Nyumba ya Kulelea Watoto na kuwa *one way* badala ya kuwa *two ways*, kutokana na kuongezeka kwa magari. Vile vile kama tulivyoeleza katika swali (b) kuwa Sheria ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe zimekuja kulinda majengo pamoja na maeneo ya wazi yaliomo katika hifadhi hiyo.

(b) Mji Mkongwe kimaumbile hauhitaji na wala haupaswi kutumika magari mengi na hasa baada ya maamuzi ya serikali kuingia katika uhifadhi kama ilivyo miji mingine.

(c) Kwa kuwa serikali ilikubali kuifunga na kuondoa matofali ya zege yaliyoifunga kipande cha barabara hiyo, Wizara ya Miundumbinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uhifadhi ya Mji Mkongwe itatekeleza ahadi hiyo mara tu baada ya kuona msongomano uliozingatiwa na Sheria za Mji Mkongwe hazitoathirika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ukiona jambo ovu unatakiwa utumie mkono wako au ulimi wako na hili ni jambo ovu na limejibiwa na Waziri karibu watatu. Kwa kweli pamoja na majibu ninayopata mimi bado sijakata tamaa, isipokuwa nitaendelea nalo na ndio sifa ya Mwakilishi.

(a) Serikali kwa nini inaruhusu ujenzi wa ghorofa zaidi ya tatu katika Mji Mkongwe kama kweli tunafuata Sheria za *UNESCO*. Mhe. Waziri naomba anipe maelezo ya kina ambayo yataweza kuniridhisha.

(b) Kwa kuwa kufunga njia hiyo ni kupoteza ramani ya matumizi ya asili ya barabara ya Mji Mkongwe, hatua hiyo ni ya kuhifadhi au kuvuruga Mji Mkongwe Mhe. Naibu Waziri?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba unisaidie utaratibu ukoje. Kwa kweli imani yangu kwamba Mhe. Mwakilishi swali hili sidhani kama anauliza kwa maslahi ya umma na pengine suala hili Kanuni yetu ya 59(9) imeeleza kama anayo maslahi binafsi basi ni vyema Mhe. Mwakilishi akayasema, ili tukaweza kujua namna gani tunaweza kukabiliana na yeye katika kupeana majibu kwa taarifa kwa umma. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa ghorofa katika eneo la Mji Mkongwe unazingatiwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe baada ya kujiridhisha kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Kwa kweli mimi sina pingamizi na Mji Mkongwe kuamua wakiwa tu kwa sababu wao ndio wasimamizi wa Mji Mkongwe kwa mujibu wa Sheria za *UNESCO* na wao ndio wanaokwenda ku-*defend* katika vikao husika. Sasa ikiwa wao wameruhusu kwamba jengo lijengwe basi bila ya shaka itakuwa wameshafanya mawasiliano. Kwa hivyo, kama itakuwa wamefanya mawasiliano na wameridhiwa basi mimi sina pingamizi.

Kuhusu suala la kufunga barabara Mji Mkongwe umekaa na kwa bahati nzuri Sheria ile ya mwaka 1994 ukisoma ibara ya 14 kwenye Kanuni zao, ibara ya 42, 43 na 44 zimeeleza vizuri kiasi gani masuala ya barabara Mamlaka ya Mji Mkongwe, Manispaa, Jeshi la Polisi na wizara husika zitakavyoweza kushauriana, ili kufanya maamuzi. Kwa hiyo, imani yangu barabara ile ilipofungwa hakuna athari iliyotokea.

Mhe. Naibu Spika, kilichopo kwanza mji wetu tunataka upungukiwe na matumizi ya magari na ndio maana ikafungwa sehemu, maana eneo la Mji Mkongwe limefika Darajani na kuna *buffer zone* ya zaidi ya mita 50. Lakini serikali ilichokiamua ni sehemu ya Mji Mkongwe, kwa ajili ya kupunguza *traffic*, ili kuendana na maelekezo tuliyopewa na wenzetu wa *UNESCO*.

Mhe. Naibu Spika, mimi siamini kwamba kufunga barabara ile tumepoteza uasilia au tumepoteza ramani ya Mji Mkongwe. Kwa kweli ukiiangalia ile sheria imesema vizuri kwamba kuna *map three*, iliyoelekeza barabara zote za Mji Mkongwe na matumizi yake, kwa mfano, kuna matumizi ya pikipiki, matumizi ya gari. Lakini madhumuni ya serikali ni kupunguza ile *traffic* katika eneo la Mji Mkongwe tena kwa baadhi ya sehemu na sio eneo lote. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amezungumza suala la msingi kabisa kwamba pengine kuliko suala la njia kuruhusu kupita mara mbili au ikawa njia moja tu, zaidi ni suala la ukubwa wa magari yanayopita pale ndiyo yanayoweza kuathiri nyumba za Mji Mkongwe.

Sasa moja katika sababu zinazosababisha gari kubwa kupita pale Mhe. Naibu Spika, kuendelea kutumika kwa Bandari ambayo inayotumika na Meli za Mizigo, na katika majibu yake Mhe. Naibu Wizara katika Baraza hili aliwahi kutamka kwamba serikali ina mpango wa kuihamisha Bandari ile ya Mizigo au meli zile kwenda katika eneo jengine.

Je, wizara imefikia wapi katika hatua ya kuihamisha bandari ile pengine kwenda katika eneo la Mtoni kule, ili eneo la Mji Mkongwe liendelee kutumika kwa abiria tu? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli Mhe. Naibu Spika ukisoma Sheria ya Mji Mkongwe na Kanuni zake imekataa na imeelekeza wazi kwamba gari inayotakiwa kuingia katika eneo la Mji Mkongwe isidizi tani mbili na sheria iko wazi kabisa. Kwa hivyo, wajibu wetu kama Wizara husika na Jeshi la Polisi ni kusimamia tu kuona sheria hii inatekelezwa vizuri.

Lakini azma ya serikali ya kuhamisha Forodha Mchanga ipo na kwa mara ya kwanza tulijenga *ramp* katika Bandari yetu ya Malindi. Lakini baada ya kuja maoni ya kutaka kujenga Terminal katika eneo la Bandari, basi tumeona ni vyema kwamba *ramp* ile isitumike.

Kwa kweli azma yetu tunataka kuiondoa Forodha Mchanga tuipeleke Mtoni, ili kuweza kutoa huduma za mizigo katika eneo lile. Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi, kwamba Bandari ya Forodha Mchanga itahama na kwenda Mtoni. *(Makofi)*

Nam. 19

Mgao Katika Ukamataji wa Magendo ya Karafuu

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:-

Katika ukamataji wa magendo ya karafuu, kuna taratibu zinazoelekeza mgao wa asilimia kwa Ofisi za Mikoa, watoa habari na wakamataji wa karafuu hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri utaratibu huu umeanza lini na fedha za mgao wa Mikoa hutumika kwa shughuli gani?

(b) Kwa nini Kikosi kinachohusika na ukamataji wa magendo hayo, ambacho kinatumia mafuta na gharama nyenginezo katika shughuli hizo hakipatiwi mgao wowote?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 lenye vifungu (a) na (b) linalohusiana na mgao unaotokana na ukamataji wa karafuu za magendo kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa mgao wa karafuu zinazokamatwa kimagendo umeanza tokea msimu wa mwaka 2004/2005, ambapo mgao huo hufanyika katika utaratibu ufuatao:-

(i) Mkoa unaohusika na ukamataji unapata asilimia 50 ya mgao.
(ii) Anayetoa taarifa ya magendo hayo anapata asilimia 20 ya mgao.
(iii) Asilimia 30 inatolewa kwa walioshiriki katika ukamataji husika.

Fedha hizo kwa ujumla Mhe. Naibu Spika, hutumika kwa ajili ya kutoa motisha kwa wote wanaohusika na ukamataji wa magendo hayo, ambapo mkoa hutumia fedha hizo za mgao kuimarisha na kutoa motisha kwa Kamati yake ya Ulinzi na Usalama, ambapo miongoni mwa Wajumbe wake ni kutoka Kikosi cha Kuzuia Magendo.

Tabaan Mhe. Naibu Spika, Kikosi cha Kuzuwia Magendo pia huwa wanapata ile asilimia 30 endapo itathibiti kwamba wao ndio waliokamata magendo hayo.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Unajua katika kipindi kilichopita cha karafuu Serikali ilikuwa na ulinzi kabambe katika sehemu zake mbali mbali. Je, katika kipindi hicho tani ngapi za karafuu zilizokamatwa na zilikuwa zina thamani gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, katika msimu uliopita wa karafuu vipolo 31 vya karafuu vilikamatwa ambavyo vilitaka kutoroshwa kwa njia ya magendo ambapo vipolo hivi baada ya kuchunjwa na kusafishwa kuondosha michanga na makonyo zilipatikana gunia 20 ambazo ni sawa sawa na kilo 848, thamani ya karafuu hizi Mhe. Naibu Spika, hapo zilipouzwa katika Shirika la *ZSTC* ni sawa sawa na shilingii 12,720,000/-.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Zanzibar waliitikia wito kwa nguvu kubwa ili kusaidia Serikali kuzuwia magendo ya karafuu, kipindi kilichopita Serikali kwa kiasi fulani ilifanikiwa kuzuwia hayo magendo ya karafuu. Sasa namuuliza Mhe. Waziri kwa sababu anapokamatwa mtu kwenye magendo ya karafuu hukamatwa na boti yake hutaifishwa na Serikali. Je, ni boti ngapi zilikamatwa katika kipindi hicho kilichopita na kutaifishwa na Serikali.

Pili, ni maeneo gani na gani ndio yaliyokuwa na kazi hiyo ngumu ya kusafirisha magendo ya karafuu ili Serikali kipindi kijacho iweze kudhibiti zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, karafuu zote zilizokamatwa katika msimu uliopita wa karafuu katika magendo zimekamatwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba maeneo ya Mtambwe na Daya.

Mhe. Naibu Spika, jahazi moja ndio iliyokamatwa na hiyo mpaka sasa hivi iko katika mikono ya ulinzi na usalama Kaskazini Pemba.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyoelewa ni kuwa Serikali inatoa pesa nyingi kwa mafuta na inawalipa askari wake fedha kushinda baharini na kuzuwia karafuu zisiende magendo na wakati mwengine ndio nyengine zinakamatwa. Lakini kwa sababu karafuu ni zao la taifa ni mantiki gani iliyochukuliwa kuwa baada ya kukamatwa karafuu hizi mgao unakwenda kwa Wakuu wa Mikoa, wakamataji pamoja na watoa taarifa kwa nini fedha nyengine hazirudi serikalini wakati hii ni mali ya Serikali.

Pili, hivyo Serikali kutoa fedha zote hizi kwa kupambana na usafirishaji wa karafuu kwa njia za magendo halafu zikikamatwa ikawa haifaidiki chochote, hatuoni kuwa ni kupoteza pesa ya wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie swali lake la pili sijalisikia vizuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Swali la pili ni kuwa, wakati Serikali inatoa fedha nyingi sana kweli kweli kwa kuhangaika kuona kuwa karafuu haisafirishwi kwa magendo na karafuu ile inapokamatwa Serikali haipati chochote fedha inakwenda kwengine, hatuoni kuwa kwa kufanya hivi Serikali ni kupoteza fedha za wananchi bure.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, Serikali katika kupambana na magendo ya karafuu baada ya kukaa na kuzingatia kwa kiasi kikubwa imeona kwamba wanaohusika na ukamataji huo pia hawana budi nao kupewa motisha katika kazi hiyo nzito. Pesa asilimia 50 inapokwenda Mkoa basi Mkoa Mhe. Naibu Spika, uko ndani ya Serikali, hii Kamati ya Ulinzi na Usalama ni sehemu ya Serikali. Kwa mantiki hiyo basi, pesa hizo asilimia 30 bado zimo ndani ya serikali ikiwemo na ile asilimia 30 ambayo inakwenda kwenye kikosi kilichokamata magendo hayo.

Nam. 91

Ukosefu wa Mwanasheria katika Idara ya Wanawake na Ustawi wa Jamii Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Idara ya Wanawake na Ustawi wa Jamii Kisiwani Pemba inakabiliwa na ukosefu wa Mwanasheria kwa muda mrefu na kuathiri upatikanaji wa huduma za kisheria hasa kwa watu wanaofanyiwa vitendo vya unyanyasaji ikiwemo ubakaji.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuajiri haraka Mwanasheria ili kesi za watoto ziweze kufuatiliwa na kuhakikisha haki ya kisheria inatendeka.

(b) Ni sababu gani za msingi zinazopelekea kukosekana wataalamu wa sheria wakati vijana wengi wenye taaluma ya sheria hubakia vibarazani kutokana na ukosefu wa kazi.

(c) Ni kesi ngapi za unyanyasaji watoto ikiwemo za ubakaji zilizoripotiwa katika mwaka 2011/2012.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni swali lake Nam. 91 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwakilishi Wizara ina mpango wa kuajiri Mwanasheria kwa ajili ya kutoa huduma za kisheria katika ofisi ya Wizara Pemba mwaka huu wa fedha 2012/2013.

(b) Sababu kubwa zinazopelekea kukosekana kwa wataalamu wa sheria katika Wizara ilikuwa ni ufinyu wa bajeti wa ajira mpya serikalini. Hata hivyo, Wizara imeshaomba Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kukubaliwa kuingiza katika makisio ya watumishi mwaka huu.

(c) Kesi zilizoripotiwa za unyanyasaji na ubakaji zilikuwa 83 na kesi hizo zote sasa hivi zinashughulikiwa, lakini kesi 10 ndio ziko Mahakamani zinasubiri maamuzi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri aliyotoa Mhe. Waziri kwa kuwa tatizo la kesi za ubakaji na watoto kupewa ujauzito imekuwa ni tatizo sugu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mahakama za watoto badala ya kesi hizo kuendelea kusikilizwa na Mahakama za kawaida.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, swali sijalifahamu hata kidogo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa kuwa kesi za ubakaji na watoto kupewa ujauzito limekuwa ni tatizo sugu, Serikali ina mapango gani wa kuanzisha haraka Mahakama za watoto badala ya kesi hizo kusikilizwa na Mahakama za kawaida ili kuondoa usumbufu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:
Mhe. Naibu Spika, Serikali tukipata fedha tutakuwa tayari haraka sana kuanzisha hizi Mahakama za Watoto, kwa sababu kinachohitajika hapa ni fedha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, naomba nielezwe ni sababu zipi hasa zinazosababisha baada ya kubakwa na kupelekwa polisi ikawa kesi ikabakia pale kwa muda mrefu bila ya mtoto yule kupelekwa hospitali na mwisho wake tukasikia kuwa watu wale wamemaliziana kwa kuozeshana.

Pili, hivi wazee kuchukua hukumu ya mtoto aliyeathirika ni sawa badala ya kuchukuliwa hatua iliyokuwemo katika misingi ya kisheria kwa tendo hili lililofanywa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:
Mhe. Naibu Spika, ni hivi juzi tu nilisoma bajeti yangu nikaeleza matatizo yote yaliopo kwamba kesi mbali mbali zinatokea nyengine zinafika Mahakamani zinapitia kwenye vituo vya *One Stop Center*, lakini bado hukumu inakuwa ni ngumu kwa Mahakimu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, sina jibu zaidi ya hayo niliyokwishayaeleza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na Mhe. Waziri kukosa jibu zaidi ya hayo aliyojibu naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Kifungu nambari 18 cha Sheria ya Mtoto Nambari 6 ya mwaka 2001, ililetwa hapa ambayo ni Sheria ya Mtoto tukatumia pesa za Serikali kupitisha sheria ile, na kwa kuwa kifungu nambari 8 kimezungumzia wazi kuundwa kwa hizi Mahakama za Watoto na sheria tumeshaipitisha na Mhe. Rais kasha saini sheria hii. Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba Serikali yetu haiko makini katika kutekeleza mambao yake. Hilo moja.

Pili, kwa kuwa sheria ipo ya kuanzisha Mahakama hizi na kwa kuwa tulitumia fedha za Serikali kuipitisha wawakilishi hapa, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba kufanya hivyo yaani Serikali imechangia kutumia matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wajumbe wanafuatilia katika kikao hiki mimi nilijibu swali kuhusu Mahakama za Watoto na nilisema kwamba Mahakama za Watoto zipo kwa mujibu wa sheria zile za zamani na kwamba Mahakama za

Watoto hivi sasa zinashughulikiwa na Hakimu wa Mkoa. Sasa uanzishaji wa Mahakama ya Watoto peke yake tumesema hizo tunazitafakari na baadae tutaanzisha Mahakama za Watoto moja kwa moja, lakini hivi sasa Mahakama za Watoto zinaendelea. Kesi za watoto zote zinahukumiwa na Hakimu wa Mkoa. Kwa hivyo, Serikali bado iko macho na Serikali bado inaendeleza katika kushughulikia kesi za watoto kwa mujibu wa Sheria na kwa mujibu wa Sheria hii Nambari 6 ya mwaka 2001. Ahsante.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Katiba na Sheria

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena hapa leo hii, ili kujadili mambo muhimu ya kimaendeleo. Tunamuomba atuongoze ili tuweze kutekeleza kazi hii kwa hekima na busara na atuwezeshe kufanikisha malengo yetu kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kuiongoza vyema nchi yetu. Uongozi wake uliojaa hekima na busara umesaidia sana kuleta mabadiliko katika ustawi wa jamii ya Zanzibar, katika kipindi hiki kifupi cha madaraka yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii ya kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kutekeleza majukumu yao na kumshauri ipasavyo Mhe. Rais. Aidha, napenda kuwapongeza kutokana na juhudi wanazofanya katika kuyapatia ufumbuzi matatizo mbalimbali ya wananchi pamoja na kutetea haki zao.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda kukupongeza kwa dhati wewe Mhe. Spika, kwa umakini wako katika kuliongoza vyema Baraza letu tukufu, na kuwafanya wananchi kujenga imani juu ya chombo chao hiki. Vile vile

napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa watendaji wa chombo hiki chini ya uongozi imara wa Ndugu Yahya Khamis Hamad, kukusaidia na kukushauri ipasavyo, na kurahisisha utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa kazi za Baraza unategemea sana ushiriki wa Kamati zake. Napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati za Baraza kwa kutekeleza majukumu yao kwa umahiri. Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, inaoyongozwa na Mhe. Ali Abdalla Ali, kwa kuishauri vizuri Wizara yangu, wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kusimamia shughuli za Serikali. Maelekezo yao yametufanya tujiweke vizuri zaidi katika kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa jumla naomba uniruhusu niwapongeze Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao ya Baraza kwa umakini. Naomba pia uniruhusu niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mgogoni kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa shughuli zangu za uwakilishi jimboni. Na pia kwa kuwa wastahamilivu sana kwa kuniruhusu wakati mwengine kuwa nje ya jimbo kwa shughuli za kiserikali. Nawaahidi mashirikiano zaidi ili kwa pamoja tuweze kuleta maedeleo zaidi katika jimbo letu.

HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 4, 564, 991,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,184,842,000.00 zilipangwa kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na Shilingi 2,380,149,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012 fedha zilizopatikana ni Shilingi 4,473,357,411.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,688,114,112.00 yaani 123% ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 1,785,243,299.00 ambazo ni 75% kwa matumizi mengine. Kwa kazi za maendeleo, Shilingi 6,018,081,000.00 ziliidhinishwa, ambapo Shilingi 690,000,000.00 ni mchango wa Serikali na Shilingi 5,328,081,000.00 ni msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya hizo, jumla ya Shilingi 795,053,025.00 zilipatikana, ambapo Shilingi 540,000,000.00 sawa na 78% zilitoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Shilingi 255,053,025.00 (5%) zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Wizara pia ilikadiria kukusanya Shilingi 311,415,000.00 ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi

2011, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 209,486,847.00, sawa na asilimia 67% *(Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Machi 2012, Wizara iliendelea kutekeleza Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria. Programu hiyo inatekelezwa chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*). Aidha, Wizara inatekeleza sehemu ya mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara (Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Kampuni na kuimarisha Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali) ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Miradi mingine ambayo inatekelezwa na Wizara ni Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara ya Katiba na Sheria, Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mradi wa Matengenezo ya Jengo la Mahkama Kuu, Mradi wa Uanzishwaji wa Mahkama ya Biashara, Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi Mashtaka na Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Takwimu na Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya taarifa hiyo ya utangulizi, sasa naomba nitoe maelezo ya utekelezaji kupitia idara na taasisi moja moja za wizara yangu kwa mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli za kila siku za Idara na Taasisi za Wizara. Idara hii ndio kiungo baina ya Wizara na taasisi zake nyengine. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 idara imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Mapitio ya Sekta ya Sheria imeanza kwa kutekeleza Mpango wa Awali. Mpango huo wa awali unahusu kufanyika kwa tafiti zitakazotoa taarifa zinazohitajika kwa ajili ya kuandaa mkakati wa mageuzi. Vile vile, Mpango wa kuimarisha uratibu wa Jumuiya za Kiraia umeanza kutekelezwa kwa kuajiri wataalamu elekezi kufanyia mapitio Sheria ya Jumuiya (Nam. 6 ya 1995) na kuandaa mpango wa utekelezaji Sera ya Jumuiya za Kiraia ya mwaka 2009. Mpango wa miaka minne wa kusaidia Taasisi zisizo za Kiserikali umeandaliwa na unatarajiwa

kutekelezwa kuanzia mwaka 2013 chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (*EU*).

Mhe. Naibu Spika, Mpango kazi, Mpango Mkakati na ripoti mbalimbali zimeandaliwa. Aidha, Idara imeratibu utayarishaji wa Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) na Hotuba ya Bajeti. Kwa upande mwingine, Idara imemuajiri Mtaalamu Elekezi kufanya utafiti juu ya hali halisi katika vyombo vya dini vilivyo chini ya Wizara. Utafiti huo unahusisha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Afisi ya Mufti wa Zanzibar na Mahkama ya Kadhi. Lengo la utafiti huo ni kuiwezesha wizara kuzifahamu zaidi changamoto na fursa zilizopo ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji wa taasisi hizo.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 124,554,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 74,554,000.00 ni za matumizi mengineyo na Shilingi 50,000,000.00 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizopatikana ni Shilingi 83,046,050.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 53,046,050.00 (71%) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 30,000,000.00 (60%) ni kwa matumizi ya kazi za maendeleo *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) Kuratibu shughuli za mipango, masuala ya Jumuiya za Kiraia na taarifa muhimu za Wizara, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watendaji;
ii) Kuratibu mabadiliko katika sekta ya sheria na kuanza taratibu za kutayarisha sera za wizara;
iii) Kuimarisha Mfumo wa tathmini na ufuatiliaji kwa wizara; na
vi) Kushirikiana na wadau kuibua vipaumbele vya kiutafiti katika Sekta ya Sheria na kuweka mpango wa utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha Jumla ya Shilingi 172, 860,000.00 kwa

matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 787, 200,000.00 kwa kazi za maendeleo, zikiwemo Shilingi 160, 000,000.00 kutoka Serikalini.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni kiungo katika kuratibu shughuli za kiutumishi na uendeshaji kwa Idara na taasisi zilizo chini ya Wizara. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 idara imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma kiwizara, Idara imo katika hatua za mwisho za kukamilisha Mwongozo wa Mafunzo utakaokuwa dira ya kuwaendeleza wafanyakazi. Lengo kuu la mpango huo ni kuifanya wizara kuwa na mipango endelevu ya kuwapatia watumishi wake mafunzo yatakayoongeza ufanisi katika kutoa huduma.

Mhe. Naibu Spika, idara imeendelea kuwapatia mafunzo mbalimbali wafanyakazi wake kuanzia ngazi ya cheti hadi shahada ya kwanza ambapo wafanyakazi 11 wamepelekwa masomoni wakiwemo wanawake saba na wanaume wanne. Aidha, idara imeratibu mpango wa mafunzo wa mwaka mmoja kwa idara na taasisi za Wizara *(angalia kiambatanisho 9b).*

Mhe. Naibu Spika, katika kukuza mawasiliano na kupashana habari, idara imekamilisha mpango wake wa kuhuwisha tovuti ya Wizara ambayo imeanza kazi mwezi wa Juni, 2012. Katika Tovuti hiyo, taarifa, matukio, sheria na machapisho mbalimbali yatakuwa yanapatikana kupitia anuani ya www.zanjustice.go.tz.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha utendaji wake, idara imeendelea na matengenezo madogo madogo ya jengo pamoja na ununuzi wa vitendea kazi vipya ikiwemo kompyuta, mashine ya kutolea fotokopi na vespa moja. Idara imeratibu vikao mbalimbali vikiwemo vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, Kamati ya Ukaguzi wa Ndani na Vikao vya Bodi ya Zabuni. Aidha, idara iliratibu vikao vya ushirikiano kati yake na Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa matayarisho ya Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011.

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza kazi za ujenzi wa jengo jipya la wizara, idara iliendelea kusimamia taratibu mbalimbali za kufanikisha kazi hiyo kama ilivyoainishwa katika mpango wake. Kazi zote zilizopangwa katika kipindi hiki zimetekelezwa ikiwemo kumpata mshauri wa kusanifu michoro ya jengo na kusimamia ujenzi, kutangaza zabuni ya kumpata mjenzi na kuanza kwa ujenzi wenyewe.

Nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, baada ya kukamilisha taratibu zote za kisheria na za kiutawala, kazi za ujenzi wa jengo hilo zimeanza rasmi baada ya kutiliana saini mkataba na Kampuni ya *China Railway Jiachang Enginnering (CRJE),* tarehe 16/04/2012. Kazi hiyo inasimamiwa na Kampuni ya Taifa ya Usanifu Majengo (*National Estates and Designing Consultancy Co Ltd – NEDCO)* ya Dar es salaam. Ujenzi wa jengo hilo la ghorofa saba umepangwa kuchukua miezi kumi na nane na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2013.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Utumishi na Uendeshaji iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 438, 552,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 220, 442,000.00 zilitumika kulipa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 218, 110,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizopatikana ni Shilingi 406, 181,728.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 247,018,565.00 (112%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 159,163,163.00 (73%) ni kwa matumizi mengineyo *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha uwezo wa kazi za kuratibu masuala ya utumishi;
ii) Kujenga mifumo ya kisasa na kuratibu usaidizi wake; na
iii) Kujenga uwezo wa kiutendaji.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 566,653,000.00 kwa kazi za kawaida.

MAHKAMA

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Mahkama ni utoaji wa haki ili kuhakikisha kila mtu anaishi kwa amani na utulivu chini ya misingi ya Utawala Bora. Katika mwaka 2011/2012, Mahkama imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, jumla ya kesi 5,477 zilifunguliwa katika Mahkama mbalimbali Unguja na Pemba ikiwa ni upungufu wa kesi 2,894 ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo kesi 8,371 zilifunguliwa. Hali hii inaonesha ufanisi zaidi katika masuala yanayohusu jinai ikiwa ni pamoja na hatua ilizochukuliwa na wizara yangu ya kuwasisitiza Jeshi la Polisi kuifanyia kazi dhana ya kukamilisha upelelezi kabla ya kufungua kesi.

Mhe. Naibu Spika, kati ya kesi 5,477 zilizofunguliwa, 1,308 ni za madai na 4,070 ni za jinai, ambapo kesi 2,604 (48%) zimetolewa uamuzi. Picha hii inaonesha kuwa bado kuna kesi nyingi ambazo hazijatolewa uamuzi na hivyo bado kuna mrundikano wa kesi *(angalia kiambatanisho 5a)*. Wizara yangu imeliona hili na tumeshaanza kuchukua hatua mbalimbali ili kulisawazisha, ikiwa ni pamoja na mazungumzo ya kufikia maamuzi (*pre-bargaining*).

Aidha, wizara imeimarisha jopo la kuharakisha kesi na imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo wanaotaka kukata rufaa wanaharakishiwa mafaili yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara ya kwanza Mahkama, imeadhimisha Siku ya Sheria Zanzibar. Madhumuni makubwa ya maadhimisho hayo ni kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa Mahkama baada ya kumaliza mapumziko ya mwisho wa mwaka. Siku hii itakuwa ikiadhimishwa kila mwaka, ili kutoa fursa kwa Majaji, Mahakimu, Makadhi, Wanasheria na Watendaji wengine wa Mahkama kujua matatizo na mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka uliopita. Hii inatupa fursa ya kuona wapi tujirekebishe kwa ajili ya utekelezaji mzuri zaidi wa malengo yetu.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inafahamu sana kuwa utendaji wa baadhi ya wafanyakazi wakiwemo makarani na mahakimu hauridhishi. Rushwa,

uamuzi wa kesi hasa za madawa ya kulevya, kesi za ubakaji na mashauri yanayohusu ardhi, ni miongoni mwa mambo yanayolalamikiwa sana na wananchi. Matatizo haya,

Mhe. Naibu Spika, hata mimi yananikera sana na hivi sasa tumeshaanza kuyachukulia hatua. Zaidi mtizamo wetu sasa ni kuwa na kesi za vipindi (*session cases*) ili kuharakisha kesi hizi za dawa za kulevya na ubakaji. Hivi sasa tumeshaanza matayarisho ya kukamilisha lengo hilo na ni matumaini yangu kuwa tatizo hili *Inshaallah* litamalizika au angalau kupungua sana.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria mpya ya Utumishi ya 2011, mnamo tarehe 31 January, 2012 Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar aliizindua Tume ya Utumishi wa Mahkama. Tume hiyo, pamoja na mambo mengine, itakuwa na kazi ya kupendekeza watu wenye sifa za kushika nafasi za ujaji, uhakimu, ukadhi na nyenginezo. Pia, Tume hiyo itakuwa na kazi za kuwachukulia hatua za kinidhamu maafisa na watendaji wa Mahkama watakapokiuka maadili ya kazi zao.
Mhe Naibu Spika, Mnamo Machi 2012, Mhe. Jaji Mkuu pamoja na watendaji wengine wa Mahkama walifanya ziara katika Vyuo vya Mafunzo Unguja. Ziara hiyo ilimwezesha Jaji Mkuu kufahamu kwa kina matatizo yanayowakabili wanafunzi na mahabusu yakiwemo masuala ya mrundikano, ucheleweshaji wa maamuzi pamoja na upatikanaji wa nakala za hukumu. Baada ya ziara hiyo, Mahkama imeanza kuyachukulia hatua matatizo hayo.

Aidha, katika azma yake ya kuona wananchi wanakuwa karibu na Mahkama kupata huduma za kisheria, Mahkama ya Mwanzo ya Dunga inategemewa kuanza kazi zake mwezi Julai 2012, na sote tunajua kwamba ni hivi juzi ambapo Mahakama hii ilifunguliwa rasmi kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Kati.

Mhe. Naibu Spika, jengo la Mahkama Kuu Vuga limefanyiwa matengenezo makubwa ya ndani na hivi sasa yameshakamilika. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 sehemu ya nje ya jengo hilo nayo itafanyiwa matengenezo. Jengo la Mahkama ya Mwanzo Chwaka limefanyiwa matengenezo madogo madogo na matengenezo ya jengo la zamani la Mahkama Mwera yamekamilika. Matengenezo ya Jengo la Mahkama Kuu Chake Chake na Mahkama ya Kadhi wa Wilaya Mwanakwerekwe yanaendelea.

Mhe. Spika, katika kuimarisha Mahkama ya Kadhi, Makadhi saba (7) wa Wilaya waliteuliwa kujaza nafasi za Makadhi zilizo wazi ili kuongeza ufanisi. Vile vile, Kadhi wa Rufaa Pemba ameteuliwa. Aidha, Mahkama kwa ushirikiano mkubwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imekamilisha kazi ya kuifanyia mapitio na kuandaa rasimu ya Sheria ya Mahkama ya Kadhi nam. 3/1985. Kazi ya kuanzisha Ripoti za Sheria (Law Reports) imeanza kwa kukusanya maamuzi ya kesi mbalimbali na kuwekwa pamoja. Hivi karibuni tunatarajia kuteua Kamati kwa ajili ya kuandaa vitabu hivyo.

Mhe. Naibu Spika**,** Wizara imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Majaji wawili wa Mahkama Kuu wanakuweko Pemba kila mwezi. Utaratibu huu umeondoa mrundikano wa kesi za Mahkama Kuu huko Pemba. Hata mambo ya utawala yanayohitaji maamuzi ya Jaji Mkuu nayo yamepungua sana kufuatia utaratibu wa Jaji Mkuu kwenda Pemba kila mwezi na kuondoa ulazima wa mafaili ya Pemba kuletwa Unguja.

Mhe. Naibu Spika, matayarisho ya kuwa na Mahkama inayoshughulikia kesi za biashara yanaendelea vyema. Rasimu ya awali ya sheria inayotoa mamlaka kwa Mahkama hiyo imeshajadiliwa na Kamati ya Uongozi ya Wizara na hivi sasa ipo tayari kwa hatua zinazofuata. Sambamba na hilo, hatua za matengenezo ya jengo litakalotumika katika Mahkama ya Biashara zinaendelea vizuri. Mkandarasi wa kulifanyia matengenezo jengo hilo ameshapatikana. Hata hivyo, imebidi matengenezo hayo yachelewe baada ya kukosa msaada wa fedha kupitia mradi wa BEST, ambao ulikuwa usaidie shughuli hiyo, kutokana na mradi huo kusitisha shughuli zake. Matengenezo hayo sasa yatafanywa na Serikali katika bajeti ya mwaka wa 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, Mahkama imo katika utaratibu wa kutayarisha Mahkama maalum ya Watoto itakayokuwepo katika jengo la Mahkama Kuu. Katika kujiandaa na suala hilo, Mahkama imepeleka baadhi ya watendaji wake Dar es salaam katika Mahkama ya Watoto Kisutu, kwa ajili ya kujifunza. Kupitia msaada wa Shirika la Kusaidia Watoto (*Save the Children),* Mahkama inategemea kupata vifaa kwa ajili ya matumizi ya Mahkama hiyo ya Watoto. Haya yote ni katika kufanikisha utekelezaji wa Sheria ya Mtoto, Sheria nam. 6/2011'.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mahkama iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,324,000,000.00 kwa kazi za kawaida.

Shilingi 1,689,696,480.00 ziliidhinishwa kwa kazi za Maendeleo ambapo Mchango wa Serikali ulikuwa Shilingi 300,000,00.00 na Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia Shilingi 1,389,696,480.00. Vile vile, jumla ya Shilingi 48,000,000.00 zilikadiriwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2012 fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni Shilingi 1,780,138,219.00 ambapo Shilingi 1,333,527,219.00 zilitumika kwa mishahara, Shilingi 444,611,000.00 zilitumika kwa stahiki nyingine za watumishi na Shilingi 507,175,000.00 (97%) zilitumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, Shilingi 280,000,000.00 (93%) zilipatikana kutoka serikalini na Shilingi 66,148,000.00 (5%) zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika)*.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka 2012/2013 Mahkama imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kumalizia matengenezo ya jengo la Mahkama Kuu Vuga na kuanza matayarisho ya matengenezo ya majengo mengine ya Mahkama;
ii. Kuendelea na hatua za kuanzisha Mahkama ya Biashara;
iii. Kukuza upatikanaji wa haki pamoja na kutoa uelewa kwa Jamii kuhusu Mahkama na Kazi zake; na
iv. Kujenga Mazingira bora ya utendaji kazi.

Mhe. Naibu Spika, ili Mahkama iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 3,145,000,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,352,000,000.00 ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 793,000,000.00 kwa matumizi ya mengineyo. Vile vile, naomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 600,000,000.00, kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, Mahkama inakusudia kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali mapato ya Shilingi 72,000,000.00.

AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndio mshauri mkuu wa serikali kwa mambo ya kisheria. Katika kutekeleza jukumu hilo Afisi hiyo inafanya shughuli mbalimbali za kisheria. Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi mbalimbali za Serikali, uandishi wa

Miswada, kusimamia kesi na mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa hati na nyaraka mbalimbali za kisheria na kufanya mambo mengine ya kisheria kwa niaba ya Serikali. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Afisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kutekeleza shughuli za kawaida, ambapo miswada 11 imetayarishwa. Katika kipindi hicho, Afisi imesimamia jumla ya kesi 59 za madai ambapo kesi tatu kati ya hizo ni mpya na 56 ni kesi za zamani. Afisi imeweza pia kuwapeleka wafanyakazi wake katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kwa upande wa kuimarisha nyenzo, Afisi ilifanikiwa kuweka mtandao maalum wa internet (dedicated bandwidth) na mtandao wa ndani ya Afisi (*local area network*-LAN).

Mhe. Naibu Spika**,** mbali ya kazi za kawaida, katika mwaka uliopita wa fedha, Afisi imechukua hatua kadhaa za kutekeleza malengo iliyojiwekea. Lengo kubwa la Afisi ndani ya miaka minne ijayo, ni kuiwezesha Serikali na taasisi zake zote kupata ushauri na huduma za kisheria zilizo bora na zinazoendana na mazingira ya sasa. Miongoni mwa huduma hizo ni pamoja na huduma za uandishi wa sheria na hati mbalimbali, uwakilishi mzuri mahkamani na ushauri, na utayarishaji na usimamizi bora wa mikataba ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia azma iliyotajwa hapo juu, Afisi imeandaa rasimu ya Sheria ya Mwanasheria Mkuu ikishirikiana na wadau wa sheria kutoka sehemu mbalimbali. Mazingatio ya sheria hiyo ni pamoja na uanzishwaji wa Vitengo mbalimbali baada ya mfumo wa sasa wa Afisi kutokuwa na mgawanyo wa wazi wa majukumu. Katika kusawazisha kasoro hiyo, Vitengo sita vitaanzishwa. Miongoni mwa Vitengo vitavyoanzishwa ni Kitengo cha Usimamizi wa Mikataba ya Serikali. Vitengo vyengine ni pamoja na Kitengo cha Uandishi wa Sheria (Drafting), Kitengo cha Usimamizi wa Madai (Litigation), Kitengo cha Huduma za Sheria za Kimataifa na Kitengo cha Utawala. Afisi tayari imeomba idhini katika Wizara ya Utumishi wa Umma ya kukubaliwa muundo mpya wa Afisi na mahitaji yake ya watumishi.
Mhe. Naibu Spika**,** katika kuimarisha ufanisi huo wa huduma za Sheria kwa Serikali, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakusudia kuwaunganisha wanasheria wote walioko Serikalini kuwa chini yake. Aidha, wanasheria hao watawekwa, kwa mujibu wa sheria hiyo, katika makundi tofauti ya kiutumishi

kuanzia Afisa wa Sheria hadi wanasheria wa Serikali wa ngazi mbalimbali. Mfumo huu utawasaidia wanasheria wa Serikali kuwa na viwango vinavyofanana vya uelewa na uelewa wa mambo mbalimbali ya taaluma ya sheria. Aidha, maslahi yataandaliwa kwa kuzingatia muundo wa Utumishi wa Wanasheria wa Serikali ili kuleta uwiano kulingana na sifa na nafasi zao.

Mhe. Naibu Spika**,** ujenzi wa jengo jipya la afisi umeendelea vizuri. Jengo hilo litakapokamilika litaiwezesha Afisi kuwa na nafasi ya kutosha kwa shughuli zake zote ikiwemo maktaba ya kisasa na ukumbi wa mafunzo ya ndani kwa ajili ya teknolojia ya kisasa (multi-media platform). Ujenzi umekamilika kwa hatua ya kunyanyua kuta na mwelekeo ni kuanza kazi ya kuezeka. Matarajio ni kukamilisha ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013.
Mhe. Naibu Spika**,** kwa upande wa kazi ya kuziweka pamoja Sheria za Zanzibar (consolidation) kuanzia mwaka 1959 hadi 2010, rasimu ya mwanzo kwa mwaka 1980 hadi 2010 imekamilika na inafanyiwa mapitio. Hatua ya pili ambayo itajumuisha kuziweka pamoja sheria zilizobaki na kuzichapisha inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Kazi hiyo itapokamilika itaiwezesha Zanzibar kuwa na toleo jipya la pamoja la sheria zote jambo ambalo kwa mara ya mwisho lilifanyika mwaka 1958.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 612,077,000.00 zikiwemo Shilingi 137,216,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 474,861,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana kufikia Machi 2012 ni Shilingi 508,350,773.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 137,224,773.00 (100%) ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 371,126,000.00 (78%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya Shilingi 1,576,329,000.00 ziliidhinishwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Katika fedha za maendeleo zilizopatikana, Shilingi 212,412,000.00 zilitoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali kuchangia ujenzi wa Jengo la Afisi ya Mwanasheria Mkuu *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*
Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka 2012/2013, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kumalizia ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Afisi;
2. Kuendeleza kazi ya kuziweka pamoja (Consolidation) na Kuzichapisha Sheria za Zanzibar za 1959 hadi 2010;

3. Kukamilisha Sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuitekeleza;

4. Kuandaa Miswaada ya Sheria mbalimbali ili kuondokana na matumizi ya Sheria za zamani za Kiingereza;

5. Kuimarisha uwezo wa Watendaji hasa Wanasheria wa Serikali kwa kuwapatia mafunzo ya Sheria; na

6. Kuimarisha viwango vya uaandaji wa Miswada na Matangazo ya kisheria.

Mhe. Naibu Spika**,** ili kuiwezesha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 802,000,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 1,800,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Mhe. Naibu Spika**,** Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amewateua Makamishna watano wa Tume ya Kurekebisha Sheria, na sasa Tume imeanza kutekeleza majukumu yake. Miongoni mwa majukumu hayo ni kufanya mapitio ya Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho ya sheria hizo ili kuzifanya ziendane na wakati na mabadiliko ya sasa kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Vile vile, Tume ina jukumu la kupendekeza njia mpya za utekelezaji wa sheria, na kufanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuimarisha mfumo wa Sheria Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kipindi cha 2011/2012, Tume imefanikiwa kupata juzuu (v*olume)* zote sita za *'Zanzibar Decrees'*, na vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi. Mfumo wa mawasiliano umeimarishwa na muundo imara wa utendaji kazi unaendelea kujengwa. Katika kuimarisha muundo huo, Tume imetayarisha Mpango Mkakati na rasimu ya awali ya Mkakati huo imekamilika.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa sasa Tume inaendelea kuratibu mapitio ya Sheria kupitia Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na kujenga mfumo wa Usimamizi na Tathmini. Tayari Tume imewasiliana na Wizara zote za Serikali ili kujua Sheria zinazotaka kufanyiwa marekibisho na imeanza kazi ya kupitia baadhi ya sheria hizo. Katika mwaka 2011/2012, Tume imezipitia na kupendekeza

marekebisho Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria 16/1986 na Sheria ya Ushahidi Sura ya 5/1917. Vile vile, Tume imeanza kuifanyia utafiti Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Nam. 9/2006. Hata hivyo, mapitio ya sheria hiyo yamesita kutokana na kazi inayoendelea ya marekebisho ya Sera ya Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kujiimarisha kiutendaji, Tume imekuwa na uhusiano wa karibu na Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania Bara, Uganda na Uingereza. Watendaji wa Tume wamejifunza kutokana na uzoefu wa utendaji kazi wa Tume za nchi hizo katika kazi za shughuli na utafiti na mapitio ya sheria, pamoja na kupatiwa vitabu vya Sheria ambavyo vinaweza kusaidia kazi za utafiti.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Tume imepanga kuongeza wafanyakazi wa kada tofauti za kiutawala akiwemo Afisa Mipango, Afisa Utumishi na Afisa Manunuzi, kuimarisha vitendea kazi na kuimarisha uwezo na taaluma za watendaji ili kuwajengea mazingira bora na kuleta ufanisi wa kazi. Katika kutimiza azma hiyo, wafanyakazi wa Tume wamepatiwa mafunzo juu ya kanuni za utumishi na udhibiti wa mahesabu.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 174,914,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 59,457,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 115,457,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2011, fedha zilizopatikana ni Shilingi 162,128,363.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 46,671,363.00 (78%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 115,457,000.00 (100%) kwa matumizi mengineyo *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka 2012/2013, Tume ya Kurekebisha Sheria imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuendelea kuimarisha zaidi Afisi ya Tume na watendaji wake ili iwe na hadhi kama zilivyo Tume za aina hii katika nchi nyengine;

ii. Kufanya tafiti kwa lengo la kugundua kasoro kwenye sheria mbalimbali;

iii. Kufanya usambazaji wa habari zinazohusiana na matumizi ya Sheria za Zanzibar; na

iv. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume hii.

Mhe. Naibu Spika**,** ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 271,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 145,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina dhima ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka na kukuza upatikanaji wa haki za jinai na kuzingatia utawala wa sheria. Kifungu cha 56A cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria Namba 2/2010 ya Uanzishwaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka zinatoa majukumu ya Afisi hii. Hadi sasa Afisi ina vituo vya kazi tisa vyenye jumla ya wafanyakazi 82, ambao inawaendeleza kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbalimbali zinazohusiana na shughuli zao (*viambatanisho nam. 5c & 9b vinahusika*).
Mhe. Naibu Spika**,** hali halisi ya utekelezaji wa kazi za kawaida ndani ya mwaka wa fedha 2011/2012 imekuwa ya mafanikio kutokana na kukua kwa shughuli za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Afisi imeendelea kusimamia na kufungua kesi katika hali ya ufanisi, pamoja na kutoa ushauri kwa Jeshi la Polisi na kwa raia wanaofika afisini. Hadi kufikia Machi 2012, jumla ya kesi 891 zimefunguliwa, majalada 70 yamepokelewa na raia wasiopungua 180 wamefika afisini kwa ushauri. Pia, Afisi imeendelea kutoa makala za Jarida la SHAHIDI ili kuielimisha jamii juu ya misingi ya haki za jinai.

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi imefanya vikao mbalimbali na tafiti katika kuandaa mazingira sahihi ya utendaji kazi. Maandalizi ya uendeshaji mashtaka kiraia kwa Mahkama za Wilaya zilizobaki yamekamilika kwa asilimia 85. Hata hivyo, Afisi inakabiliwa na changamoto ya Idadi ndogo ya wanasheria, ambapo hadi sasa, pamoja na kupata ruhusa ya kuajiri wanasheria watano, bado wanasheria watano zaidi wanahitajika.

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi imeimarisha na kuendeleza mifumo ya utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na kuzindua miongozo ya upatikanaji wa ushahidi wa kitaalamu katika fani ya utibabu (*Standard Operating Procedures for*

Forensic Medical Practitioners – SOP). Hali kadhalika, Afisi imeimarisha huduma kwa kufanya manunuzi na matengenezo ya vifaa, kulipia gharama za mawasiliano na uendeshaji kazi na kufanya mikutano ya wadau ya kila mwezi katika kuratibu kazi za uendeshaji mashtaka.

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi imezifanyia matengenezo afisi ndogo za waendesha mashtaka Mkoani, Konde, Wete na Mwera. Vile vile, nyumba ya kuishi Chake Chake imekwisha ezekwa na ujenzi unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2012/2013. Matayarisho ya ujenzi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba yamefikia hatua ya kumtafuta mjenzi. Kwa upande mwengine, ujenzi wa Afisi ndogo ya waendesha mashtaka katika Mahkama ya Chake Chake haukuweza kufanyika kutokana na uchache wa fedha.

Mhe. Naibu Spika**,** napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria kimekwishaanza kazi rasmi. Hivi sasa kituo kimeshapata uongozi wa juu, akiwemo Mkuu wa Kituo. Mpango mkakati wa miaka mitano umetayarishwa na kuanza kutumika. Kituo kimeendesha mafunzo ya uandishi wa kisheria na kundi la kwanza lilikuwa na wanafunzi 18 ambao ni wanasheria kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 724,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 534,000,000.00 kwa kazi za maendeleo, pamoja na ruzuku ya Shilingi 50,000,000.00. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2012, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni Shilingi 619,050,025.00. Shilingi 297,153,025.00 zimetumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 321,897,000.00 (80%) zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za Maendeleo, Shilingi 200,000,000.00 (80%) zilipatikana kutoka serikalini na Shilingi 95,580,585.00 (34%) zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ruzuku iliyopatikana ni Shilingi 43,800,000.00 (88%).

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imejiwekea malengo yafuatayo kwa mwaka wa fedha 2012/2013;

1. Kukuza uwezo wa Afisi kwa kuimarisha rasilimali watu, miundombinu na upatikanaji wa vitendea kazi;
2. Kuimarisha na kuendeleza kazi za Uendeshaji wa Mashtaka; na

3. Kukamilisha kazi za Uendeshaji wa Mashtaka kiraia katika wilaya zilizobaki.

Mhe. Naibu Spika**,** ili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iweze kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 879,000,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida, Shilingi 250,000,000.00 kwa kazi za maendeleo, na ruzuku ya Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria.

AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar ina jukumu kubwa la kutoa miongozo na kutatua migogoro mbalimbali ya kidini Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Afisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi ya Mufti imeendelea kuimarisha uratibu wa taasisi za kidini, kutembelea baadhi ya Misikiti na Madrasa, pamoja na kuimarisha uendeshaji bora wa Madrasa Unguja na Pemba, ambapo Madrasa 2,000 zimetambuliwa. Aidha, Afisi imefanya kazi ya kuzitambua taasisi za kidini 73 zilizopata usajili kwa Mrajis Mkuu wa Serikali, na baadaye kufanya nazo mikutano kwa lengo la kuzikumbusha wajibu wao. Vile vile, Afisi imeendelea na utaratibu wake wa kupokea na kujibu maswali ya kidini, pamoja na kutatua migogoro ya kidini iliyowasilishwa kwenye Afisi hiyo.

Mhe. Naibu Spika**,** Baraza la Ulamaa ambalo limeundwa chini ya Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mufti ambacho kinaanzisha kuwepo kwa Kanuni za Baraza la Ulamaa ni kiungo muhimu katika masuala yanayohusu dini yetu ya Kiislamu. Katika kipindi cha 2011/2012, vikao viwili vya Maulamaa vilifanyika kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika**,** katika juhudi za kuendeleza dini ya Kiiislamu, Afisi imerekebisha Kanuni za Baraza la Ulamaa ambazo tayari zimeshatiwa saini na zimeshapelekwa kuchapishwa. Kwa kutumia Kanuni hizo mpya, Maulamaa hao wamekwisha kutangazwa rasmi. Baraza hilo litaanza kazi rasmi kuanzi mwaka wa fedha 2012/2013. Mhe. Naibu Spika, nina furaha kulieleza Baraza lako tukufu kwamba Afisi ya Mufti Pemba imepatiwa kifungu chake cha fedha (Sub Vote), ili kuimarisha utendaji wa kazi wa Afisi

hiyo. Afisi ya Mufti Pemba inaongozwa na Naibu Mufti na ni matumaini yetu kuwa shughuli nyingi zinazofanywa Unguja, sasa zitafanyika pia Pemba kwa ufanisi mkubwa. Vile vile, Naibu Mufti alihudhuria Mkutano wa Umoja wa Waislamu wa Afrika ya Mashariki (UWAM) uliofanyika Lamu Kenya, kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na kubadilishana taarifa mbalimbali zikiwemo za kuandama kwa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi imesimamia warsha ya siku moja juu ya amani na utulivu Zanzibar iliyohudhuriwa na wafuasi wa vyama mbalimbali vya siasa, madhehebu ya dini mbalimbali, vyombo vya habari, na vyombo vya ulinzi. Kwa upande mwingine, Wizara yangu ilichukua jitihada ya kuwaita vikundi vya kidini katika vikao ili kuwataka kuepukana na vurugu na fujo nchini mwetu. Baada ya kuona kuwa bado vikundi hivyo havihubiri dini ambayo ndio lengo walilojisajilia, wizara yangu ilitoa barua ya onyo ili kuvionya vikundi hivyo. Ni matumaini yetu kwamba barua hiyo iliwatanabahisha na kwa kiwango kikubwa vikundi hivyo vitajirekebisha.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake Afisi ya Mufti Pemba imezitembelea madrasa na vyuo vya Qurani katika Wilaya zote za Pemba na kutoa miongozo na ushauri katika kuendeleza elimu ya dini ya kiislamu. Aidha, mikutano minane inayohusu uhamasishaji na umuhimu wa utafiti katika dini ya Kiislamu imefanyika kwa lengo la kusisitiza umoja na kuondoa tofauti na mifarakano katika jamii. Afisi imeimarisha mawasiliano na taasisi za kidini ndani na nje ya nchi ambapo Masheikh kutoka nchi mbalimbali walitembelea Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mufti wa Zanzibar iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 198,263,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 128,036,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 70,227,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2011 fedha zilizopatikana ni Shilingi 133,348,574.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 96,906,308.00 (76%) ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 36,442,266.00 (52%) kwa matumizi mengineyo *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Afisi ya Mufti imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea Kujenga mahusiano na taasisi za kidini pamoja na kuweka Mfumo wa usimamizi na tathmini Unguja na Pemba;

ii. Kutayarisha na kuanza kutekeleza Mpango wa Kuimarisha Afisi ya Mufti kwa kuzingatia matokeo ya Utafiti wa vyombo vya dini;

iii. Kutekeleza Mpango wa Kudhibiti UKIMWI kwa njia za Kiislam; na

iv. Kuimarisha huduma za maktaba ya Kiislam na kituo cha kuhifadhia kumbukumbu za maulamaa.

Mhe. Naibu Spika**,** ili Afisi ya Mufti wa Zanzibar iweze kutekeleza kikamilifu malengo iliyojiwekea kwa mwaka ujao wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 338,324,000.00 kwa kazi za kawaida.

AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika**,** Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inahusika na shughuli za usajilli kwa mujibu wa Sheria zinazoongoza aina mbalimbali za usajili. Shughuli zinazosimamiwa na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ni pamoja na usajili wa taasisi za biashara, hati za mali za ubunifu, pamoja na usajili wa nyaraka mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao katika visiwa vya Zanzibar, zikiwemo za ndoa na talaka.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Afisi ya Mrajis wa Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza kazi zake za kawaida. Hadi kufikia Machi 2011, jumla ya vizazi 36,123 vimesajiliwa; wanaume 20,711 na wanawake 15,412. Kwa upande mwengine, jumla ya vifo 2,751 vimesajiliwa; wanaume 1,688 na wanawake 1,063 (*angalia kiambatanisho nam. 7a)*. Jumla ya ndoa 3,125 zilisajiliwa kupitia mashekh, lakini hakuna talaka zilizosajiliwa. Ndoa zilizosajiliwa mahakamani ni 125 na talaka 375. Natoa wito kupitia Baraza lako tukufu kuwahimiza wananchi kufanya usajili kwa wakati muafaka.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imesajili kampuni 139, majina ya biashara 271, alama za biashara 180, na Jumuiya za Kiraia 71. Vile vile, Afisi ya Mrajis ilisajili jumla ya nyaraka 738 za dhamana za Benki (A1), mauziano na urithi (A2), nyaraka za wakfu, hiba, kodi, kiapo na mikataba ya

uhaulishaji wa vyombo vya moto (A3) na waraka wa kufuta dhamana za Benki (A4).

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Afisi imeendelea na kazi za kuandaa mfumo mpya wa uimarishaji wa Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka pamoja na upatikanaji wa takwimu zake. Mradi huu umekusudia kufanya Mageuzi makubwa yatakayopelekea kufanya usajili kwa kompyuta. Mabadiliko haya yatarahisisha, siyo tu upatikanaji wa vyeti, bali pia taarifa za kitakwimu ambazo ni muhimu sana kwa Maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika**,** sambamba na kuajiri wataalamu kutengeneza mfumo mpya wa Usajili Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka, rasimu ya sheria imetayarishwa. Vile vile, vikao vya wadau juu ya matumizi ya nambari ya utambulisho wa mtu (Personal Identification Number - PIN) vilifanyika. Namba hii ya utambulisho itasaidia kuwatambua watu kirahisi. Wadau walioshiriki vikao hivyo ni pamoja na Wizara ya Elimu, Bodi ya Mapato Zanzibar, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Afisi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika**,** kazi ya kuratibu mageuzi ya mfumo wa utoaji wa leseni za biashara inaendelea. Kwa sasa mtaalamu anayefanya kazi hiyo tayari amekabidhi ripoti ya awamu ya tatu pamoja na rasimu ya sheria. Tayari Wizara imeanza kuifanyia kazi ripoti hiyo pamoja na rasimu ya sheria, na lengo letu ni kukamilisha shughuli hiyo katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, miswada ya sheria ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na ule wa Usajili wa Taasisi za Biashara tayari imekamilika na inatarajiwa kusomwa kwa mara ya kwanza katika Baraza lako tukufu. Rasimu za Miswada ya Sheria za Kampuni na Ufilisi tayari zimeshapitiwa na Kamati ya Uongozi ya Wizara. Rasimu hizo zimezingatia mapendekezo ya wadau, mahitaji ya wakati huu na uzoefu wa kimataifa ili kuhakikisha mafanikio ya utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha Usimamizi na Usajili wa Tasnia ya Mali za ubunifu, Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la kusimamia Mali Bunifu Duniani (WIPO) imefanikiwa kuurekebisha na

kuimarisha mfumo wa usajili wa hati za mali za ubunifu (Industrial Property Automation System - IPAS) kwa kuweka toleo jipya la mfumo huo. Mfumo wa awali ulisita kufanya kazi kutokana na matatizo mbalimbali yakiwemo ya uchakavu wa vifaa.

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 336,281,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 149,344,000.00 zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 186,937,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2011 fedha zilizopatikana ni Shilingi 275,488,464.00. Kati ya hizo, Shilingi 160,721,510.00 (108%) kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 114,761,954.00 (61%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 2,504,337,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za Maendeleo, zikiwemo Shilingi 90,000,000.00 kutoka Serikalini na Shilingi 2,078,056,000.00 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Fedha zilizopatikana ni Shilingi 30,000,000.00 kutoka serikalini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ilikadiria kukusanya Shilingi 263,415,000.00. Hadi kufikia Machi 2011, Shilingi 146,255,974.00 (55%) zilikusanywa *(viambatanisho vya 1& 3 vinahusika).*

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2012/2013, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha marekebisho ya mifumo ya usajili na sheria zinazoongoza usajili ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa tasnia ya mali za ubunifu; na

ii. Kuendeleza na kuimarisha Afisi kiutendaji na kuelimisha jamii juu ya shughuli mbalimbali za Afisi ya Mrajis Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha Afisi itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 265, 673,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 100, 000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi 109, 855,000.00.

AFISI YA MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO

Mhe. Naibu Spika, Afisi hii ni mpya. Kabla ya kuanzishwa kwake usajili wa vizazi na vifo ulikuwa ukisimamiwa na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Zanzibar. Afisi hii imeanza kazi baada ya kuteuliwa Mrajis wa Vizazi na Vifo

pamoja na Naibu wake. Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo Zanzibar kwa mujibu wa sheria ina majukumu mawili makuu. Kwanza kusajili Vizazi na Vifo, na pili kutunza kumbukumbu zitokanazo na usajili huo. Mbali na majukumu hayo, Afisi ina jukumu la kuishauri serikali juu ya masuala yote yanayohusiana na usajili wa vizazi na vifo.
Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2011/2012, Afisi ilikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa lililosababishwa na kukosekana kwa magamba ya kuchapishia vyeti hivyo. Ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara ilichukua hatua za dharura kwa kununua magamba 20,000 ya kuchapishia vyeti na kufanya kazi muda wa ziada kwa lengo la kuondosha mrundikano uliokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, ninayo furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa vyeti vilivyokuwa vimerundikana kusubiri hatua za kukamilisha vyote vimetiwa saini na watu wengi wamepata vyeti vyao. Wizara iliweka mpango maalum wa kutoa vyeti hivyo siku za Jumamosi na Jumapili, na kuwaarifu wananchi juu ya utaratibu huo kupitia vyombo vya habari. Pamoja na hatua hiyo, bado kuna vyeti ambavyo wenyewe hawajafika kuvichukua. Kupitia Baraza lako tukufu nawaomba wananchi ambao bado hawajachukua vyeti vyao, wafike Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, kwenye jengo la zamani la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), pamoja na afisi za wilaya Unguja na Pemba kwa kuchukua vyeti vyao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hatua nyengine zilizochukuliwa kuondosha tatizo la upatikanaji wa vyeti, ni kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Takwimu na Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, na Talaka. Mradi huu uliopata msaada kutoka shirika la *UNFPA* utaanza na majaribio katika wilaya mbili za mkoa wa Mjini Magharibi kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013. Majaribio ya awali ya mradi huu yameonesha uwezekano wa kupatikana cheti ndani ya kipindi kisichozidi wiki moja, baada ya kipande cha mtoto aliyezaliwa, (na taratibu nyengine muhimu) kuwasilishwa Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

v. Kutekeleza mpango wa mabadiliko katika mfumo wa usajili; na
vi. Kuimarisha Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kiutendaji katika utoaji wa huduma kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 305, 159,000.00 kwa matumizi ya kawaida, na Shilingi 3, 000, 000,000.00 kwa kazi za maendeleo, ukiwemo Mchango wa Serikali wa Shilingi 400, 000,000. Aidha, Afisi ya

Mrajis wa Vizazi na Vifo inakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi 416, 500,000.00.

AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar ina dhima kisheria ya kuhakikisha kuwa maslahi, hali, na hadhi za wabunifu wa Zanzibar zinaimarika kwa kupatiwa malipo yanayotokana na matumizi ya kazi zao kibiashara. Jukumu hilo linatekelezwa kwa kusajili kazi zao, kutoa leseni kwa matumizi halali ya kazi hizo kwa wanaozitumia kibiashara, pamoja na kukusanya na kugawa mirabaha kwa wasanii ambao kazi zao zimetumika katika maeneo mbalimbali. Vile vile, Afisi ya Hakimiliki inatekeleza majukumu yake kwa kutoa taaluma kwa wabunifu, watumiaji wa kazi za hakimiliki na jamii kwa ujumla, ili kuelewa matumizi halali na thamani ya kazi hizo kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake Afisi imeendesha vikao vya Bodi ya Hakimiliki Zanzibar ambavyo ndivyo vinavyotoa muongozo katika utekelezaji wa shughuli za Afisi. Aidha, imewapeleka mafunzoni maafisa wake watatu katika mafunzo ya ugawaji wa mirabaha kwa kutumia mfumo maalum wa Kimataifa wa *'WIPO Software for Collective Management of Copyright and Related Rights (WIPOCOS)'* wa kuhifadhi kumbukumbu za wabunifu na kazi zao pamoja na ugawaji wa mirabaha huko Dar es Salaam, katika Chama cha Hakimiliki Tanzania Bara. Vile vile, Afisi imeendelea na kazi zake za kawaida za usajili na kuweka kumbukumbu za kazi zilizosajiliwa na hatimaye kuingiza taarifa hizo katika mfumo wa *WIPOCOS*.

Aidha, kazi 141 za hakimiliki zilisajiliwa. Idadi hiyo inafanya jumla ya kazi zote za hakimiliki zilizosajiliwa kufikia 1,126 kuanzia mwaka 2007 kazi hiyo ilipoanza. Kwa uchambuzi wa kazi zilizosajiliwa, (angalia kiambatanisho nam. 7c).

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2012, Afisi imesambaza fomu za marejesho ya kazi za hakimiliki (*log sheets*) katika vituo vyote vya utangazaji vya umma na binafsi kwa lengo la kupata taarifa sahihi juu ya kazi zilizotumika na zenye kutoa mwelekeo wa ugawaji mirabaha kwa wahusika. Aidha, Afisi imetoa mafunzo kwa watangazaji na watayarishaji wa vipindi vya redio na televisheni juu ya umuhimu wa kujaza fomu za marejesho.

Vile vile, Afisi imeendelea na jitihada za kuwafanya watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara kutambua umuhimu wa kazi za hakimiliki kwa biashara zao na kukubali dhana ya ulipiaji wa matumizi ya kazi hizo kibiashara. Afisi imefanikiwa kutatua migogoro, ukiwemo mgogoro baina ya *Zanzibar One*

Modern Taarab na Culture Musical Club kuhusu umiliki wa nyimbo ya '*Tunapendana*'. Kazi nyengine zilizofanywa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria na kuandaa na kupitia mikataba ya wamiliki na watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, Afisi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, ilifanya msako ili kuwabaini wakwepaji wa malipo ya mirabaha kwenye maduka yanayokodisha kazi za hakimiliki, na kubaini vitendo vya uharamia wa kazi za hakimiliki. Katika msako huo uliofanyika Februari 2012, nakala haramu 6,525 za vinasa sauti na picha vya kielektroniki vilikamatwa. Wamiliki 44 wanaotuhumiwa kuuza kazi za hakimiliki kinyume na Sheria ya Hakimiliki (Nam. 14) ya mwaka 2003, wanatarajiwa kufikishwa Mahakamani. Aidha, msako huo ulibaini kiasi kikubwa cha usambazaji wa vinasa sauti na picha vya kielektroniki vinavyokiuka maadili.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa masuala ya hakimiliki, pamoja na kupambana na uharamia wa kazi za hakimiliki, Afisi imefanya mafunzo kwa maafisa hamsini wa Jeshi la Polisi Unguja, ambako kesi za uvunjaji wa hakimiliki zinaripotiwa kwa hatua za awali. Kwa mafunzo hayo, Jeshi la Polisi limeamua kuanzisha dawati la Hakimiliki (*Copyright Desk*), na kuteua askari wa usimamizi wa hakimiliki katika mikoa yote ya Zanzibar, pamoja na kuanzisha kikundi kazi cha hakimiliki kwa lengo la kuwa na ufuatiliaji mzuri wa masuala ya hakimiliki. Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Zanzibar, inaendesha vipindi vya kila wiki kwa ajili ya kuelimisha Umma. Jumla ya vipindi 13 vya redio vilirushwa hewani, ambapo sheria na masuala mbalimbali ya hakimiliki zilichambuliwa na kutolewa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, lengo la kuipitia na kuifanyia marekebisho Sheria ya Hakimiliki Nam. 14/2003 linatekelezwa kwa pamoja kati ya Afisi na Shirika la Milki Ubunifu Ulimwenguni (*World Intellectual Property Organisation - WIPO*). Katika hatua ya awali, Afisi imeainisha maeneo muhimu ya marekebisho na tayari yameshatumwa WIPO ambapo kazi ya kuandaa Mswada kwa kuingiza masuala mapya ya mikataba na makubaliano yaliyofikiwa ulimwenguni katika fani ya hakimiliki imeanza. Rasimu ya marekebisho itakapokamilika itafikishwa kwa wadau mbalimbali kupata maoni yao.

Mhe. Naibu Spika, Afisi inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo uelewa mdogo wa jamii na taasisi za serikali juu ya hakimiliki, mipaka ya uhalali wa matumizi ya kazi za hakimiliki, pamoja na mchango wa hakimiliki kwa uchumi wa nchi. Changamoto nyengine ni ufinyu wa bajeti, ufinyu wa nafasi za afisi, ukosefu wa maktaba yenye vifaa maalum kwa ajili ya kuhifadhi mali

za hakimiliki na usalama kwa watendaji. Changamoto hizi zinatafutiwa ufumbuzi ili kuweza kupata ufanisi zaidi katika kazi zetu.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iliidhinishiwa ruzuku ya Shilingi 100, 000,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 42, 625,392.00 kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 57, 374,608.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, fedha zilizopatikana ni Shilingi 64, 300,000.00. Shilingi 31, 859,310.00 (75%) kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 32, 440,690.00 (57%) kwa matumizi mengineyo *(Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Afisi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

vii. Kupunguza uharamia wa kazi za Hakimiliki;
viii. Kuendelea kuipitia na kuifanyia marekebisho Sheria ya Hakimiliki ili iweze kutumika katika mwaka huu wa fedha; na
ix. Kuelimisha jamii juu ya masuala ya Hakimiliki na umuhimu wake.

Mhe Spika, Ili Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/ 2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Ruzuku ya Shilingi 120, 000,000.00, kwa kazi za kawaida.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina wajibu wa kusimamia Mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa, Hijja, Zakka na Misaada ya kheri.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni imeendelea na kazi za usimamizi wa mali za wakfu na amana, na kwa mwaka 2011/2012 imezipitia na kuzifanyia uhakiki mali inazozisimamia ili kuwa na taarifa sahihi. Katika uhakiki huo, imebainika kuwa mali halisi inazozisimamia ni nyumba 260 za Wakfu, nyumba 29 za Amana, mashamba manne na vikataa tisa vya Wakfu kwa Unguja na Pemba. Katika kuzitunza mali hizo, msikiti na nyumba tisa zimefanyiwa matengenezo, na mashamba mawili yamefanyiwa usafi na kupandwa miti mbalimbali. Jumla ya Shilingi 57, 252,600.00 zilitumika.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni imefanya utafiti wa kuzitambua nyaraka zilizopotea, kujua wasia wa wakfu hizo, pamoja na kuwatambua wanufaika halali. Katika utekelezaji wa kazi hiyo, nyaraka 1,053 zimepatikana na wasia 68 zimetafsiriwa na sasa zinahakikiwa ili zifanyiwe kazi. Kazi ya utafiti

inaendelea. Katika kuhakikisha usimamizi bora wa mali za Wakfu, watendaji wa Kamisheni walifanya ziara za kimasomo Shirika la Nyumba la Taifa *NHC*, Taasisi ya Nyaraka na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni imeongeza juhudi ya kuhakikisha kuwa wapangaji wanalipa kodi kwa mujibu wa soko, pamoja na kulipa madeni. Kutokana na juhudi hiyo, jumla ya Shilingi 203, 144,425.00 zimekusanywa Unguja, na Shilingi 26, 837,200.00 Pemba, ikiwa ni malipo ya madeni na kodi. Fedha hizo tayari zimegaiwa kwa wanufaika.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni imeendelea kutoa huduma za Mirathi kwa watu mbalimbali. Jumla ya *tirka* mpya 435 zimefunguliwa Unguja na tirka 73 zimefunguliwa Pemba. Aidha, tirka 344 zenye thamani ya Shilingi 1, 716, 782,295.75 zimefungwa Unguja na tirka 96 zenye thamani ya Shilingi 448, 124,343.15 zimefungwa Pemba. Sambamba na hayo Kamisheni imefanya mapitio ya kumbukumbu za mirathi na kubaini kuwepo kwa warathi ambao hawajachukua haki zao.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2012, Mafaili ya mwaka 2000, 2001, 2002 na 2004 tayari yameshapitiwa. Katika uhakiki wa mafaili ya mwaka 2000 imegundulika kuwa wanufaika wa mafaili 87 kati ya 383 hawajachukua haki zao kwa kutokamilisha taratibu. Hatua za kuwasiliana na wahusika zimechukuliwa kupitia njia mbalimbali zikiwemo matangazo na masheha, ili taratibu za mirathi zikamilishwe na wahusika wapatiwe haki zao.

Mhe. Naibu Spika, katika kurithisha mali za marehemu mara nyengine hujitokeza mizozo. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2011/2012, jumla ya mizozo 20 imesuluhishwa na mizozo 12 inaendelea kutafutiwa ufumbuzi. Vile vile, kesi 29 zimeshughulikiwa na Kamisheni katika Mahkama mbalimbali za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya uratibu wa safari za Hijja imeendelea vizuri. Jumla ya Mahujaji 2,118 walitekeleza ibada hiyo mwaka 2011/2012, ambapo mahujaji 996 walisafiri kupitia vikundi vya Zanzibar, kama inavyoonesha katika *kiambatanisho nam. 8*. Katika Mwaka wa Fedha 2012/13, Kamisheni imejipanga kuimarisha huduma na uratibu wa Shughuli za Hijja. Aidha, Sala na Mabaraza ya Iddi yameyaratibiwa vyema. Azma ya Serikali ni kuifanya Sala na Baraza la Idd El Hajj liwe linazunguka kimaeneo.

Mhe. Naibu Spika, mfumo wa shughuli za Zakka uko katika hatua nzuri. Akaunti maalum ya Zakka imefunguliwa katika Benki ya Kiislamu ya PBZ na tayari zakka imeshaanza kupokelewa na kugaiwa. Tunatoa wito kwa Waislamu wote Zanzibar na wale walio nje ya Zanzibar kutimiza wajibu wao wa kutoa Zakka na sadaka, kwa madhumuni ya kujitakasa wao na kuwasaidia

watu wanaohitaji misaada. Kamisheni kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kidini imeendelea kufanikisha upatikanaji wa misaada ya kheri na ugawaji wa misaada hiyo kwa jamii. Siku zote tunaaidhiwa kutoa moja ili *Allah* atulipe kumi. Tuchangamkieni hayo kwa faida ya hapa duniani na kesho akhera twendako.

Mhe. Naibu Spika, hapa niwatanabahishe wananchi kuwa mali za Wakfu sio za Serikali. Ni mali za waumini walizozikabidhi kwa Mwenyezi Mungu na kuwekwa dhamana kwetu sisi. Kwa maana hiyo, tunatakiwa sisi na wapangaji kuyaona hayo na kusaidia wasia wa walioweka wakfu hizo utekelezeke. Ule mtindo wa baadhi ya wapangaji wanaozikodisha nyumba hizo mara nne au tano zaidi ya bei waliyokodishiwa au kuchukua vilemba ni sawa na kuwaibia au kuwanyang'anya wanufaika wa wakfu hizo. Mwenyezi Mungu hayuko radhi nao kwa hilo, na sisi tuliopewa jukumu la kulinda mali hizo tutakapogundua udhalimu huo, tutachukua hatua kali kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kuwa Wizara yangu imepandisha kodi za nyumba za wakfu ili zilingane na hali ya soko. Hali hii imezingatia kuhifadhi mali zenyewe na kuwezesha utekelezwaji wa wasia za wale walioweka wakfu. Ifahamike kuwa wanufaika wa wakfu sio wapangaji, bali ni wale ambao kila muweka wakfu huagiza wanufaike wakiwemo mayatima, masikini, Misikiti, wagonjwa, madrasa na shughuli nyengine za kheri. Hata hivyo, pamoja na kuongezwa bei hizo bado zingali chini ukilinganisha na hali ya soko.

Mhe. Naibu Spika, kodi ya nyumba ya ghorofa yenye vyumba zaidi ya vitatu, imeongezwa kutoka Shilingi 35,000 hadi Shilingi 100,000.00, lakini bado kuna malalamiko ya kutaka kupunguzwa kwa kodi hiyo. Huku ni kufisidi kwa makusudi mali na malengo ya Wakfu. Ni vyema tukubali kubadilika. Ninawakumbusha ile kauli ya *Sayyidna Omar bin Khatwab* aliposema "*Ni vyema kuiendea haki iliyokudhihirikia kuliko kudumu katika batili uliyoizowea"*.

Mhe. Naibu Spika, ili kuongeza viwango vyao vya elimu, jumla ya wafanyakazi saba wa Kamisheni walipelekwa masomoni na wafanyakazi wawili waliendelea na masomo katika fani mbalimbali. Vile vile, wafanyakazi 32 walinufaika na mafunzo ya ndani katika fani za urithi, wakfu, usuluhishi wa mizozo, kompyuta na uandishi wa ripoti (*angalia kiambatanisho nam. 9b*).

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Kamisheni iliidhinishiwa ruzuku ya jumla ya Shilingi 300,000, 000.00. Hadi kufikia Machi 2012 fedha zilizoingizwa ni Shilingi 281, 579,831.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 160, 832,739.00 (57%) zilitumika kulipa mishahara na Shilingi

120, 747,092.00 (43%) zilitumika kwa matumizi mengineyo, kama kinavyoonesha kiambatanisho namba 1.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha Kamisheni imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendeleza uimarishaji wa Mfumo wa Ukusanyaji na Ugawaji wa Zakka na Sadaka;
ii. Kuendeleza Mfumo bora wa usimamizi wa mali za Wakfu na Amana; na
iii. Kuimarisha Mfumo wa Utendaji na Uratibu.

Mhe. Naibu Spika, ili kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Ruzuku ya Shilingi 460,000,000.00 pamoja na makusanyo na matumizi ya shilingi 179,000,000.00 yanayotokana na mapato ya ndani.

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika, Afisi Kuu Pemba ni kiungo kikuu katika kusimamia shughuli za utendaji wa Wizara pamoja na taasisi zake Kisiwani Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Afisi Kuu Pemba imeweza kutekeleza majukumu yake ya kusimamia shughuli za Wizara katika utekelezaji wa malengo yake Pemba kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, Afisi imetembelea Idara zote za Wizara zilizoko Pemba kuhamasisha utendaji kazi na uwajibikaji, pamoja na kufanya mikutano ya robo mwaka. Afisi Kuu Pemba kupitia kitengo chake cha Jumuia za Kiraia imezihakiki baadhi ya Jumuia za Kiraia kwa lengo la kuzitambua na kuziorodhesha katika daftari la usajili wa Jumuia. Aidha, Afisi imefanya mkutano wa uhamasishaji kuhusu usawa wa kijinsia kwa baadhi ya maafisa wa wizara.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na shughuli hizo, Afisi imelifanyia matengenezo jengo lake lililopo Chake Chake na kununua samani pamoja na baadhi ya vifaa vya kufanyia kazi. Katika kuwaendeleza wafanyakazi wake kwa ajili ya kuwafanya wamudu vizuri zaidi majukumu yao, wafanyakazi watatu wamepatiwa nafasi za mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi Kuu Pemba, ilikadiria kutumia Shilingi 282,350,000.00 kwa kazi za kawaida, ambapo Shilingi 182,178,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 100,172,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kufikia Machi 2012 jumla ya Shilingi 168,972,438.00 zilikuwa zimepatikana, ambapo Shilingi

110,613,180.00 (61%) zimetumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 58,359,258.00 (58%) zimetumika kwa matumizi mengineyo *(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Afisi Kuu - Pemba inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

x. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba, zikiwemo shughuli za Jumuia za Kiraia;
xi. Kuimarisha mazingira ya kazi, na kuwaendeleza wafanyakazi wa Wizara Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ili Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyotarajiwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 165, 331,000.00 kwa ajili ya kazi za kawaida.

MAREKEBISHO YA KATIBA

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu imo katika hatua muhimu kwa khatma yetu na ya vizazi vyetu, ambao inahusu ukusanyaji maoni kwa ajili ya kuandika upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kila mwananchi wa Zanzibar ana uhuru wa maoni kikatiba [Kif. 18(1) cha Katiba ya Zanzibar], lakini maoni hayo yasikiuke mipaka kwa kukera mwananchi mwengine au kuvuruga maslahi ya umma kif 24(1). Kwa maana hiyo, mtu anaweza, akipenda, kusema anataka nini kirekebishwe katika muungano huo. Jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa maoni yake ni kwa maslahi ya Zanzibar na Wazanzibari. Kimsingi, lengo letu ni kuifanya Zanzibar kuwa na haki na uhuru wake kamili ndani ya Muungano wetu, lengo ambalo litaifanya Zanzibar kutekeleza mambo yake ya kimaendeleo bila ya kuingiliwa.

Mhe. Naibu Spika, kazi hii ni ya wananchi wenyewe, na wala si ya Wizara ya Katiba au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kazi ya Serikali kupitia Wizara hii, ni kusimamia yale yote ambayo wananchi watayapendekeza katika katiba hiyo. Wizara yangu inawahakikishia Wazanzibari kuwa itaendelea kutoa ufafanuzi kuhusu matakwa ya Katiba zetu mbili, ya Jamhuri ya Muungano na ya Zanzibar pale ambapo itahitajika. Wizara yangu imegawa Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika kila wilaya kwa kupitia Wakuu wa Mikoa. Katiba hizo ni kidogo na hazitoshi, lakini pale tutakapozipata nyengine basi pia tutaendeleza kuzigawa.

MALENGO YA JUMLA YA WIZARA

Mhe. Naibu Spika, Wizara itaendelea kupambana na tatizo la ucheleweshaji wa kesi katika mahkama zetu na kuhakikisha matatizo ya wananchi katika

usimamizi na ufuatiliaji wa haki zao yanapungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, kuhusu ucheleweshaji wa vyeti, Wizara itaendeleza ushirikiano kwa kuwaelimisha zaidi watendaji wa Wilayani na Masheha, ili kuhakikisha vyeti vya kutosha vinapatikana kwa wakati. Vile vile, Wizara itaendelea kushirikiana na Idara ya Uchapaji kuhakikisha upatikanaji wa magamba ya kutosha ya vyeti kwa wakati muafaka.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo niliyoyatoa hapo juu, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutoa kwa muhtasari mwelekeo wa malengo ya utekelezaji ambayo Wizara imedhamiria kuyatekeleza kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kama ifuatavyo:-

1. Kukuza utoaji wa huduma bora kwa jamii;
2. Kukuza upatikanaji wa haki;
3. Kukuza uwazi na ushirikishwaji wa wananchi katika mambo mbalimbali;
4. Kukuza uratibu na usimamizi wa shughuli za Wizara;
5. Kuwajengea uwezo watendaji ili waweze kumudu vyema zaidi kazi zao; na
6. Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya Taasisi za Wizara na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya sheria.

MIRADI YA WIZARA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Wizara ya Katiba na Sheria itatekeleza miradi kumi ya maendeleo. Minane kati ya hiyo ni miradi inayoendelea na miwili ni miradi mipya. Miradi inayoendelea ni:-

Ujenzi wa Jengo la Wizara ya Katiba na Sheria; Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria; Mpango wa Kurekebisha Mfumo wa Usajili wa Kampuni za Biashara na Kuimarisha Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali; Mradi wa Uimarishaji Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka pamoja na Upatikanaji wa Takwimu zake; Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; Mradi wa Kuimarisha Majengo ya Mahkama; Mradi wa Uanzishwaji wa Mahkama ya Biashara; na Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Miradi miwili mipya ni:-

Mradi wa Kuzijengea Uwezo Taasisi za Wizara na Mradi wa Mapitio ya Sheria za Zanzibar (*Kiambatanisho nam. 4 kinahusika)*.

SHUKRANI

Mhe. Naibu Spika, Napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiwasilisha Hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, shukurani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu. Vile vile, nawashukuru Watendaji Wakuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa jinsi wanavyoonesha mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu yao ya kazi. Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza hili, kwa michango yao yenye manufaa kwa Wizara na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Wizara imekuwa ikifanya kazi zake kwa mashirikiano na washirika wa maendeleo mbalimbali. Kwa heshima na taadhima naomba uniruhusu niwashukuru wale wote wanaotusaidia wakiwemo *UNDP*, *ADB*, *WIPO*, *WTO*, Shirika la Mali Bunifu la Afrika (*ARIPO*), Benki ya Dunia, *UNFPA*, Norway, Sweden, Jumuia ya Ulaya, African Muslim Agency, Benki ya Maendeleo ya Kiislam (*IDB*), *Save the Children*, Vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano zikiwemo Mahkama, Tume ya Kurekebisha Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Serikali ya Saudi Arabia, Serikali ya Algeria, Tume ya Kurekebisha Sheria ya Uganda, *Zanzibar Legal Services Centre*, vikundi mbalimbali vilivyosafirisha Mahujaji, na Jumuia na Taasisi mbalimbali za kidini Zanzibar.

HITIMISHO:

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia, ili wizara yangu iweze kutekeleza malengo yake vyema, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na baadaye waidhinishe matumizi ya shilingi 7,591,000,000/= ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 kwa kazi za kawaida, na shilingi 6,682,200,000/= kwa kazi za maendeleo.

Kati ya fedha hizo, shilingi 3,455,000,000/= ni kutoka serikalini na 3,227,200,000/= kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kiasi hiki, ni ongezeko kwa karibu asilimia 36.8% ya fedha ambazo wizara yangu iliidhinishiwa na Baraza lako tukufu kwa mwaka 2011/2012.

Vile vile, naliomba Baraza lako liikubalie Wizara yangu ichangie shilingi 598,355,000/= kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, wizara hapa imekisia ongezeko la asilimia 92 ambazo tunahisi tutazifikia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hivyo kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha na Matumizi, 2011/2012

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
Afisi ya Mufti wa Zanzibar	Mishahara na Stahiki za watumishi	128,036,000	96,027,000	96,906,308	31,129,692	76%
	Matumizi Mengineyo	70,227,000	59,541,500	36,442,266	33,784,734	52%
	Jumla	***198,263,000***	***155,568,500***	***133,348,574***	*64,914,426*	*67%*
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara na Stahiki za watumishi	-		-	-	
	Matumizi Mengineyo	74,554,000	71,524,000	53,046,050	24,790,950	71%
	Jumla	***74,554,000***	***71,524,000***	***53,046,050***	**24,790,950**	**71%**
	Maendeleo Serikali	50,000,000	50,000,000	30,000,000	20,000,000	60%

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
	Maendeleo DP - UNDP		93,324,440	93,324,440		
	Jumla Maendeleo	**50,000,000**	**143,324,440**	**123,324,440**	**20,000,000**	247%
	Jumla Kuu	**124,554,000**	**214,848,440**	**173,087,490**	-51,816,490	142%
Afisi ya Hakimiliki	Mishahara na Stahiki za watumishi	42,625,000	31,969,044	31,859,310	10,765,690	75%
	Matumizi Mengineyo	57,375,000	46,202,500	32,440,690	24,934,310	57%
	Jumla	***100,000,000***	*67,980,932*	***64,300,000***	35,700,000	64%
Afisi ya Mrajis Mkuu	Mishahara na Stahiki za watumishi	149,344,000	160,721,510	160,721,510	-11,377,510	108%
	Matumizi Mengineyo	186,937,000	85,399,044	114,761,954	72,175,046	61%
	Jumla	***336,281,000***	*246,120,554*	***275,483,464***	60,797,536	82%
	Maendeleo Serikali	90,000,000	90,000,000	30,000,000	60,000,000	33%
	Maendeleo	2,078,056,000	2,078,056,001	-	2,078,056,000	0%

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
	DP					
	Jumla Maendeleo	***2,168,056,000***	***2,168,056,000***	***30,000,000***	**2,138,056,000**	1%
	Jumla Kuu	***2,504,337,000***	***2,414,176,555***	***305,483,464***	2,198,853,536	12%
	Makusanyo	263,415,000	197,561,250	146,255,974	117,159,026	56%
Idara ya Utumishi na Uendeshaji	Mishahara na Stahiki za watumishi	220,442,000	247,018,565	247,018,565	-26,576,565	112%
	Matumizi Mengineyo	218,110,000	184,209,000	159,163,163	58,946,837	73%
	Jumla	***438,552,000***	*262,435,588*	***406,181,728***	32,370,272	93%
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	Mishahara na Stahiki za watumishi	217,544,000	224,418,859	224,418,859	- 6,874,859	103%
	Matumizi Mengineyo	82,456,000	197,685,000	77,938,918	4,517,082	95%
	Jumla ruzuku	***300,000,000***	***422,103,859***	***302,357,777***	2,357,777	101%
	Makusanyo	166,884,000			166,884,000	0%
	Jumla Kuu	**466,884,000**			466,884,000	0%

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
Afisi Kuu Pemba	Mishahara na Stahiki za watumishi	182,178,000	110,613,180	110,613,180	71,564,820	61%
	Matumizi Mengineyo	100,172,000	58,359,258	58,359,258	41,812,742	58%
	Jumla	***282,350,000***	*168,972,438*	***168,972,438***	113,377,562	60%
Mahkama	Mishahara na Stahiki za watumishi	724,000,000	1,335,527,219	1,335,527,219	- 611,527,219	184%
	Matumizi Mengineyo	600,000,000	444,611,000	507,175,000	155,389,000	97%
	Jumla	*1,324,000,000*	*1,780,138,219*	*1,780,138,219*	- 456,138,219	134%
	Maendeleo Serikali	300,000,000	300,000,000	280,000,000	20,000,000	93%
	Maendeleo DP	1,389,696,480	1,274,696,480	66,148,000	1,323,548,000	5%
	Jumla Maendeleo	1,689,696,000	1,574,696,480	346,148,000	1,343,548,000	20%
	Jumla Kuu	**3,013,696,000**	**3,354,834,699**	**2,126,286,219**	887,409,781	**71%**
	Makusanyo	48,000,000	36,000,000	63,230,873	-15,230,873	132%

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	Mishahara na Stahiki za watumishi	137,216,000	102,912,072	137,224,773	-8,773	100%
	Matumizi Mengineyo	474,861,000	370,412,200	371,126,000	103,735,000	78%
	Jumla	*612,077,000*	*473,324,272*	*508,350,773*	103,726,227	83%
	Maendeleo Serikali	-	-	212,412,000	212,412,000	
	Maendeleo DP - UNDP	1,576,329,000	-	-	1,576,329,000	0%
	Jumla Maendeleo	*1,576,329,000*	-	*212,412,000*	1,363,917,000	13%
	Jumla Kuu	**2,188,406,000**	**473,321,200**	**707,908,773**	1,480,497,227	**32%**
Tume ya Kurekebisha Sheria	Mishahara na Stahiki za watumishi	59,457,000	44,592,750	46,671,363	12,785,637	78%
	Matumizi Mengineyo	115,457,000	94,497,000	115,457,000	-	100%
	Jumla	*174,914,000*	*139,089,750*	*162,128,363*	12,785,637	93%
Afisi ya Mkurugenzi wa	Mishahara na Stahiki za	324,000,000	297,153,025	297,153,025	26,846,975	92%

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
Mashtaka	watumishi					
	Matumizi Mengineyo	400,000,000	350,000,000	321,897,000	78,103,000	80%
	Jumla	*724,000,000*	*647,153,025*	*619,050,025*	104,949,975	86%
	Maendeleo Serikali	250,000,000	220,000,000	200,000,000	50,000,000	80%
	Maendeleo DP	284,000,000	284,000,000	95,580,585	234,000,000	34%
	Jumla Maendeleo	534,000,000	504,000,000	250,000,000	284,000,000	55%
	Ruzuku	50,000,000	44,000,000	43,800,000	6,200,000	88%
	Jumla Kuu	***1,308,000,000***	***1,195,153,025***	***958,430,610***	***349,569,390***	***73%***

MUHTASARI WA BAJETI WA WIZARA	BAJETI 2011/12	ZILIZOTENGWA JULAI-MACHI 2011/2012	ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI 2011/2012	SALIO ZILIZOTENGWA KWA MWAKA	%
Jumla Mishahara	2,184,842,000	2,650,918,322	2,688,114,112	513,135,112	123%
Jumla Matumizi Mengine	2,380,149,000	1,962,440,502	1,785,243,299	594,905,701	75%
Jumla ya Wizara (Mishahara, Stahiki za watumishi na OC)	4,564,991,000	4,434,376,235	4,473,357,411	91,633,589	98%
Maendeleo SMZ	690,000,000	660,000,000	540,000,000	150,000,000	78%
Jumla ya Wizara Maendeleo DPs	5,328,081,000	3,730,076,921	255,053,025	5,073,027,975	5%
Jumla Maendeleo	6,018,081,000	4,390,076,921	795,053,025	5,223,027,975	13%
Jumla Kuu ya Wizara	10,633,072,000	8,868,453,155	5,524,622,436	5,108,449,564	52%
Jumla Makusanyo	311,415,000	233,561,250	209,486,847	101,928,153	67%
Jumla Ruzuku	450,000,000	534,084,791	410,457,777	39,542,223	91%

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2012/2013

FUNGU/IDARA	KAZI ZA KAWAIDA					KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI ZA WATUMISHI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	MCHANGO WA SERIKALI	WAHISANI	JUMLA FEDHA ZA MA
14 - Mahkama Kuu	3,145,000,000	2,352,000,000	793,000,000	2,301,020,000	43,980,000	600,000,000		
15 - Mwanasheria Mkuu wa Serikali	802,000,000	197,000,000	605,000,000	-		1,800,000,000	0	
46 - Tume ya Kurekebisha Sheria	271,000,000	94,000,000	177,000,000		-	145,000,000	0	
35 - Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	879,000,000	411,000,000	468,000,000	685,800,000	193,200,000	250,000,000	0	
36/03 - Afisi Kuu Pemba	165,331,000	80,159,000	85,172,000	-	165,331,000	0	0	
36/04 - Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	172,860,000	83,306,000	89,554,000	172,860,000	-	160,000,000	627,200,000	
36/05 - Afisi ya Mufti wa Zanzibar	338,324,000	235,298,000	103,026,000	249,741,000	88,583,000	0	0	

FUNGU/IDARA	KAZI ZA KAWAIDA					KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI ZA WATUMISHI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	MCHANGO WA SERIKALI	WAHISANI	JUMLA FEDHA ZA MA
36/06 - Idara ya Utumishi na Uendeshaji	566,653,000	314,343,000	252,310,000	566,653,000	-	0	0	
36/11Mrajis Mkuu	265,673,000	115,674,000	149,999,000	249,674,000	15,999,000	100,000,000		
36/901 - Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo	305,159,000	134,222,000	170,937,000	231,021,000	74,138,000	400,000,000	2,600,000,000	
Ruzuku - DPP	100,000,000	30,000,000	70,000,000	-	-	0	0	
Ruzuku - Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	460,000,000	291,280,000	168,720,000	364,135,000	95,865,000	0	0	
Ruzuku-Afisi ya Hakimiliki	120,000,000	39,548,000	80,452,000	120,000,000	-	0	0	
JUMLA VOTE 36 + Ruzuku	**2,394,000,000**	**1,309,130,052**	**1,084,869,948**	**1,954,084,000**	**439,916,000**	**660,000,000**	**3,227,200,000**	**3,887,200,000**
JUMLA VOTE 36	**1,814,000,000**	**963,002,000**	**850,998,000**	**1,469,949,000**	**334,051,000**	**660,000,000**	**3,227,200,000**	**3,887,200,000**
JUMLA KUU	**7,591,000,000**	**4,393,130,052**	**3,197,869,948**	**4,940,904,000**	**1,477,096,000**	**3,455,000,000**	**3,227,200,000**	**6,682,200,000**

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato na Makadirio ya 2012/2013

IDARA/TAASISI	MAKADIRIO 2011/2012	MAKUSANYO HALISI 2011/12	%	MATARAJIO JUNI 2011	JUMLA HADI JUNI 2011	%	MAKADIRIO 2012/2013
36/11**MRAJIS MKUU WA SERIKALI**	263,415,000	146,255,974	55.5%	85,941,302	232,197,276	88%	109,855,000
14**MAHKAMA**	48,000,000	63,230,873.00	131.7%	69,930,573	133,161,446	277%	72,000,000
36/902 **MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO**	0	0	0%	0	0	0%	416,500,000
JUMLA KUU	**311,415,000**	**209,486,847**	67.3%	**155,871,875**	**365,358,722**	117%	**598,355,000**

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2012 – 2013

Nam. ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Mchango wa Wahisani	Mhisani	Jumla Kuu
74017	Ujenzi wa Jengo la Wizara ya KS	0			0
74018	Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria	60,000,000	627,200,000	UNDP	687,200,000
72201	Kurekebisha mfumo wa Usajili wa Kampuni ya Biashara na Kuimarisha Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	100,000,000	0		100,000,000
74019	Mradi wa Mageuzi katika Usajili waTakwimu za Vizazi na Vifo	400,000,000	2,600,000,000		3,000,000,000
72212	Mradi wa kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	250,000,000			250,000,000
72234	Kuimarisha Mahkama Kuu	271,800,000	0		271,800,000
72239	Uanzishwaji wa Mahkama ya Biashara	328,200,000	0		328,200,000
72185	Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu	1,800,000,000	0		1,800,000,000
	Mradi wa Kuzijengea Uwezo Taasisi za Wizara	100,000,000	0		100,000,000

Nam. ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Mchango wa Wahisani	Mhisani	Jumla Kuu
	Mradi wa Mapitio ya Sheria za Zanzibar	145,000,000	0		145,000,000
	JUMLA KUU	**3,455,000,000**	**3,427,200,000**		**6,682,200,000**

Kiambatanisho 5a: Ufunguaji wa Kesi Mahkamani Julai 2011 hadi Machi 2012

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama ya	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Rufaa	2	2	0	0	0	0	0	0	0
M/Kuu Vuga	83	48	0	12	0	14	0	9	4
M/Kuu Pemba	24	1	0	1	1	21	0	1	1
Kazi	16	16	1	0	0	0	0	0	0
Kadhi wa Rufaa Unguja	44	44	4	0	0	0	0	0	0
Kadhi Rufaa Pemba	4	0	0	0	0	4	1	0	0
Mkoa Vuga	136	28	3	92	13	11	0	5	0
Mkoa Mfenesini	77	4	0	72	6	1	0	0	0
Mkoa Mwera	72	6	6	57	49	4	4	5	2
Mkoa Wete	63	4	0	55	35	1	0	3	0

Kiambatanisho 5a: Ufunguaji wa Kesi Mahkamani Julai 2011 hadi Machi 2012

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama ya	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mkoa Chake	59	2	0	55	2	2	0	0	0
Wilaya Mw/kwe	532	44	3	488	245	0	0	0	0
Wilaya Mwera	405	4	4	400	228	1	1	0	0
Wilaya Mkokotoni	505	8	4	497	393	0	0	0	0
Wilaya Mfenesini	218	2	0	211	115	2	2	3	0
Wilaya Makunduchi	80	0	0	79	26	1	0	0	0
Wilaya Mkoani	66	1	0	65	41	0	0	0	0
Wilaya Chake	74	4	0	64	41	0	0	0	0
Wilaya Wete	98	0	0	98	27	0	0	0	0

Kiambatanisho 5a: Ufunguaji wa Kesi Mahkamani Julai 2011 hadi Machi 2012

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama ya	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Wilaya Konde	92	0	0	92	35	0	0	0	0
Watoto Vuga	19	0	0	19	19	0	0	0	0
Watoto Mwera	20	0	0	7	7	0	0	5	1
Watoto Mfenesini	20	0	0	20	7	0	0	0	0
Watoto Chake	6	0	0	6	0	0	0	0	0
Watoto Wete	7	0	0	7	0	0	0	0	0
Jumla	**2714**	**218**	**25**	**2397**	**1255**	**64**	**8**	**35**	**8**

Kiambatanisho 5b: Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo na Kadhi

Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo						**Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Kadhi**		
Mahkama ya Mwanzo	**Kesi za Madai**			**Kesi za Jinai**		**Mahkama za Kadhi Wilaya**	**Kesi za Madai**	
	Jumla	**Zilizo funguliwa**	**Zilizo tolewa uamuzi**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizotolewa uamuzi**		**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa uamuzi**
Manispaa Malindi	419	0	0	0	0			
Mwanakwerekwe	159	20	3	139	37	Mjini	644	131
Mwera	260	8	8	252	114	Mwera	23	11
Makunduchi	131	10	4	121	64	Mfenesini	40	20
Chwaka	79	5	4	74	49	Mkokotoni	46	21
Mfenesini	178	0	0	178	160	Makunduchi	20	0
Mkokotoni	188	38	10	150	100	Chwaka	2	0
Mkoani	79	8	1	71	22	Mkoani	41	10
Kengeja	11	1	1	10	6	Kengeja	6	0
Chake chake	94	11	2	83	35	Chake chake	48	9
Wete	81	9	0	72	29	Wete	50	2
Konde	114	10	1	104	86	Konde	50	6
Jumla	**1793**	**120**	**34**	**1673**	**1057**	**Jumla**	**970**	**217**

Kiambatanisho 5c: Vituo vya Kazi - Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

1	Makao Makuu ya Afisi - Miembeni (Uwanja wa Matumbaku)
2	Kitengo Cha Mashtaka - Mahkama Kuu - Vuga
3	Afisi ya Waendesha Mashtaka, Mahkama za Wilaya - M"kwe
4	Kitengo Cha Mashtaka - Mahkama ya Mkoa - Mfenesini
5	Kitengo Cha Mashtaka - Mahkama ya Mkoa - Mwera
6	Afisi Kuu - Chake Chake Pemba
7	Kitengo Cha Mashtaka - Mahkama ya Mkoa - Wete
8	Kitengo Cha Mashtaka - Mahkama ya Mkoa - Mkoani
9	Kitengo Cha Mashtaka - Mahkama ya Mkoa - Konde

Kiambatanisho 6: Miswada - Afisi ya Mwanasheria Mkuu 2011/2012

a. Miswada ya Sheria iliyoandaliwa
i. Mswada wa kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu;
ii. Mswada wa kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara
iii. Mswada wa kurekebisha baadhi ya Sheria;
iv. Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi
v. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar.

vi. Mswada wa Tume ya Mipango ya Zanzibar.
vii. Mswada wa sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.
viii. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii
ix. Mswada wa sheria ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma.
x. Mswada wa Sheria ya Chuo cha Utafiti wa Kilimo.
xi. Mswada wa sheria ya Baraza la kipimo na Tathimini ya Elimu.

b. Machapisho katika Gazeti Rasmi la Serikali
i. Milk Regulations; 2011
ii. The labour Regulatios (Mediation and Arbitration) Regulations; 2011;
iii. The lodated salt Regulations, 2011;
iv. Kanuni za kusimsmia huduma, 2011
v. Kanuni za Uhaulishaji Ardhi
vi. The Re-establishiment of Business Council, 2011;
vii. Kanuni za kuweka Utaratibu wa maombi ya Uingizaji, Usafirishaji na Upitishaji wa Bidhaa, 2011
viii. The Zanzibar Investment Promotion Authority Financial Regulations 2011
ix. The Zanzibar Investment Promotion Authority Financial Regulations 2011
x. The Zanzibar Broadcasting Corporation Establishment Order, 2011
xi. The Plastic Bag (Banning)Regulation, 2011
xii. The Goods and Services Regulations, 2011
xiii. The Regulations For Licensing and Controlling Use of Chain saw, 2011
xiv. The Private Employment Agents Regulations, 2012
xv. The labour Advisory Board Regulatios, 2012

Kiambatanisho 7a: Vizazi na Vifo vilivyosajiliwa kiwilaya

Wilaya	Vizazi			Vifo		
	wanawake	**wanaume**	**Jumla**	**wanawake**	**wanaume**	**Jumla**
Mjini	5,812	6,150	11,962	514	491	1005
Magharibi	1,549	1,663	3,212	187	172	359
Kaskazini A	1,489	1,468	2,957	90	99	189
Kaskazini B	1,186	1,167	2,353	33	18	51
Kusini	1,039	979	2,018	51	36	87
Kati	688	673	1,361	15	25	40
Jumla Unguja	***11,763***	***12,089***	***23,863***	***890***	***841***	***1,731***
Wete	1,579	1,558	3,137	84	93	177
Micheweni	1,885	2,005	3,890	99	96	195
Chakechake	1,372	1,090	2,462	135	195	330
Mkoani	1,384	1,387	2,771	165	153	318
Jumla Pemba	***6,220***	***6,040***	***12,260***	***483***	***537***	***1,020***
JUMLA KUU	**17,983**	**18,129**	**36123**	**1,373**	**1,378**	**2,751**

Kiambatanisho 7b: Mapato - Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali 2011/2012

KASMA	ENEO LA MAPATO	ZILIZOIDHINISHWA	ZILIZOKUSANYWA HADI FEBRUARI	MAPATO YA MWEZI MACHI	ZILIZOPATIKANA HADI MACHI	PUNGUFU/ ZIADA
114602	Estate Duty	510,000	396,000	-	396,000	114,000
142207	Usajili Vizazi na Vifo	153,000,000	59,112,550	8,639,500	67,752,050	85,247,950
142208	Usajili Ndoa na Talaka	18,360,000	12,600,500	850,000	13,450,000	4,909,500
142233	Usajili Alama za Biashara	31,620,000	14,750,000	2,515,000	17,265,000	14,355,000
142234	Usajili Kampuni	36,720,000	15,596,570	3,170,700	18,767,270	17,952,730
142235	Usajili Majina ya Biashara	14,280,000	10,764,000	928,000	11,692,000	2,588,000
142236	Ada mbalimbali	1,785,000	423,198	-	423,198	1,361,802
142237	Ada za Usajili wa Nyaraka	7,140,000	12,667,700	3,451,250	16,118,950	8,978,950
	JUMLA	**263,415,000**	**126,310,518**	**19,554,450**	**145,864,968**	**117,550,032**

Kiambatanisho 7c: Usajili wa Kazi za Hakimiliki

AINA YA KAZI	2007/2008	2008/2009	2009/2010	2010/2011	2011/2012
Miziki	318	50	103	10	42
Qasida	5	16	5	8	25
Vitabu	13	11	2	5	37
Filamu	1	6	3	5	8
Mawaidha	0	0	0	26	-
Miswada ya Vitabu	30	15	15	5	3
Miswada ya Filamu	0	0	5	3	6
Tamthiliya	15	1	8	1	-
Maandishi ya Miradi	0	0	1	1	-
Michoro	0	22	0	1	20
JUMLA	**382**	**121**	**137**	**64**	**141**

Kiambatanisho 8: Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2011

	SHIRIKA	ME	KE	JUMLA	WA Z'BAR
1.	**Ahlu Daawa Hajj and Travelling Agency**	**48**	**39**	**87**	**44**
2.	**Alharamayn Development Fund**	**51**	**40**	**91**	**66**

3-4	**Alfirdaus & Hajj Caravan**	**108**	**72**	**180**	**55**
5	**Al- Maarifa Charitable Centre**	**-**	**-**	**-**	**-**
6-7	**Jumuiya ya Maimamu & Alkhayria**	**46**	**25**	**71**	**68**
8.	**Jumuiya ya Istiqama**	**109**	**104**	**213**	**102**
9	**Khidmat Islamiyya Charitable Society**	**65**	**51**	**116**	**32**
10-11	**Zanzibar Hajj andTravelling Agency (ZAHATA) & Labayka**	**41**	**29**	**70**	**70**
12	**Zanzibar Istiqama Hajj Travelling Agency (ZIHATA)**	**81**	**87**	**168**	**131**
	JUMLA	**549**	**447**	**996**	**568**

Idara/Taasisi	Jumla	Unguja		Pemba		Wafanyakazi Kielimu		
		W/me	W/ke	W/me	W/ke	Cheti au chini	Stashahada au zaidi	% Stashahada au zaidi
Mahkama	**352**	156	84	76	36	268	84	**16%**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	**38**	24	14	0	0	23	15	39%
Tume ya Kurekebisha Sheria	**19**	11	8	0	0	10	9	**47%**
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	**82**	44	23	11	4	36	46	**56%**
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	**12**	6	6	0	0	3	9	**75%**
Idara ya Utumishi na Uendeshaji	**51**	29	22	0	0	33	18	**35%**
Afisi Kuu Pemba	**34**	0	0	21	13	23	11	**32%**
Idara ya Mufti wa Zanzibar	**43**	18	13	8	4	29	14	**32%**
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	**50**	24	11	10	5	28	22	**44%**
Mrajis wa Vizazi Vifo	**19**	5	14	0	0	15	4	**21%**
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	**6**	0	5	1	0	0	6	**100%**
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	**89**	38	18	24	9	66	23	**25%**
Jumla	**795**	**355**	**218**	**151**	**71**	**534**	**261**	**33%**

Kiambatanisho 9a: Idadi ya Wafanyakazi 2011/2012

	SHAHADA YA UZAMILI		STASHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA KWANZA		STASHAHADA YA JUU		STASHAHADA		CHETI		JUMLA
IDARA	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	
Mahkama		3			2	3			4	12	5	3	**32**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu		1			2				3	11	5	3	**28**
Afisi ya M/ Mashtaka	1	2									1		**4**
Tume ya Kurekebisha Sheria													
Idara ya Mipango na Sera		2			1				1				**4**
Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1	1	2	1	1	1			2		1	2	**11**
Afisi Kuu Pemba									1	1	2		**4**
Afisi ya Mufti wa Zanzibar	1								1			2	**2**
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali													
Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo												2	**2**
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki				1									**1**
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana		1				1			1	3	2	1	**9**
JUMLA	**3**	**10**	**2**	**2**	**6**	**5**			**13**	**27**	**16**	**13**	**97**

Kiambatanisho 9b: Wafanyakazi Waliopo Mafunzoni 2011/2012

Kiambatanisho 9c: Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mfupi 2011/2012

NA	IDARA/TAASISI	W/KE	W/ME	JUMLA
1	Mahkama	6	2	**8**
2	Afisi ya Mwanasheria Mkuu	0	3	**3**
3	Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	5	6	**11**
4	Tume ya Kurekebisha Sheria	3	3	**6**
5	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	0	2	2
6	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1	0	**1**
7	Afisi Kuu Pemba	0	0	**0**
8	Afisi ya Mufti wa Zanzibar	0	0	**0**
9	Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	0	0	**0**

10	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	2	1	**3**
11	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	0	0	**0**
	JUMLA	**17**	**17**	**34**

Mhe. Naibu Spika: Namshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake kwa ufasaha, kwa kutumia muda usiozidi saa moja na Nuku. Sasa tunamkaribisha mchangiaji wa mwanzo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, ambapo kwa niaba Mhe. Wanu Hafidh Ameir atawasilisha hotuba hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) Mhe. Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kunipa nguvu za kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, halikadhalika napenda kukushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ya awali kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii muhimu katika utawala wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, sio kosa kutamka Wizara ya Katiba na Sheria ni katika wizara zenye bahati ya kupata watendaji wachapakazi kazi. Kamati yangu inawapongeza sana watendaji wa wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa jitihada zao kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, nampongeza Mhe. Waziri kwa ustadi wake katika kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake, vile vile nawapongeza watendaji wote wa wizara hii waliohusika, kwa namna moja au nyengine, katika kumtayarishia Mhe. Waziri hotuba iliyosomwa hivi punde. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mpungufu wa fadhila nisipowapongeza Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wote, ambao Kamati ikifanya kazi za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuihoji serikali na kutoa, maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
8.	Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	-	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kusema kwamba, kiujumla Wizara ya Katiba na Sheria ndio wizara inayohusika moja kwa moja kuhakikisha kuwa mamlaka ya nchi ni ya wananchi wenyewe. Aidha, pamoja na mambo mengine wizara hii inajukumu kubwa la kusimamia upatikanaji wa haki na kuzingatia utawala wa sheria.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti:

Mhe. Naibu Spika, ili kuongeza ufanisi wa kazi za Wizara, Kamati inaishauri wizara inapoleta kazi zake za kawaida katika kamati iweke utaratibu mzuri wa kutoa ufafanuzi wa jumla wa bajeti ya wizara, kila kifungu kiwe na maelezo yake ya matumizi ipasavyo, kwani hizi ni pesa za walipa kodi na sisi kama ndio wasimamizi wa pesa hizo. Hivyo lazima tuone mtiririko mzima wa matumizi, ili tuweze kutoa mapendekezo yetu kwa ufanisi zaidi.

Kamati pia imesisitiza haja ya wizara kuelimisha wananchi jinsi ya kutoa michango yao katika mchakato mzima wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa kama haki yao ya msingi, kwani wananchi hutofautiana kifikra na uchanganuzi wa mambo. Hivyo, elimu ilikua na haja ya kutolewa kabla Tume haijaanza kukusanya maoni yake hapa Zanzibar, ingawa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wakati akijibu hoja za Wajumbe mbele ya Baraza hili, alisema kwamba serikali haina msimamo kuhusiana na hilo na maamuzi ni ya wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo:
Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaishukuru serikali kwa kuanzisha afisi hii mpya ambayo imeitenganisha na Afisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi na kuondoa kero kwa wananchi waliokuwa wakisumbuka kupata huduma muhimu zinazotolewa na afisi hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati inasikitishwa sana kutokana na lengo la afisi hii kutofikiwa kutokana na kero kwa wananchi hivi sasa kuongezeka, ambapo kumekuwa na usumbufu mkubwa zaidi ya ilivyokuwa mwanzo katika suala zima la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Pia wananchi ambao wanaishi vijijini wanapelekewa huduma hiyo huko huko Vijini lakini huduma hizo hutolewa kwa kutumia wafanyakazi wa Afisi za Mikoa na Wilaya.

Kutokana na matatizo hayo kamati inaishauri serikali kuiruhusu wizara hii kuajiri wafanyakazi wa kudumu katika Wilaya na Mikoa ili kuepusha matatizo ya upatikanaji wa vyeti. Hii ni kutokana na kuwa afisi hii haina udhibiti na Watendaji wanaofanya shughuli hizi katika Wilaya na Mikoa kwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuthibitisha hilo Watendaji hawa hushiriki katika shughuli mbali mbali za kitaifa na kupelekea utendaji kwa upande wa Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kuzorota hali ambayo inasababisha kero kubwa kwa wananchi.

Tume ya Kurekebisha Sheria:

Mhe. Naibu Spika, kamati imeridhishwa na malengo iliojipangia Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Hata hivyo, kamati yetu imesikitishwa na kitendo cha serikali cha kutokuwa na mipango madhubuti wakati inapoamua kuanzisha jambo. Kitendo hiki huchangia kwa asilimia kubwa kuwaletea usumbufu watendaji wake na hatimae kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi unaokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, tunasema hili baada ya Tume hii kuhamishia shughuli zake katika jengo la Kamisheni ya Wafku na Mali ya Amana hapo Mbweni, wakati hapo kabla ilikuwa inatekeleza shughuli zake hapo Maisara kwenye jengo la Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo maarufu *EACROTANAL*.

Mhe. Naibu Spika, ingawa kamati yetu haijalitembelea jengo linalotumika hivi sasa. Hata hivyo, ni imani yetu kwamba jengo hilo litakuwa na nafasi ya kutosha itakayowawezesha watendaji wa Tume hii kutekeleza majukumu yao bila ya usumbufu wowote. Kwani hapo kabla Tume ya Kurekebisha Sheria

ilikuwa inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa nafasi katika jengo walilokuwa wanalitumia. Kwa mnasaba huo, tunaishauri serikali kuwa na mipango madhubuti inapoamua kuanzisha jambo, ili kuwaondoshea usumbufu Watendaji wake wa kuhamahama ovyo kama watoto wa paka.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria miongoni mwa majukumu yake ni kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho ya sheria. Kamati yetu haijaridhishwa na kiwango cha fedha kilichokadiriwa Tume hii kutumia ingawa kwa mwaka huu wa fedha kimeongezeka.

Mhe. Naibu Spika, tunashauri hili kwa kuwa Tume hii haina marejeo *'reference'* yoyote inayowaongoza katika kutekeleza shughuli zao, ingawa hapo kabla serikali iliwahi kuanzisha Tume kama hii lakini haikuwa na mafanikio. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Saba imelifufua tena jambo hili kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu. Hivyo basi, tunaiomba serikali ilifikirie suala hili ili malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi hii yafikiwe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katueleza kwamba katika mwaka huu wa fedha, Tume ya Kurekebisha inatarajia kufanya utafiti kwa lengo la kugundua kasoro kwenye sheria mbali mbali, tunaliunga mkono wazo hilo. Hata hivyo, tunaishauri Tume kuwapatia taaluma ya utafiti watendaji wake, ili waendane na wakati tulionao sambamba na kufanya shughuli zao kwa taaluma zaidi. Aidha, tunawashauri watafiti hawa kuwa wabunifu na wachangamke, jambo hili litasaidia kutokurekebisha sheria zetu mara kwa mara. Kwani imebainika kwamba Watafiti wa Tume hii hawana taaluma ya utafiti, jambo ambalo litachangia kuzorotesha utendaji wao.

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka:

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kusimamia vyema ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na hatimae kupelekea kuokoa fedha za walipa kodi wa nchi hii. Hii ni kutokana na kuwa Chuo hiki kilijengwa chini ya gharama zilizokusudiwa. Mhe. Naibu Spika, tunawashukuru kwa dhati kabisa wasimamizi wote wa ujenzi wa Chuo hicho kwa uaminifu wao waliouonesha, hasa tukizingatia kwamba baadhi ya Watendaji wa Taasisi za Serikali hutumia nafasi hiyo kama ni moja ya kianzio cha kujipatia kipato. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, tunauomba Uongozi wa Chuo hiki kukamilisha taratibu zote zinazotakiwa za usajili haraka iwezekanavyo, ili

Chuo hiki kisajiliwe rasmi. Hatua hii itaisaidia Chuo kutambulika zaidi na hatimae kuweza kujiendesha wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Chuo hiki kinatekeleza vyema majukumu yake kama nilivyoeleza hapo awali hatuna mashaka na ongezeko la asilimia mia moja la Fungu 35 kwenye Kifungu 0202. Hivyo, kutokana na kauli yetu hiyo tunaiomba serikali kukiingizia Chuo hiki Ruzuku ya shilingi 100,000,000/= mapema iwezekanavyo, ili kizidi kutekeleza kwa ufanisi malengo yake kiliojipangia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Watendaji wa Afisi hii ni waaminifu Kamati yetu haina budi pia kuiomba Benki ya Maendeleo ya Afrika. *'African Development Bank – ADB'* kukitimizia Chuo hiki zile ahadi ilizotoa ikiwa ni pamoja na kugharamia kazi ya kuimarisha mitaala ya Chuo.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba hili kwa kuwa tunakishauri Chuo hiki kuingiza katika mitaala yake somo la*'Communication Skill',* kwani imebainika kwamba baadhi ya wananchi wakiwemo wanasheria wetu hushindwa kujieleza kwa Lugha ya Kiingereza. Hivyo, endapo wataendelea kupatiwa taaluma hiyo kuna uwezekeno mkubwa wa kukuza elimu zao.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa upande wa Pemba inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa nafasi. Kwa kuwa kamati yetu ilielezwa kwamba afisi hii inatarajia kuhamia katika jengo jengine siku ya Jumatatu ya tarehe 16 Julai, 2012 (yaani leo hii). Tunamuomba Mhe. Waziri wakati wa majumuisho atueleze kama uhamiaji huo umefanyika na kama haukufanyika ni kitu gani kilichowakwamisha.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba hili kwa kuwa Watendaji wa Afisi hii kuendelea kubaki katika jengo wanalotumia hivi sasa ni kwenda kinyume na matakwa ya Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na masuala ya Kazi Duniani *'International Labuor Organisation – ILO'*, jambo ambalo wanalielewa kwani baadhi ya watendaji wa Afisi hii ni Wanasheria. Hivyo, haitokuwa busara kwa Watendaji hawa kuvunja sheria hizi.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu:

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa anawasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yake mwaka jana katika ukurasa wa 21 wa kitabu chake alitueleza kwamba, Afisi hii itaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Afisi, na katika mwaka huu wa fedha katika ukurasa wa 22 ametueleza kuwa Afisi hii inatarajia kukamilisha ujenzi wa jengo hili kwa mwaka huu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kauli mbili hizo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza sana Afisi hii kwa kuweza kusimamia vyema ujenzi huo. Aidha, tunashukuru serikali kwa kuiingizia fedha za Kazi za Maendeleo Afisi hii kwa wakati, jambo ambalo limeipelekea Afisi hii kutarajia kumaliza ujenzi huo kama ilivyopanga.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulijuulisha Baraza lako Tukufu kwamba hadi tunawasilisha hotuba hii, Kamati yetu imeshindwa kupata namna bora ya kueleza sifa za Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, kwa jinsi anavyoweza kusimamia vyema majukumu yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunatamka haya kwa kuwa Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa Mkurugenzi wa Mashtaka alisimamia vyema shughuli mbali mbali za afisi hiyo na kupata mafanikio makubwa na leo hii ameweza kuanza shughuli za ujenzi wa afisi yake mnamo mwezi wa Agosti, 2011 na anatarajia kumaliza ujenzi huo na kuhamia katika Afisi hiyo mnamo mwezi wa Januari mwaka 2013. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mafanikio mbali mbali yanayopatikana kutokana na utendaji bora wa Mhe. Othman Masoud Othman, tunaishauri serikali kumtumia vyema Mheshimiwa huyu katika masuala mbali mbali kwa maslahi ya maendeleo ya nchi yetu na pia kumtunuku Hati Maalum ya utendaji kazi bora serikalini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo, kamati hii inaishauri afisi hii kuwa makini wakati wa ununuzi wa vifaa vya Afisi hii. Kwani imebainika kwamba asilimia kubwa ya vifaa vinavyonunuliwa na baadhi ya taasisi huwa haviendani na mazingira ya nchi na kupelekea kupotea ovyo fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, tunaiomba Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuzishajiisha Wizara za Serikali kutunga Kanuni haraka iwezekanavyo kwa zile sheria zinazohitaji hivyo, ili ziweze kuleta urahisi katika matumizi yake.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 21 wa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri ya mwaka jana, alitueleza kwamba afisi hii imedhamiria kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mikataba ya Serikali. Lakini leo hii ametueleza kwamba miongoni mwa mazingatio ya Sheria ya Afisi hii inayotarajiwa kukamilishwa katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na kuanzishwa Kitengo hicho.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa baadhi ya Taasisi za Umma zinafunga mikataba bila ya kuishirikisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu, tunashauri sheria hiyo ikamilishwe haraka, ili kuondoa kasoro na migongano inayojitokeza hivi sasa, na zaidi pale Zanzibar itakapoanza kukabiliana na mikataba ya ufuatiliaji na uchimbaji wa mafuta. *(Makofi)*

Afisi ya Msajili wa Hakimiliki:

Mhe. Naibu Spika, ingawa kwa mwaka huu wa fedha Ruzuku ya Afisi hii imeongezeka kutoka shilingi 100, 000,000/= hadi shilingi 120, 000,000/=, bado kiwango hicho ni kidogo kutokana na majukumu mazito na changamoto mbali mbali zinazoikabili Afisi hii. Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki inakabiliwa na ufinyu na nafasi katika ofisi wanayoitumia ambalo ni jengo la Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Afisi hii imeazimwa na Wizara hiyo jumla ya vyumba vitatu ambavyo ni vidogo na havina hewa ya kutosha. Vyumba hivyo vinatumika kama ofisi na ghala ya kutunzia kazi za hakimliki zilizosajiliwa na zile zilizokamatwa. Vifaa hivi vya kielektroniki vikiwemo *CDs, VHS, DVDs* ni rahisi kuibika, aidha, vinapopata joto hutowa harufu nzito ambayo hewa yake inavutwa na wafanyakazi hawa kila siku ambayo pia inaaminika kuwa ni sumu hivyo kuna uwezekano mkubwa wa watendaji hawa kuathiri kidogo kidogo. Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo, kamati hii inaiomba serikali kuitafutia jengo Afisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa huzuni tunatamka kwamba Afisi ya Msajili wa Hakimiliki kwa upande wa Pemba imefungwa kwa kuwa mtendaji wa afisi hii yupo masomoni na kuna uwezekano mkubwa wa mtendaji huyo kutokufanya tena kazi katika afisi hii. Hii ni kutokana na kuwa masomo anayosomea hivi sasa hayaendani na utendaji wa shughuli za Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Hivyo, tunaishauri Afisi hii kuajiri mtendaji katika Afisi ya Pemba, ili na wananchi wa huko waweze kufaidika na dhamira ya uanzishwaji wa Afisi hii pamoja na kuwaondoshea usumbufu wasanii wa Pemba kuja Unguja kufuata huduma hizi.

Mahkama:
Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inazipongeza Mahkama zote kwa kuendeleza vyema utoaji haki kwa wananchi. Hata hivyo, Wizara ya Katiba na Sheria inapaswa kuendelea kuwatupia macho Majaji na Mahakimu wanaolalamikiwa kwa kujihusisha na rushwa na hivyo kuathiri utoaji wa haki na misingi ya utawala bora. Jambo hili huwapelekea wananchi kukosa imani kwa mhimili huu muhimu wa dola. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ingawa Mhe. Waziri wa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakati akijibu hoja ya 38 dhidi ya Ofisi yake alilieleza Baraza hili kwamba dhamira ya Serikali sio kujenga matabaka miongoni mwa Vyombo vya Dola bali ni kuweka usawa katika masuala ya maslahi. Kamati yetu haina mashaka na kauli hiyo, isipokuwa imebaini kwamba Serikali imejenga matabaka ndani ya Chombo kimoja cha Dola (yaani Mahkama).

Mhe. Naibu Spika, tunatamka hili baada ya kilio kikubwa cha Mahakimu wa Mahkama za Mwanzo kupewa nyongeza ya mafuta tu ukilinganisha na Mahakimu wengine wakati wa kufanya marekebisho ya mishahara. Mhe. Naibu Spika, ijapokuwa Mheshimiwa Waziri alitueleza kuwa tatizo hili litamalizika baada ya Mahkama kuwasilisha na kukubaliwa Muundo wake *'Scheme of Service'* na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, bado Kamati yetu haikuridhika na maamuzi hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mtumishi hupewa maslahi yake kutokana na kiwango chake cha elimu, muda aloutumia akiwa kazini na mengineyo, na kwa kuwa wapo Mahakimu wa Mahkama za Mwanzo wenye Diploma na wengine wana Cheti. Je, Mhe. Waziri Tume ya Utumishi wa Mahkama ilipokuwa akifanya maamuzi haya imezingatia kitu gani hata ikapelekea watumishi hawa wa umma wenye elimu tofauti kulipwa kiwango kimoja cha mshahara? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inamuomba Mhe. Waziri kulipatia jibu swali letu hilo wakati wa kujibu hoja za Wajumbe kwa faida ya Kamati na Wajumbe wote wa Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kutupatia semina kuhusiana na marekebisho ya Sheria ya Mahkama ya Kadhi ya mwaka 1985. Mhe. Naibu Spika, tunaunga mkono utekelezwaji wa ahadi ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria aliyoitoa mwaka jana ya kuifanyia mapitio Sheria hiyo. *(Makofi)*

Hata hivyo, tunaishauri Wizara kuwa makini wakati wa kutekeleza hili, kwani sheria hii inagusa masuala ya dini, hivyo, sio busara kuwekwa mambo ambayo yanapingana na matakwa ya dini hii. Aidha, tunaiomba Wizara kuyafanyia kazi maoni mbali mbali ya Wajumbe waliyoyatoa kwenye Rasimu hiyo ya Sheria huko Bwawani. *(Makofi)*

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana:
Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa kuandaa na kuzindua kwa mafanikio makubwa mpango wa Zakka Zanzibar, hatua ambayo iliambatana na uzinduzi wa Muongozo wa Zakka.
Mhe. Naibu Spika, wakati Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alipokuwa akijibu hoja ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni alilieleza Baraza hili kwamba, nyumba 20 za *Block* No. 10 hapo Michenzani za watu ambao hawakupatikana zitarejeshwa katika mikono ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ikiwa Kamati yetu ni mchunga wa Wizara hii na kama tujuavyo kwamba kila mchunga atawajibika mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kile alichokichunga, hivyo, tunaomba kadhia hii ishughulikiwe haraka iwezekanavyo hasa tukizingatia kwamba suala hili linaendana na masuala ya kidini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunaiomba serikali kuwa makini wakati wa kutoa fedha katika Taasisi zake ili kuwaondoshea usumbufu watendaji wake. Mhe. Naibu Spika, tunashauri hili baada ya Watendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba kutopata mishahara yao kwa wakati. Jambo hili lilisababishwa na kuchelewa kuingizwa kwa fedha za Ruzuku ya Kamisheni hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pamoja na Kamisheni kuingiziwa jumla ya shilingi 18,000,000/= mnamo mwezi wa Juni, 2012 bado kuna kasoro ya shilingi 3,000,000/= ambayo haijalipwa. Kwa kuwa Ruzuku ya Kamisheni haikidhi mahitaji yao, tunaiomba Serikali kukimalizia kiasi hicho cha fedha kilichobaki ili iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia. *(Makofi)*

Afisi Kuu Pemba:

Mhe. Naibu Spika, kamati ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi Kuu Pemba pamoja na Idara zake inazoziratibu na kujionea hali halisi ya utendaji wake wa kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa ujumla tumeridhika kwa kiasi na utekelezaji wa Ofisi hii, hata hivyo, tunaiomba serikali kuipatia usafiri Ofisi hii kwani gari iliyopo ni moja na endapo Mhe. Waziri atakwenda Pemba basi Afisa Mdhamini wa Wizara hii hukosa usafiri kwa kipindi chote ambacho Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria atakachokuwepo huko, jambo ambalo hupelekea usumbufu mkubwa kwa Mtendaji huyo.

Mhe. Naibu Spika, tunaunga mkono hatua iliyochukuliwa na Kitengo cha Jumuiya za Kiraia cha kuzihakiki na hatimae kuziorodhesha katika daftari la usajili wa Jumuiya, Jumuiya hizi. Hatua hii ni muhimu kwani itaisaidia Ofisi

kuzitambua Jumuiya zinazofanya kazi na kuzifuta zile ambazo hazitekelezi majukumu yake na kupelekea kuwa na idadi halisi ya Jumuiya hizo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maoni hayo ya kamati niwaombe sasa Waheshimiwa Wajumbe wayakubali na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2012/2013 ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama tulivyoidhinisha kwenye kamati yetu, ambapo wizara hii imepanga kutumia jumla ya shilingi 7, 591, 000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 6, 682, 200,000/= kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 3, 455, 000,000/= kutoka serikalini na 3, 227, 200,000/= kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutamka bayana kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Vijana na Wanawake wote wa Mkoa wa Kusini naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa asilimia mia (100%) na nawaomba Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu waichangie na hatimae wayakubali makadirio yote yalioombwa kwa Wizara hii, ili waende wakafanye kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunamshukuru Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa niaba ya Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa kutumia muda vizuri. Sasa tunaendelea na wachangiaji na mchangiaji anayefuatia atakuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, afuatie Mhe. Abdalla Juma Adballa na baadae Mhe. Ismail Jussa Ladhu. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, napenda sana kukushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuichangia hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa kweli sitaki nipoteze muda niende moja kwa moja kwenye Mahakama zetu.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama zetu mara nyingi sana wakati nilipokuwa nikichangia nikawa natoa vigezo vya sheria kwa mujibu wa Katiba yetu hii ya Zanzibar. Sasa nilikuwa nikisikia tu na Mhe. Waziri wetu wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipokuwa akinijibu, sasa leo nataka nimsikie mwenyewe hasa mwenye wizara hii aweze kuniambia aidha humu kwenye Katiba tufute au tusifute. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya mambo yamerekebishwa na ninakubaliana nayo na wala sina utata nayo. Lakini katika mambo haya ya kada au *level* hizi za usomi, kuna wengine mara nyingi sana huwa ninawatetea kuhusu haki zao

nao zinachelewa kuwafika kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Tume ya Utumishi.

Sasa humu imo Tume ya Utumishi, ambayo kwa mujibu wa utaratibu ndani ya Katiba imo na ndio maana nikaeleza kuwa na Mhe. Waziri atakuja kunijibu, kwamba hii je tuifute au tuendelee nayo, kwa sababu hii ingefuta mambo yote na wala kusingekuwa na utata huo ambao uliotokezea.

Mhe. Naibu Spika, katika haki na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ameelezea hapa zile *standard* za *level* za Majaji, Mawakili mpaka kufikia Mahakama ya Mwanzo. Kwa kweli kuhusu hili niishukuru sana wizara, tunasikia hivi karibuni alikutana nao hawa na kuwajibu kwamba yumo mbioni kuwatekelezea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje aniambie amefikia *level* gani katika kuwatafutia watu haki zao.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Makarani. Mhe. Naibu Spika, Makarani ndio wenye kesi ni sawa kule hospitali *oderlies* na *nurses* ndio watendaji, lakini katika Mahakama Makarani ndio watendaji wakuu, Jaji anangojea apelekewe *file* na Karani akikataa hakuna *file* na wala kesi hakuna, utasema nini na wao mishahara yao ni midogo sana.

Kwa kweli na wao katika maeneo haya Mhe. Waziri hamjaangalia. Kwa mfano, *secretary* wa Mahakama Kuu wa Majaji anapata maposho mengi na yeye huyu tunamuweka wapi na yeye huyu ana mchezo mbaya sana na atakula rushwa tu na huna njia ya kufanya. Lakini jinsi ya kumdhibiti asile rushwa, basi ni vyema aangaliwe na yeye mafao yake tena sana na tunayo tabia ya kuchelewa, sasa kila tukichelewa basi na wao wataendelea kula rushwa na kupoteza ushahidi, yaani *files* zitapotea tu.

Mhe. Naibu Spika, sehemu nyingi sana hata maposho kwa maderera na wao wameongezewa, lakini hawa sijui wamekosa nini hawa Makarani. Kwa kweli ninavyokujua Mhe. Waziri basi ukitoka hapa leo utawaita Makarani kwa ajili ya kuwahakikishia kwamba na wao watapandishiwa mishahara yao, ninayo imani hiyo, kwa sababu wale wa Mahakama ya Mwanzo tayari umeshafanya kikoa nao na umewaahidi, hivyo sidhani kama utarejea nyuma katika masuala haya. Kwanza Mhe. Waziri wewe *Alhamdulillah* umeridhika na maisha na wala hutoona choyo kabisa na wao hawa kuwatafutia misingi ya fedha yao, kwa ajili ya maslahi yao.

Vile vile kuna vijana hivi sasa ambao wamerudi kusoma nchi tofauti, lakini mpaka leo sijasikia kupandishwa vyeo, kulikoni? Mhe. Naibu Spika, tunahangaika kutafuta Majiji wa Mahakama ya Ardhi, kumbe vile tunao watu

wenye sifa, wapo mpaka leo wameng'ang'ania nafasi zile za Mahakama ya Wilaya na watu tayari wameshakwenda kuchukua negree pamoja na mambo mengine, basi ni vyema tuwape haki zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni sababu gani na mimi nashangaa sana. Sasa kama kuna Tume, basi iangalie uwezo jinsi gani ambavyo wanaweza kutoa *recommandation* zao za kusema hawa hawafai kwa moja, mbili, tatu. Lakini basi mtu akisema ndio iwe hivyo na wala haiwezekani Mhe. Naibu Spika, hivyo ni vyema Mhe. Waziri aiangalie Tume yake ina nini sasa, kwa sababu inatupotezea wakati, ndio maana kesi zimerundikana nyingi kumbe vile tunao ukiritimba huo tu.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana vijana wetu waliorudi kusoma wapewe haki zao, kwani nafasi zipo za utendaji wa kazi, kama vile Mahakama ya Ardhi na kijana yule tunampa tabu na wala haongezewi mtu wa kumsaidia pale na yupo mwanamama pale, yaani ni watu wawili ah! Mhe. Naibu Spika, naomba sana watafutiwe nafasi na wao, ili waweze kujisikia.

Sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 26. Mhe. Naibu Spika, hapa napenda niendelee kusifu tu Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wanakwenda vizuri, lakini utaratibu wa kesi zinakawia tu, labda niseme hilo. Kwa hivyo, wawe na *speed* kwa ajili ya kuharakisha kesi kuweza kufikisha Makahamani, ili kuondoa hitilafu ndogo ndogo na baadhi ya mambo mengine yanayotakiwa kupelekwa ushahidi pale Mahakamani usipotee ushahidi ule, kwa sababu kuna vitu vyengine vina-*expire*.

Kwa maana hiyo, hapo ningewaomba Mhe. Mkurugenzi mhusika aharakishe sana suala hili na tunavyomjua sisi wengine ni mwalimu wetu na amebobea sheria na tuko naye pamoja. Mhe. Naibu Spika, kwa hilo tujitahidi sana.
Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 34 Ofisi ya Mraji Mkuu wa Serikali. Kwa kweli hapa ninaomba sana kwa sababu kuna mambo yanafanyika kinyume na utaratibu. Sasa nadhani tujiridhishe Mhe. Naibu Spika na kujiridhisha kwenye ni kwamba sasa kusitendeke mchezo wa kufanya makampuni hewa, tujiridhishe hivyo Mhe. Naibu Spika na tujipange vizuri.

Vile vile kuna mambo mengi tu ambayo nimeyaona Mhe. Waziri. Lakini kwa kuwa wewe pamoja na Mrajis wako muko *understanding* kabisa na masuala kama haya ya jamii, basi mimi hapa sitaki kutia *comments* zangu, kwa sababu siku hizi nasubiri kwenye buku ndiko kwenye kabari yenyewe na hapa nakuachia tu. Kwa hivyo, hapa nasema kwamba Mhe. Waziri ujitahidi sana katika masuala ujaribu kufanya marekebisho, ili yasitokezee matatizo ambayo ya watu kudhumiwa au mtu kwa binafsi anafanya makampuni hewa.

Mheshimiwa nende kwenye Kamisheni ya Wakfu na Amana, hapa nasifu sana kwa utendaji wao ingawa na kasoro zipo. Katika kurithishana mali na hapa panaingiliana na lile suala la Kampuni. Naomba niulize swali Mheshimiwa. Je, Wizara yako ina sheria ya kutengeneza hati ya nyumba za Michenzani. Kama huna sheria hiyo basi nakuomba sana kuna hati imefanywa kwa nyumba za Kilimani na Wizara yako sijui ndio mnaita Wanasheria *declaration* sijui kama ndio hivyo. Basi naomba Mheshimiwa uifute kwani itakuwa ni kinyume na utaratibu wa ufanyaji wa hicho kitu.

Ninavyojua mimi nyumba za Michenzani, nyumba za Kilimani zina hati zake za asili na wenye mamlaka ni wao. Itakuwaja Mambomsige au Kwenye Mrajisi Mkuu mtu atengeneze hati. Sheria hiyo hata Mwanasheria Mkuu sijui kama kaiona hiyo na hii hata ukimpa Mwanasheria aijibu nitaridhika sana, ili nione jinsi gani nitaweza kuupata huo ufafanuzi. Vipi utaweza kufanya *registration* ndani ya *registration* basi sheria moja naomba tuifute kabisa ili tukubaliane moja iwe sahihi na michezo hii ipo mingi tu.

Mhe. Spika, sasa hivi nikupe tahadhari Mheshiwa Waziri, sasa hivi kule ardhi yule mwenyekiti wa kuhaulisha bodi hajachaguliwa. Hapa ndio hatari, wakati wowote hati zitatoka Mambomsige. Nina imani hiyo neema kwako wewe inaanguka kwa wafanyakazi wako. Sio kwako wewe hupati nema hii hapana, nasema neema kwa watendaji wako inaanguka.

Mimi nilishangaa sana kuwa Mwenyekiti wa Bodi mpaka leo hajaweza kuwekwa ni kitu cha kusikitisha. Tunatoa mianya ya kuweza watu kufanya mambo kinyume na sheria. Kwa sababu wewe huwezi kuhusika kwenda kuhaulisha kule, lakini mtu anafanya hati ya kuhaulisha kutoka kwako kupeleka ardhi na bado mtu anaambiwa kapewa haki. Mheshimiwa hichi kitu naomba sana ukiangalie tena kwa uangalifu sana kisikuharibie sifa zako katika utendaji Mheshimiwa.

Mheshimiwa ukitaka vielelezo vya kuonesha hilo basi wahusika wako wanao watu wa Mambomsige watakueleza. Na hiyo kesi yenyewe mpaka leo haijapatiwa ufumbuzi wa ufungaji wa faili, halijafungwa lakini ndio tunasema kwamba utaratibu ufanyike, lakini nakuomba sana, Mheshimiwa utizame haki ilipo na kuweza kupatikana.

Mheshimiwe niende katika masuala ya Hati Miliki, katika umilikishaji masuala ya umilikaji. Kwanza nimsifu sana Mhe. Mkurugenzi wa Hati Miliki, Afisi Mrajisi wa Hati Miliki. Mheshimiwa hapa pana utendaji mzuri, lakini matatizo yaliyokuwepo kwamba kijiofisi babo ni kidogo. Ameshaeleza hapa Mwenyekiti wa Kamati na mimi naunga mkono. Mheshimiwa Afisi imekuwa ghala, ni aibu moja hiyo. Mambo yanakusanywa mle zinatumika kemikali.

Nakubaliana nao wakati huna ile ya kuziba pua masaa 24, tunategemea nini. Mtu ana mwili wake lakini ananyonyeka, hujui ananyonyeka nini, ananyonyeka na kemikali kabisa. Hicho kitu ambacho kinasikitisha sana. Angalia Mheshimiwa pale katika ile Afisi yako takriban wote, nani mnene pale. Kwa sababu ya nini? Ni kemikali zile ni kitu mbaya sana.

Mheshimiwa naomba sana kawakamate wahusika wenye mambo ya majumba haya, kuna watu wanakaa tu bure bure. Hebu wapeni na hawa watu wajisikie na waweze kufanya kazi zao kwa vizuri. Lakini nimsifu sana ingawa Mkurugenzi huyu anafanya kazi ya hatari. Siku moja nilikuja na lalamiko kuhusu habari ya Afisi hii lakini *Wallahi* sijapata kuona hata sikumoja Afisi moja nikatendewa haki kama ulivyofanya wewe.

Mheshimiwa nilivyofika tu pale nilivyokueleza tu pale kuna *problem* hii na hii kwa hawa watu wanaouza hawa *cassette*. Mheshimiwa ulilifanyia kazi pale pale ukamwita Katibu ukamwita na Mkurugenzi mwenyewe. Mheshimiwa niliridhika sana siku ile na nilijisikia raha sana. Niliona kuwa kweli mimi Mwakilishi kuwa leo Mhe. Waziri unayohaki ya kuniringia, lakini hukufanya kitendo hicho kwa kuhofia siku kama leo kwenye bajeti, maana yake ningekukamata tu lakini uliotea na kuweza kunisaidia.

Kazi ile nimeifatilia na nimegundua kuna mambo mengine hawa ndugu zetu wanauza zile kanda za usingizi. Kwa kweli mama kafanya kazi nzuri sana. Nimeoneshwa kanda nyingi sana za usingizi Mheshimiwa nyengine nilizitia kwenye gari yangu basi zimeibiwa. Mpaka leo nashindwa kujibu kuwa nilizirejesha au sijazirejesha kuona vile vielelezo. Wanauza hawa ndugu zetu kanda za usingizi, naomba sana ndugu zetu waache, hizi kanda kabisa, kuziuza. Wanawapotosha watoto wetu. Mazingira haya anapoyafanyia kazi mkurugenzi ndio yanamkuta mambo chungumzima.

Mimi nilijaribu kuzungumza nao vijana wenzangu kuwambia jamani kama kasoro mama atakuwa nazo kasoro ndio ubinaadamu kiutendaji lakini anarekebishika. Alikuwa tayari tukutane nao wale vijana tuzungumze. Lakini baadaye wakampelekea ujumbe mbaya sana kwa kweli hata mimi umenitisha. Si vizuri kumpelekea mtu ujumbe ambao mbaya sana, lakini hawajajua imani yake ndani yake. Imani yake ni kuweza kuwasaidia wale vijana lakini wamemtisha.

Mhe. Waziri pamoja na kutishwa kwake lakini anaendelea na kazi yake nzuri sana, tena sana. Hongera sana mwana mama, kumbe kina mama wakiwezeshwa na kina baba wanaweza kufanya hayo mambo, sio peke yao.

Nimalizie kwenye marekebisho ya Katiba, ndio safari yangu ninakoelekea. Mheshimiwa itanibidi sasa nisome, nakuomba kwa sheria uniruhusu kidogo nisome halafu kuna suala itanibidi niulize. Mheshimiwa anasema hivi kifungu cha 125 ukurasa wa 54 kinasema hivi:-

Kifungu cha 125 "Nchi yetu imo katika hatua muhimu kwa hatima yetu na vizazi vyetu ambayo inahusu ukusanyaji wa maoni kwa ajili ya kuandika upya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano kila mwananchi wa Zanzibari ana uhuru, maoni kikatiba, Kifungu cha 18(1) cha Katiba ya Zanzibar, lakini maoni hayo yasikiuke mipaka kwa kukera wananchi wengine au kumvurugia maslahi ya umma"

Kifungu cha 24(1) "Kwa maana hiyo mtu anaweza akipenda kusema anataka nini kirekebishwe katika Muungano huo jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa maoni yake ni kwa maslahi ya Zanzibar na Wazanzibari. Kimsingi lengo latu ni kufanya Zanzibari kuwa na haki na Uhuru wake kamili ndani ya Muungano wetu lengo ambalo litaifanya Zanzibar kutekeleza mambo yake ya kimaendeleo bila ya kuingiliwa"

Mheshimiwa tuna Katiba hii hapa. Katiba yetu Zanzibar tukiangalia mazingira yake mwisho wake Chumbe. Tuwambie ukweli wananchi tusiwafiche, tuseme ukweli. Mheshimiwa naomba leo kidogo niseme nipe hata dakika 30. Mimi linanisikitisha sana jambo moja, kilichonileta hapa nimechaguliwa na wananchi nije kuwasemea maslahi yao, ninapokosa kuwasemea kwanza nakosa mambo mawili. Jambo la kwanza Mwenyezi Mungu anakwambia umekula dhulma.

Jambo la pili watakosa kunipa kura kwa sababu sikuwatetea haki yao. Humu mimi nina kinga na fursa, nina wajibu wa kusema yale ambayo nimeyaona mimi yana kero kwa kuielekezea Serikali kidole. Nitakapokwenda chamani sitosema jambo la humu nitasema jambo la chamani. Naomba jamani mtusaidie hilo. Hii imeundwa na wanachama wenyewe na wananchi wenyewe walioiunda Katiba hii.

Leo naomba nipewe maana ya kupumua, Mhe. Abubakary uniletee nini maana ya kupumua. Mimi nashangaa naambiwa Mshimba anasema kupumua, naijua kupumua ina tafsiri nyingi. Lakini leo tumeifanya kupumua imeletwa na watu fulani tu. Tunakosea Mheshimiwa tangu huko nyuma kupumua imo, hakuna mtu asiyejua kama binaadamu ukifanya kazi unatakiwa upumue.

Mimi nashangaa sana Mheshimiwa kuambiwa sisi kina Mshimba na nani wanasema kupumua. Hapana Mheshimiwa, napumua ninapomaliza Baraza, sindio kupumua, nikikwambia Mhe. Naibu Spika, leo nataka nipumue uniachie niseme, nina maana yangu kwamba leo uniachie niseme kwa raha. Juzi Mhe. Makamo wa Pili namnukuu amesema kuwa huru kwa kila mwananchi aseme lile analoliona, Mheshimiwa tusioneshane vidole.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie kitu kimoja. Tulipokuwa tunaitaka Serikali ya Kitaifa ndio haya haya ya Muungano baadaye tunakuja kuoneana aibu. Mwisho si tuliikubali sindio hii inayotupa leo jeuri ya kusema hapa. Ukweli tuuseme hivyo kwa nini tuwapotoshe wananchi wetu. Tuwambie kama Katiba yetu haifanyi kazi ndani ya Muungano tunaona tabu gani kuwambia. Hatuna uchumi Zanzibar, tunaona tabu gani kuwambia. Lakini namgeukia Mhe. Waziri kazi hii ilikuwa uifanye wewe kabla ya kuamshwa ulikuwa uifanye mapema kazi hii, wewe ndio kazi yako hii. Ilikuwa wananchi wa Wizara yako ndio wenye kazi hasa ya kitengo maalum kuwaelimisha wananchi sheria, kuwaelimisha watu waijue Katiba ya Muungano na ya Zanzibar.

Katiba yetu imefichwa, huo ni ukweli usifichwe, umemezwa waaaa. Hii hapa naona haya hata kuitoa huko mbele ya safari kwa sababu inaishia Chumbe, ukweli tuseme hivyo. Lakini sasa wakati huu hapa hapa ndio pa kupatiza hakuna pengine tusidanganyane, tumechoka na kero. Nawaomba wanasheria mnapokuja kunijibu maswali yangu mnijibu kwa sheria.

Tumesema gesi asilimia imo ndani ya Muungano niambieni Wizara yake iko wapi, mbona hampigi makofi hapo, *are you serious,* si kitu cha mchezo. Mimi nauliza suala dogo tu hapo, lisikupeni tabu wana sheria, nakupeni tabu. Nishati Zanzibar wanayo nishati, lakini kwenye Muungano nambie sasa kule nishati nakubaliana nayo, Bara nishati ipo na Zanzibar nishati ipo, haya nambie nishati ya pili iko wapi ya mafuta. Ndio maana hapa mnashindwa kuyachimba mafuta kwa sababu sheria hapa iko wapi ya kuweza kutulinda sisi kuweza kuyachimba. Tuambizane ukweli jamani tusiwadanganye wananchi, tunashindwa kutokana na kwamba hatuna sheria ya kuchimba.

Tumesema tuna gesi asilia hapa wenzetu wameshaanza kuchimba gesi asilia wana ma-*trillion* ya fedha hapa wangetupa *trillion* moja tu. Sasa hii Wizara iko wapi, tayari inakusanya fedha. Mhe. Abubakary hili ni kero kubwa mimi hapa sikuachi mpaka unitafutie Wizara yangu hii niijue nikadai pesa zangu.

Mhe. Naibu Spika, gesi asilia leo tuna miaka mingapi tumeshachimba. Nani Mzanzibari kahusishwa kule, halafu usiseme ukisema unatishiwa amani

katika Chama. Nitasema miye. Hebu uliza Mheshimiwa hiyo Wizara imeundwa tuseme *ok*, Wizara ya Katiba kule kwetu kwa Mhe. Samia wapo hao wafanyakazi wawili watatu tu Wazanzibari, sijui kama wamefika angalau 20 tunajua ile ipo. Wizara ya Mambo ya Ndani tunajua kidogo wawili watatu wamo. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje tunajua wawili watatu wamo. Wizara hii iko wapi? Halafu mtu usiseme jamani, tunakamatana hapa vipesa viwili vitatu vya wavunja jasho tunanyang'anyiana mishahara haipandi wala haishuki, tunagombana mle mle, kumbe fedha tunazo zile pale.

Mimi nataka nikwambieni kidogo Mawaziri, sikilizeni msioni tabu hebu mkenda katika *cabinet* yenu ya Baraza la Mapinduzi hebu mmoja ajitolee amwambie Mhe. Waziri katika Bangokitita mtakapokwenda. Mhe. Waziri hebu tumpeleke Mshimba mara hii, *Wallah* nitakuja nazo miye si masihara niko *serious* sifanyi mzaha wala sitaki umaarufu, umaarufu tangu asubuhi ninao. Kwa sababu nilikuwa nikicheza mpira miye umaarufu ninao hakuna asiyenijua, nimechezea Miembeni, nimechezea Mwembeladu, wala siuchukui umaarufu kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini ni haki yangu kwa mujibu wa Katiba hii hapa ndio kazi yangu mimi kusema Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, alitwambia Mhe. Salmin waliambiwa kwamba kule zile fedha zipo. Mhe. Abubakary kikao ulichoanza kwenda wewe niletee minutes za kikao hapa, mmekaa na mmejadili kuamua sasa hivi jambo hili *stop* kwa Wazanzibari biashara zao zipite. *Minutes* za kikao unazo wewe, kama unazo naomba niletee hapa kwa mujibu wa sheria, kama kweli mlikuwa mnakaa, mnajadili mambo yaliyokuwa yenye haki na sheria.

Mhe. Naibu Spika, ninachosema kuwa Wazanzibari tupewe fursa tujadili mambo yetu kwa upeo kabisa kuhusu mstakbali wa Muungano. Sisi jamani tunakufa, tunaondoka duniani watoto wetu tutawapa mashaka tena ilivyokuwa sheria, mwalimu wangu alinisomesha jana nilivunjika moyo. Sisi tunakaa tunapiga kofi hapa kumbe gumu sana hili suala la kujitoa kwenye mafuta.

Mhe. Naibu Spika, tusidanganyane jamani kwa mujibu wa Katiba hata kidogo tusidanganyane ni gumu. Lakini urahisi wake hapa kwenye maoni sasa hivi ndio njia *open* kabisa hakuna njia nyengine yeyote. Mambo yote hapa hapa tusitishane, wananchi nendeni katoeni maoni yenu. Mnafikiri sasa hivi Wazanzibari hawajui, mimi naomba sana Wazanzibari watuamini sisi Wawakilishi wao, watusikilize sisi.

Siku moja nilimwambia Mhe. Naibu Spika, kuna mtu kenda kutufanyia kikao Pemba katika kuwambia watu vizuri katiba anakwenda kutajwa Mshimba mpinzani kwani hamumjui. Imekusaidia nini? Yeye kaambiwa pale akazungumzie masuala ya maoni jinsi gani wananchi waweze kuzungumzia

suala la Muungano. Ndio, mpinzani kwa neema. Simuachii kiongozi yoyote kama wa CCM au wa CUF akala dhulma za wananchi mimi nikanyamaza kimya, siwezi utumbo huo. Mimi nitasema *Haki Lilahi Taala* ilivyo nilivyosomeshwa na mwalimu wangu.

Halafu vya kuchekesha yeye anazungumza naambiwa sikiliza huko mimi namsikia kwenye simu, nikacheka sana nikasema aaah! Msomi mzima anakwenda kusema utumbo kama huo. Wao wenyewe kule Pemba walimdharau maana niliwekewa na *message* nikaletewa. Kwa kweli jamani tusifike pahali kama huko. Wewe ni kiongozi elimisha lile ambalo unaloliona wewe muwafaka, usiwadanganye wananchi.

Mimi ninachosema kwamba mimi Muungano nautaka lakini nautaka kwa sheria zangu zitakazokubalika. Mimi ninachosema nitaunga mkono baada ya Mhe. Abubakary nilipomuuliza maswali yangu hayo matatu aje kunijibu ili niweze kumuungia mkono. Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, nasema tena la mwisho, naomba nipewe *definition* ya kupumuwa, kwa sababu kupumua imekuwa nongwa sasa hivi, jamani kupumua hakuisema UAMSHO tu, kupumua ina tafsiri nyingi. Mhe. Naibu Spika, naomba kupumua sasa. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima tukawa tunajadili mambo ya nchi yetu leo hapa. Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia hii fursa ya kusema mambo machache kidogo katika Wizara hii ya Katiba.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niipongeze Wizara kwa jitihada zake za kuboresha Mahakama. Tumeambiwa hapa katika ukurasa nafikiri ukurasa wa 14 nimeusahau kidogo. Tumeambiwa kwamba kuna mrundikano wa kesi, karibu kesi 5477 kwa mwaka mmoja. Sasa Wizara inafanya juhudi ya kuandaa Mahakama tofauti kwa ajili ya kusikiliza kesi maalum. Kwa mfano kuna Mahakama ya Ardhi, Kazi yake ni kusikiliza kesi za ardhi. Tumeambiwa kunatayarishwa Mahakama ya biashara ambayo kazi yake itashughulikia ikishughulikia kesi za biashara. Kuna Mahakama ya Watoto, lakini pia wizara hii ikiendelea na juhudi zake inaweza ikaanzisha Makama ya kesi za madai mbali na *criminal* kesi mbali. Hii itasaidia kurahisisha ule utendaji wa Mahakama na kesi zitakuwa zinakwenda haraka haraka.

Pamoja na juhudi hizo Mhe. Naibu Spika, inaonekana kuna changamoto za hapa na pale. Kwa mfano Mahkama ya Ardhi ipo muda mrefu kidogo. Moja katika mambo yanayosumbua sana ni kwamba kesi hazendi haraka. Sijui ni kwa sababu ya uchache wa Mahakimu au sijui ni kwa sababu ya ugumu wa kesi zenyewe. Kuna mwananchi mmoja alinisikitikia kwamba wana shamba

lao la mirathi ina mgogoro kidogo na imebidi mgogoro ule upelekwe kwenye Mahakama ya Ardhi. Kinachotendeka pale ni kwamba inaakhirishwa kesi kutoka leo mpaka miezi 6 inayokuja.

Mimi nashangaa sijui kwa sababu gani. Na hiyo miezi zite ikifika inapigwa tena tarehe mpaka miezi sita. Kwa kweli hili jana linakatisha tamaa sana. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri suala hili alione ili kesi za ardhi nazo ziende kwa haraka kama ambavyo kesi nyengine za criminal na nyengine zinavyokwenda haraka.

Mhe. Waziri katika ukurasa wa 15 Mhe. Waziri naomba ninukuu kidogo hapa ametupa habari za Mahakama hii ya Biashara. Lakini akatwambia hatua za matengenezo ya jengo litakalotumika kama Mahkama ya Biashara zinaendelea vizuri. Huku mwisho akasema hata hivyo imebidi matengenezo hayo yachelewe baada ya kukosa msaada wa fedha kutoka mradi wa BEST. Huko nyuma kidogo nilipata habari kama BEST waliwahi kutoa pesa, tena sio kwa matengenezo ya jengo ni kwa ajili ya jengo jipya na pesa hazikuwa kidogo zingeweza kumudu kujenga jengo jipya. Nilitaka ufafanuzi tu Mhe. Waziri atwambie pesa hizi hazikuwahi kutolewa au zilizolewa zikafanyiwa kazi gani mpaka ikabidi leo serikali sasa ndio inajikamua kamua kutengeneza jengo kongwe kwa ajili ya kuendeshea Mahakama hii ya Biashara.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka niende kwenye ukurasa wa 12 ambayo kwa kauli ya Mhe. Waziri mwenyewe na mimi hichi ndio kilio changu cha siku nyingi Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu kidogo Waziri alivyosema, paragrafu ya 30 inasema:

> "Wizara yangu inafahamu sana kuwa utendaji wa baadhi ya wafanyakazi wakiwemo makarani na Mahakimu hauridhishi, rushwa, uwamuzi wa kesi hasa za madawa ya kulevya, kesi za ubakaji na mashauri yanayohusu ardhi, miongoni mwa mambo yanayolalamikiwa sana na wananchi."

Mhe. Naibu Spika, nikinukuu kifungu hichi kwa sababu niliwahi kusema kwamba kuna ukiukwaji mkubwa wa maadili ya Mahakimu. *Indicator* zinaonesha kwamba kuna tabia ya rushwa kwa Mahakimu lazima niseme hivyo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna kijiji kule kwetu Pemba kuna watu wana tabia mbaya, wanauza bangi na jeshi la polisi baada ya kupewa ripoti na wasamaria wema wamefanya juhudi kubwa sana na nawapongeza sana. Wamekwenda wakawakamata wauza bangi wale, wakawafungulia kesi. Lakini kesi zao pale Mahakamani kila kesi inayopelekwa wamekamatwa si chini ya mara mbili au

mara tatu mtu huyo huyo mmoja. La kusikitisha zaidi mara nyengine anaekamata ni RCO wa Mkoa ni mtu mmoja ambaye anaaminika sana ndio maana kapewa kile cheo. Leo anakwenda mpaka Mhakamani anatoa ushahidi lakini Mahakama bado inashindwa kuthibitisha kwamba yule mtu ni mtenda kosa.

Kinachotokea ni kwamba anawauzia watu bangi, wanavuta bangi na wanafanya uhalifu tena mkubwa. Kuna polisi jamii siku hizi, wamewakamata wakawapeleka si chini ya mara mbili au mara tatu. Mahakama hakuna kinachofanyika, watu wale wanaachiwa, wanakuja tena wanafanya makosa yale yale. Kama kiongozi wa wananchi nikamuendea RPC wa Mkoa wa Kusini Pemba. Nikamwambia RPC maneno ninayoyasikia mitaani yanatisha, wananchi sasa wamekosa imani na jeshi la Polisi, wamekosa imani na Mahakama. Kwa sababu wahalifu wapo wanawaadhibu, wanafanya juhudi wanawakamata wanawapeleka lakini hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Sasa mtu akikosa imani anaweza akafanya jambo jengine baya zaidi. Nilikuwa naomba sana kama ni wadau wa masuala haya mchukue hatua. Nakumbuka hata Mhe. Waziri nilimwambia na Mhe. Waziri alikwenda mpaka Pemba kwa taarifa alizonipa akazungumza nao. Mhe. Naibu Spika, hakuna hatua iliyochukuliwa, uhalifu uliendelea.

Mhe. Naibu spika, kuna muhalifu mmoja akawakata ng'ombe watano miguu. Kesi ikapelekwa hakuna hatua iliyochukuliwa. Kisema unaambiwa ushahidi haukukamilika. Sijui maana yake ushahidi uwe vipi, ng'ombe wa watu watano kasha wakata miguu, mashahidi wamekwenda wamesena ni yeye, kwa kauli yake akasema nitamfanyishia fulani na kitendo kimefanyika bado ushahidi haupatikani. Sikusudii kuingilia uwamuzi wa Mahakama wala upelelezi maana mimi si mpelelezi. Lakini mazingira yanaonesha hivyo, lakini akaachiwa. Mara ya pili kamkamata punda kampiga mapanga akamuuwa, akapelekwa pia akaachiwa. Mara ya tatu kamtundika punda kamuuwa, huyo huyo.

Mhe. Naibu Spika, haki haitendeki sasa kama haitendeki mimi kwa tafsiri nyengine nasema ni kumvunjia haki yake ya kibinaadamu huyu kijana anayefanya hivi. Kwa sababu unapomuona ni muhalifu ukamkamata na kosa ukamtia hatiani, ukampeleka jela, umemnusuru na mambo mengi huku. Lakini kijana huyo Mhe. Naibu Spika, baada ya kuona Serikali inashindwa kuchua hatua sijui nani lakini watu wamemkamata usiku mmoja wakampiga mpaka macho yake yamepotea. Haya yote yanatokana kwamba haki haikutendeka.

Mhe. Naibu Spika, mara moja mimi nilikuwa jela. Nilipofika kule jela nilimkuta mtoto mdogo, napenda sana kuitoa hiyo hadithi. kwa sababu ni *very*

interesting. Nilimkuta mtoto mdogo kafungwa, kifupi, kidogo dogo, wale askari wa jela kule wamwita kijukuu, maana yake ni kidogo hivi. Mimi nikauliza jamani hata huyu kulikoni wakanambia huyu mtoto ni mkorofi, baba yake Mzazi ndio kenda kumwambia Jaji huyu mtoto mfunge. Hakimu akashangaa wewe mzee lakini una akili timamu wewe nimfunge mtoto wako kweli huyu ni mtoto wako. Akamwambia ni mtoto wangu, nimemzaa mwenyewe naomba umfunge. Kwa sababu kama hukumfunga mimi sipati utulivu, hata usingizi hauji kwa tabia zake.

Hakimu yule akasikiliza busara za mzee zile akampeleka jela yule mtoto. Akawa jela mzee huko akawa kapumua kwa sababu anajua mwanawe yuko jela lakini yeye akawa kapumua. Kilichomfanya apumue kwa sababu hapati zile hadithi kwamba mwanao kakosewa jiwe, kakosewa panga, mwanao hivi hapati tena zile hadithi. Lakini muda ulifika akamaliza katoka, siku aliyotoka wiki haikufika kenda kuingia nyumba ya mtu kaiba kakamatwa kapigwa mapanga kauliwa.

Sasa ikiwa Mahakama haikufanya kuwaadhibu watu, watu watahukumu kwa mikono yao Mhe. Naibu Spika, ndio tatizo langu lilipo hapo. Sasa kwa nini watu hawahukumiwi kwa sababu anakwenda mtu na kesi, kesi ikishakumkalia vibaya hatulii mtu yule, atamuendea Jaji pembeni pembeni huko bwana nisaidie. Atamwambia sasa kama unataka nikusaidie lete kitu fulanni. Sasa yule hata rumande hawekwi, anaambiwa basi nenda katafute, kama alishtakiwa kwa kuiba ng'ombe anakwenda kuiba ng'ombe mwengine auze apate pesa akampe Jaji huo ndio ukweli.

Sasa hizi Mhe. Naibu Spika, ni jambo moja baya sana. Nilikuwa nadhani kuna Jopo hapa nimelikuta linaitwa kwamba ni "Jopo la Kuharakisha Kesi" nilikuwa naomba sana hili jopo lisiangalie tu kuharakisha kesi lakini liangalie hata mienendo ya Mahakimu wetu, tabia zao. Mheshimiwa Hakimu akishakuwa hatekelezi wajibu wake anaweza akasababisha maafa makubwa sana. Nilikuwa naomba sana hilo alifanyie kazi.

Halafu nimeona katika kitabu hichi na ni manung'uniko ya siku nyingi haya. Kule Pemba hakuna Jaji Mkaazi wa Mahakama Kuu, kule Pemba hayupo, sasa mtokeo yake kila mwezi wanapangwa Majaji wawili kutoka hapa kwenda Pemba kusikiliza kesi. Lakini posho la Jaji mmoja kumtoa hapa kumpeleka Pemba Mhe. Naibu Spika, ni pesa nyingi, yule ni mtu mkubwa Jaji wa Mahakama Kuu ni mtu mkubwa si chini ya laki 7 kwa Majaji wawili hizo ni shilingi milioni moja na laki nne, kila mwezi wanakwenda, milioni moja na laki nne mara kumi na mbili ni pesa nyingi sana Mheshimiwa. Sasa kwa nini hatuweki Jaji kule akawa yeye yuko wa kudumu Jaji mkaazi kule Pemba haondoki akawa anashughulikia zile kesi za Mahkama Kuu tu kuliko kila siku

kugharimika kutoa Jaji hapa kwa pesa nyingi ukimpeleka kule ninafikiri Waziri atatueleza. Mahkama moja katika kazi zake ni kutafsiri sheria lakini mara nyengine ni kutoa haki. Mimi nilikuwa naomba sana tubadilishe kidogo tusiseme kama mahkama inatoa haki.

Na ninasema hivi kwa sababu mahkama zinasikiliza kesi za madai zinatoa uamuzi, lakini ule uamuzi wa mahkama hauheshimiwi, matokeo kama kulikuwa na mtu apate haki yake mahkama ishaamua lakini anaendelea kuwa haki yake haipati. Sasa tuseme mahkama badala ya kutoa haki zinatenda haki. Mambo mawili tofauti hapo kutoa haki na kutenda haki maana ya kutenda haki nini? Ni kutafsiri kwamba mwenye haki ni huyu huku ni kutenda haki. Lakini mtoaji haki ni yule mtu mwenyewe aliyelalamikiwa. Mhe. Naibu Spika, maana yangu hapo ni kwamba maamuzi ya mahkama yaheshimiwe.

Nikiondoka hapo hapo haraka haraka niangalie Ofisi ya Mufti ukurasa wa 30 Mhe. Naibu Spika, ndipo penye Ofisi ya Mufti na miongozo yake hiyo ni sehemu ya utulivu wa jamii yetu. Lakini jambo la kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika, mpaka leo hana gari ya kufanyia kazi zake, ni gari ya kugaiwa tena bovu na huyo aliyemgaia naona aibu hata kumtaja. Maana yake haiwezekani yeye akamgaie Mhe. Mufti gari. Nilikuwa naangalia kwenye fungu la Ofisi ya Mufti hapa, kwenye hili tabu kubwa nikakutia kuna milioni 249741 nikafikiri labda katika hizi mna manunuzi ya gari, nikenda katika kifungu 311200 ununuzi wa mashine na zana nikakuta hapana gari hata moja pale pana friji na kompyuta basi fungu lile lina shilingi milioni nne na laki moja.

Na ukiangalia hata ofisi ya Pemba na pale pana milioni mbili na laki tano. Yeye kaambiwa atanunuliwa Honda, vespa na ciao Naibu Mufti labda huyu. Sasa kwa kifupi ofisi ya Mufti bado haijafanyiwa haki nilikuwa naomba sana yule ni mtu mkubwa, ni mtu aliyekuwa hawezi harakati za kutembea kwa miguu kutokana na umri na mazingira yake. Kwa hivyo Wizara ifanye juhudi hata ikibidi kufanya *re-allocation* Mhe. Naibu Spika, naomba Waziri afanye *re-allocation* lakini tuone katika mwaka huu Mhe. Mufti anapata gari ya kufanyia shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine muhimu sana ambalo nimetaka nilizungumze kwa ufupi ofisi hii ya Mufti moja katika kazi zake ni kufanya uratibu wa madrasa, wanapita kwenye taasisi za dini, wanapita kwenye madrasa za kur-ani. Kwa masikitiko makubwa Mhe. Naibu Spika, kumezuka wimbi la watu wanaojiita wao ni walimu wa chuoni, lakini wanajenga mabanda wanakusanya watoto wa watu halafu wanawafanyia mambo yasiyostahiki. Hili wimbi lipo kubwa na anaweza akafanya hapa akeshagunduliwa akahama mtaa huu akenda akahamia mtaa mwengine

akenda akafanya kama hivyo. Nilikuwa ninaiomba sana Ofisi ya Mufti ifanye utafiti wa karibu sana kujua tabia za walimu wanaosomesha madrasa, wengine wana tabia chafu sana ninafikiri nikisema hivyo ninafahamika.

Lakini ikiwezekana hata kutayarisha utaratibu wa leseni japo hilo litapigiwa makelele sana, lakini mtu aliyekuwa tabia yake ni mbaya asipewe ruhusa ya kukusanya watoto wa watu hili jambo limetokea sana Mhe. Naibu Spika.

Nataka niipongeze sana Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Wakfu niliwahi kusema mara mbili tatu hapa, Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 49 Kamisheni ya Wakfu imetueleza kwamba tayari wamefungua *account* maalum ya zakka katika Benki ya Kiislam ya PBZ na tayari imeshaanza kufanya kazi *account* na tayari watu wanaanza kuweka zakka zao. Hili suala nimelizungumza siku nyingi ndani ya nchi yetu kuna watu wengine wana uwezo wa kutoa zakka lakini hawana mioyo ya kutoa zakka, wengine wana uwezo wa kutoa zakka na mioyo ya kutoa zakka wanayo lakini kulikuwa hakujawa na uratibu. Sasa Kamisheni ya Wakfu imefanya juhudi hii nilikuwa naomba sana kwanza niwapongeze lakini pili wafanye juhudi maalum ya kuhamasisha watu watoe zakka. Mhe. Naibu Spika, nchi hii ina maskini sana hii, lakini kuna maskini waliopindukia lakini kuna watu walio na utajiri uliopindukia, wakihamasishwa vizuri wanaweza wakaweka *balance*. Na itatusaidia kuondoa mabalaa mengi kwa sababu moja katika dhambi kubwa Mhe. Spika, zakka ni nguzo ya kiislam. Moja katika dhambi kubwa ni mtu kuwa na uwezo wa kutoa zakka akawa hatoi zakka. Tunaweza tukajishtukia siku moja katika nchi yetu tunapata mabalaa kwa sababu ya kukiuka amri hii. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Kamisheni ya Wakfu ifanye juhudi ya kukusanya zakka na kuhamasisha.

Katika Ofisi ya Mrajis nitasema maneno mawili Mhe. Naibu Spika, muda sina tena lakini Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, nakumbuka niliwahi kusema mara moja hapa kwamba ninaipongeza hii ofisi kwa kuondoa tatizo la madai ya vyeti. Nimeambiwa katika bajeti hii wametayarisha magamba ya vyeti karibu 20,000 ambayo yaliweza kukidhi haja ya mahitaji yaliopo. Lakini tatizo la Ofisi hii wanatumia yale mataipu sijui kwa nini, mimi ninashindwa kujua kuna hekma gani mpaka leo katika nchi hii kuna makompyuta kila ofisi lakini vyeti vya kuzaliwa vinapigwa na mataipreta yale hayaandiki vizuri na sasa hivi kuna malalamiko mengi vyeti vya watu vinakosewa. Na sisi siku hizi Mhe. Naibu Spika, cheti ukikosea herufi moja tu, maana yake *system* iliyopo ni ya mtandao, *computerization*, kompyuta haikubali kupokea ndio maana kuna malalamiko watu wanakwenda na vyeti vyao wanashindwa kupata paspoti, wanakwenda na vyeti vyao wanashindwa kupata vitambulisho vyengine vya kura na nini. Sasa kwa nini hatubadiliki? Tukatafuta mashine nzuri za kuandikia.

Jambo la mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, ninajua unaniangalia jana tulikuwa na semina, moja katika mambo ambayo nilijifunza yaliyonisikitisha ni kwamba hii Zanzibar kukosa *sovereignity*, sasa tunawakilishwa kila kitu kuna sheria za kimataifa wenzetu Tanzania Bara kule wanakwenda wakifika wanaridhia sheria za kimataifa zile kama zilivyo, maana angalau kuna nchi nyengine wanapembua wanasema tunaridhia lakini kwa sharti kifungu hiki na hiki hatukubali kwa mujibu wa silka na tabia zetu na dini zetu na nini. Lakini wao wanaridhia kila kitu wenzetu Tanzania Bara kule, matokeo yake kuna mikataba ya kimataifa inatufunga mpaka sisi Wazanzibari maana sisi tumo ndani ya Tanzania. Unakuta jambo Fulani hili ni haki lakini kwa mujibu wa ibada zetu, dini zetu na desturi zetu zile si haki kwetu sisi. Sasa kwa nini hawamchukui Mwanasheria wetu wa Zanzibar akenda kule akawa yeye anajua mazingira yetu ya Zanzibar, kwamba hili ukilipeleka Zanzibar halitapokelewa na linaweza kuwa ni sababu ya mzozo litakataliwa. Lakini wao wanakwenda kwa sababu ya mwamvuli wa Muungano, na kwa sababu Zanzibar haijulikani kimataifa wanatuletea mambo ambayo hayatufai.

Sasa Mhe. Mwanasheria yupo, Mhe. Waziri wa Katiba yupo na sisi kama Baraza tupo, kuna sheria za haki za watoto imepokelewa kama ilivyo, miongoni mwa yaliyotajwa mule ni kwamba mtoto ana haki ya kufuata dini atakayo. Sasa sisi kama ni waislamu tunaoamini uislamu hivyo Mhe. Naibu Spika, hivyo wewe unaweza kumuacha mwanao akaacha kufuata uislamu akafuata dini nyengine anayotaka? Uislam sisi hauturuhusu kufanya hivyo. Jambo kama hili wenzetu wairaq waliliekea *objection* wakasema sisi tutaichukua sheria hii lakini hili hatulitaki kwa sababu haliendani na dini yetu na wakaruhusiwa. Sisi kwa sababu hatuna Mwakilishi wetu kule Tanzania wameyachukua kama yalivyo, matokeo yake hapa hayatekelezeki. Na kwa sababu umeshaambiwa ni haki ya kimataifa ukimrudi mwanao kwa hilo sasa unaingia katika kuvunja haki, jambo ambalo kiislam si haki kweli. Sasa nilikuwa naomba sana tutafute upenyo lakini hili kwa kweli sisi wengine hatuko radhi kuendelea kama hivi lilivyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kwisha kusema hayo mimi naunga mkono hoja hii ya bajeti kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru bwana wetu muumba azza wajalla kwa kutujaalia neema zake akatujaalia kuwa hai na wazima tukiendelea na mjadala wetu. Nakushukuru na wewe Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ila nikutaarifu mapema tu umuombe Mhe. Jaku ajiandae kwa jioni tukijaaliwa.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kupoteza muda naomba na mimi nichangie machache, kwanza nithibitishe yale ambayo yamesomwa na Kamati kama ni maoni ambayo tumeyatoa nadhani Waziri atayafanyia kazi lakini nje ya yale Mhe. Naibu Spika, yapo machache naomba niyazungumze.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, niungane na wote kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake. Kama ilivyosemwa katika hotuba ya Kamati ni wizara yenye watendaji makini, mahiri wanaozitambua fani zao na ndio maana wanafanya kazi kubwa ya kurejesha imani ya wananchi katika taasisi mbali mbali ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, niruhusu nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Asaa kwa heshima kubwa aliyopewa ya kutuwakilisha wazanzibari akiwa Katibu katika Tume ya Kukusanya Maoni. Lakini vile vile kwa heshima ya chombo hiki Mhe. Naibu Spika, nimpongeze na Ndugu Mdungi kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara. Nimpongeze na aliyekuwa Katibu wetu Mhe. Ibrahim Mzee ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Mashtaka. Hiyo inathibitisha kwamba Baraza hili linaandaa vizuri watu wa kuja kuchukua dhamana kubwa kubwa katika nchi yetu. Na hii ni fakhari kwa chombo hiki Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa sikamilishi shukurani zangu kama sikuungama na mimi kumpa heshima ya aina yake na pongezi nyingi Mhe. Mwanasheria Mkuu Mhe. Othman Masoud. Kama mimi ningeliambiwa nichague mfanyakazi bora katika Zanzibar hii ningemtunuku cheti hicho Mhe. Othman Masoud. Kazi nzuri kaifanya katika Idara ya Muendesha Mashtaka au Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na sasa kazi kama hiyo anaifanya katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, pongezi hizo ziwe kwa niaba ya watendaji wengine wote wa Wizara hii ambao wanafanya kazi nzuri. Mhe. Naibu Spika, nimemsahau na mmoja Mhe. Jaji Mkuu tangu ameteuliwa tunaanza kuona mabadiliko katika mahkama anazoziongoza, wote hawa niwatakie kila la kheri katika kuendelea kuitumikia nchi yetu na watu wake.

Mhe. Naibu Spika, haraka haraka niyaguse maeneo ambayo yanahusu Wizara hii. Kwanza Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza Wizara na Waziri kwa kusimamia mara hii kuongeza fungu la bajeti kwa Ofisi ya Mufti. Mhe. Naibu Spika, ilikuwa inasikitisha tulipokuwa tunatembelea Ofisi hii ilikuwa haipewi umuhimu. Lakini mara hii tumeona bajeti yake imepanda sana bado haitoshi hakuna kinachotosha, lakini angalau kuna mabadiliko makubwa kutoka mwaka jana. Lakini kwa kutenga fungu dogo la kuihudumia Ofisi ya Mufti kwa Pemba kuifanya ofisi hiyo iweze kufanya kazi katika visiwa vyote viwili Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze vile vile Wizara hii kwa kuja na muongozo wa zakka na kuweka utaratibu sasa wa kukusanya na kutoa zakka ambao kwa wale wananchi ambao wanataka kutoa zakka zao kupitia ofisi hii. Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo kuna maeneo machache ambayo ningemuomba Mhe. Waziri haya akayatupia macho.

La kwanza Mhe. Naibu Spika, linahusu utekelezaji wa hukumu. Mjumbe aliyetangulia hapa kasema Mhe. Naibu Spika, mwananchi anapokuwa amefika kikomo cha kutafuta haki yake hukimbilia mahkamani, na ni imani yetu kwamba atapofika kupata hukumu akapata haki yake mahkamani basi vyombo vya nchi vimsimamie kupata haki yake. Sasa Mheshimiwa kumejengeka utaratibu katika nchi yetu kwamba kuna kesi zinakwenda mahkamani lakini tunajenga mfumo kudhani kwamba kuna watu wako juu ya sheria kwamba wako *above the law*.

Mhe. Naibu Spika, mifano iko mingi nataka kutoa mfano mmoja tu. Kuna kesi tuliizungujmza juzi hapa kesi ye eneo la Shakani na maeneo yanayohusiana na hayo. Kuna watu tu Mhe. Naibu Spika, kina Bwana Abdalla Rashid, Bwana Mohd Hija kwa kujidhani kuwa wao wako juu ya sheria wanafika kila inapotaka kutekelezwa hukumu ya kesi ambayo mpaka Mzee yule amefika kuondoka duniani na leo warithi wake wanaendelea kuumbuka kwa kukosa haki zao, kwa sababu kila ikitaka kutekelezwa haki ile tunaambiwa wanatoka na mikuki na mishale ati kuwazuia Polisi kutosimamia vyema suala la utekelezaji wa hukumu ile ambayo imefika katika Mahkama ya rufaa Mhe. Naibu Spika.

Lakini ziko na kesi nyengine siku hizi nyingi wananchi wanalalamika kwamba wanakwenda Mahkamani zinatolewa hukumu hazipati kutekelezwa. Nataka kumuomba Mhe. Waziri akija anisaidie kwamba wananchi kama hawa wakifika hapo wafanye nini ili wapate haki yao ikiwa wameshafika mwisho kabisa wa ukomo wa kwenda kutafuta haki yao. Hili Mheshimiwa halipendezi na wala halitoi picha nzuri katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile nigusie suala la mahkama Mhe. Waziri katika kitabu chake ukurasa wa 13 kaligusa. Suala la kusema kwamba bado kuna malalamiko kuhusu rushwa katika mahkama zetu. Na hii nataka kusema Mhe. Naibu Spika, liko katika mahkama hizi zetu za kawaida kwa maana ya mahkama kuu na mahkama zake. Lakini pia katika mahkama za Kadhi. Mhe. Naibu Spika, kuna kesi moja inahusu katika hao Makadhi wake wapya ambao Mhe. Waziri katwambia wameteuliwa ili kuziba lile pengo. Kuna kesi ya madai unakuta upande mmoja kwenda kufanya utafiti kazi anawasiliana upande mmoja ana jumla ya simu mia mbili anawasiliana na Wakili na mteja

upande mmoja. Unajiuliza wewe mtu kama huyu kweli ataweza kusimamia haki katika kesi kama hiyo?

Suala hili limepelekwa katika vyombo huko linachunguzwa lakini Mhe. Naibu Spika, haya ni mambo ambayo wananchi wengi wanayalalamikia kwamba yanapelekea watu kupoteza imani na vyombo hivi katika kupata haki zao. Kwa hivyo nilikuwa nasema tunaona utaratibu unafanywa, tunaona Jaji Mkuu mpya anajitahidi kutembelea na kutoa maagizo kila wakati, tunaona kazi inayofanywa na Mrajis wa Mahkama katika kusimamia hili, ninawapongeza wote lakini bado kuna *challenge* kubwa walisimamie.

Sambamba na hilo Mhe. Naibu Spika, kuna lile suala la kukosekana kwa kanuni zinazoongoza mwenendo wa kesi katika mahkama ya Kadhi, matokeo yake tumegundua kwamba wengi wanafanya kazi kwa mazoea tu na kwa mujibu wa akili yake inavyomtuma lakini hana muongozo. Tuliwahi kuliuliza hili katika Kamati tukaambiwa walitakiwa watumie zile kanuni zinazoongoza mwenendo wa kawaida wa kesi za madai katika mahkama za kawaida. Lakini tumegundua baadae kwa maelezo ya watendaji wenyewe wa mahkama, kwamba hata hizo hazitumiki kwa sababu hao Makadhi wenyewe kuzielewa hawazielewi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nasema ninafurahi kwamba sasa Wizara inafanya juhudi ya kuona kwamba inafanya mapitio ya sheria ya Kadhi ile ya Mahkama ya Kadhi lakini pia na kanuni zake nikiamini kwamba hilo litasaidia kunyanyua ule mfumo mzima wa utendaji kazi na utoaji wa haki.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia haraka haraka nigusie Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Wamejitahidi wamefanya marekebisho ninafurahi lakini mimi naomba pia katika mafungu haya Mhe. Waziri aiangalie Afisi ya Mrajis Pemba na nimetizama katika hili buku la bajeti tumemwambia katika bajeti na hapa narejea tena kwamba ukitizama kidogo bajeti yao mara hii imeshuka na wakati wana mahitaji mengi pale yanakosekana. Masuala ya usafiri na vitu vyengine nilikuwa naomba pia alitizame kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, naomba pia nizungumze kidogo katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwanza nianze na suala la hija. Waheshimiwa ziko taarifa kwamba pamoja na kwamba Kamisheni hii ndio iliyopewa dhamana ya kusimamia hija lakini kwa sababu kule Saudi Arabia nchi inayotambulika ni Jamhuri ya Muungano, ndio katika yale yale makero yasiyokwisha tunaambiwa kuna kitu kinaitwa *Biitha* ndio inayotambulika lakini *biitha* haiko hapa. Sasa hawa wote mawakala wa hija hapa Zanzibar wanakusanya mambo yao wapeleke kule wao ndio wanao-*process* masuala yote ya kupata visa kupeleka orodha na mapema kujua ndege gani ndio itakayotumika ili

maandalizi yafanywe. Tunaambiwa hivi sasa hivi washafunga Saudi Arabia lakini Tanzania hawajapeleka mahitaji yale.

Sasa inawezekana kwamba huku wameshafanya kazi yao Zanzibar lakini kwa sababu hakuna usimamizi haziendi kwa sababu ndio yale matatizo ya mwisho mwisho ndege haijulikani ipi, usafiri unakuwa mashaka mambo mengi Mheshimiwa bado yanaleta matatizo makubwa. Kwa hivyo nasema tunajua kuna malalamiko ya wananchi kwa hizo taasisi za binafsi na hii *biitha* Mhe. Waziri aifuatilie atwambie kuna tatizo gani kwamba mpaka leo haikutekeleza wajibu wake, matokeo yake wanaathirika wao huko ndugu zetu wa damu lakini mpaka sisi huku Zanzibar tunaathirika kwa sababu tunatumia hii ofisi moja. Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri akija anipe maelezo.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo katika Kamisheni ya Wakfu ninashukuru kwamba Waziri kalieleza katika kitabu chake suala la kupandisha kodi nyumba za wakfu na amelitolea maelezo marefu. Hili tumelizungumza muda mrefu Mhe. Naibu Spika, mimi na yeye hata katika Kamati, kwa sababu watu wengi waliokuwa wanatumia nyumba za wakfu wapo katika Jimbo la Mji Mkongwe na wengine wapo katika Jimbo la Chake Chake katika kisiwa cha Pemba.

Sasa hili nakumbuka tulikubaliana na Mhe. Waziri katika Kamati kwamba ili hoja zieleweke na wananchi wapate kumaliza ile kiu yao na malalamiko yao, basi ningemuomba Waziri afanye kikao kimoja Unguja, kimoja Pemba kwa sababu watu wenyewe wote wako maeneo mamoja ili awaeleze hizi hoja na wao yale malalamiko yao wapate ile faraja wamesikilizwa na Waziri mwenyewe apate kuyamaliza. Kwa sababu akitaka kumpokea mmoja mmoja wako wengi sana Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri alizingatie ili baada ya kumaliza bajeti yake hii apange siku ili na sisi tusaidiane nae Wawakilishi wa maeneo haya mawili ili tupate kutoa maelezo ili yawakinaishe wananchi kutokana na malalamiko yao ambayo wanayo.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala hapa limezungumzwa ukitizama hotuba ya bajeti, kwenye maeneo ya michango ya washirika wa maendeleo utakuta kuna asilimia tano tu ya fedha ambazo zimetolewa. Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kuna maelezo hapa Waziri hakuyasema na pengine kwa nia njema lakini mimi nataka niyaseme. Maana yake mara nyengine ukimstahi mke ndugu hutozaa nae Mhe. Naibu Spika. Mheshimiwa tumefuatilia hili na tuliambiwa ndani ya Kamati kwamba sababu moja iliyokuwepo hapa ni choyo na husda ya ndugu zetu wa damu. Mradi huu wa BEST unaratibiwa kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano lakini kuna fungu la fedha linakuja Zanzibar kuna fungu linabakia Tanganyika.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunaambiwa kulikuwa na fedha ambazo hazijaombwa hapa watendaji watujibu hili, walipofika kuziomba World Bank wanawaambia mnaweza kuziomba ambao wanaosimamia huu mradi. Kwa hivyo ziombeni kabla ya huu mwaka wa fedha haujamalizika mnawahi. Lakini kwa sababu anayesimamia ni bwana mkubwa sie hatuna mamlaka wale wamekwamisha kule tunajua mara nyingi utoaji wa fedha hizi mara zote za washirika maendeleo hazifiki 100 *percent* mara chache sinafika asilimia mia moja. Lakini asilimia tano ni kutokana na hujuma. Sasa Mhe. Naibu Spika, mambo kama haya yaliyotufikisha pale tukasema tunapoteza imani na ndugu zetu hawa kwamba kweli wana nia njema na sisi hawa? Kwa hivyo nilitegemea Waziri aliguse kwa faida ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu sisi ni Wawakilishi wa wananchi Mhe. Naibu Spika, hili limejibiwa katika Kamati limetusikitisha limetuvunja moyo sana na linazidi kuturudishia imani kwamba ndugu zetu hawa hawana nia njema na sisi, na imefika pahala wengine wakasema waachiwe wapumue Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie katika suala kubwa na muhimu kuliko yote katika Wizara hii. Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yake Mhe. Waziri ukurasa wa 54 amezungumzia suala la marekebisho ya Katiba na utaratibu unaoendelea hivi sasa wa ukusanyaji wa maoni. Ninafurahi Mhe. Naibu Spika, kwamba Mhe. Waziri katika hotuba yake hii kasema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itasimamia na kuheshimu mawazo na maoni ya wananchi wa Zanzibar.

Mimi sina sababu ya kutomuamini Mhe. Waziri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kwamba Rais wetu Dr. Ali Mohammed Shein atatuongoza katika kusimamia kile ambacho Wazanzibari wanakitaka na watakidai kupitia utaratibu huu ambao umewekwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna suala hapa ambalo linazungumzwa na Mhe. Waziri kaligusa kwamba wananchi wetu wamekosa elimu mapema, na katika kosa kubwa tutakalolifanya katika *process* hii Mhe. Naibu Spika, ni kwenda tukiwa tumegawanyika wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, muungano huu ulipoundwa haukushirikisha vyama, Zanzibar kulikuwa kuna Afro Shirazi na Tanganyika kulikuwa kuna Tanu, lakini hawakukutanisha halmashauri za vyama hivi wala marehemu Mzee Abeid Amani Karume Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar aliposhiriki katika mazungumzo yale hakwenda kama Rais wa Afro Shirazi kenda kama Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Na vile vile Mhe. Julius Nyerere kule kaja hapa kama Rais wa Jamhuri ya Tanganyika hakuja kama Rais wa Tanu.

Sasa tutakuja kufanya makosa makubwa Mhe. Naibu Spika, leo ambapo tumepata fursa ya mwanzo ambayo ilikosekana ikaakhirishwa kwa muda usiojulikana mwaka 1965 na kushiriki katika kuamua hatma ya Muungano huu tukaipeleka kivyama ile Mhe. Naibu Spika. Na mimi ninashukuru *reference* yangu katika hili sio kiongozi wa chama cha wananchi CUF kuna waraka mimi nawaomba viongozi wenu wakausome uliandikwa na sasa hivi Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Pius Msekwa aliuandika mwaka 1994, na baadae ameuingiza katika kitabu chake, kile kitabu ninacho na waraka ule ninao. Akikosoa hatua ya mwaka 1994 wakati linakwenda kufutwa azimio la kudai serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano, akakosoa utaratibu uliotumika kulifanya suala la chama na yeye kaandika kwa maelezo fasaha na uchambuzi mzuri sana Mhe. Pius Msekwa kwamba muungano huu haukushirikisha Afro Shirazi na Tanu. Na kwa hivyo leo kulifanya suala la Muungano ni sera ya Chama ni makosa.

Lakini niseme makosa haya sote tumeyafanya, ukienda katika CUF ndani yake inayo sera kuhusu muungano, ukienda katika CCM ilani yake inayo sera kuhusu muungano. Lakini nasema sasa hivi wakati Wazanzibari tunafikiria na kuamua hatma na mustakbali wetu Mheshimiwa tutafanya makosa makubwa sana tukirudi katika vyama, tukataka misimamo ya vyama ndio ituongoze.

Mhe. Naibu Spika, CUF ina sera ya Serikali tatu mimi lakini pamoja na kuwa Unaibu Katibu Mkuu wangu siamini kwamba sera ya Serikali tatu kwa sasa itaisaidia Zanzibar. Kama ambavyo siamini kwamba sera za serikali mbili hizi ziliopo sasa ambao ni sera ya CCM kama itaisaidia Zanzibar vile vile. Mhe. Naibu Spika, mimi naamini wanachokihitaji wazanzibari hivi sasa wanataka kuona Jamhuri ya Watu wa Zanzibar inasimama tena ikiwa na mamlaka kamili ya kitaifa na kimataifa. Wanataka kuona lile tamko alilolitoa Mzee Abeid Amaan Karume wakati huo ikiitwa *Sauti ya Unguja* tarehe 15 Januari na nimesoma sana Mhe. Naibu Spika, maana imo katika kitabu cha Afro Shirazi katika *library* yangu kiko nyumbani pale, alipotangaza kuanzia leo Zanzibar ni nchi huru na haitoingiliwa na mtu yeyote katika kuamua mamlaka yake. Lakini kisha likasimamishwa katika zile sheria kuu 5 za mwanzo; *decree* za Baraza la Mapinduzi zikieleza mwelekeo wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, wazanzibari wamechoka kudhalilishwa kwamba leo mnakutana mkutano wa viongozi wa Afrika Mashariki lakini Rais wa Zanzibar anakwenda pale kama mgeni mualikwa. Rwanda na Burundi waliokaribishwa juzi Rais wao anaingia pale ana maamuzi wetu sisi anafinywafinywa. Mhe. Naibu Spika, hili wazanzibari limewachosha. Na katika hili niseme kabisa Mhe. Naibu Spika, nasikia katika huko kujitwika madaraka ya kutuamulia mambo yetu kando ya pili ya bahari huku ninasikia suala la Afrika Mashariki limeshafika pahala sasa kumeandaliwa rasimu ya

Katiba ati ya Shirikisho la Afrika Mashariki inayoitaka kuifunga Zanzibar na haki zake huku wazanzibari wenyewe hatujui Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Waziri akija anambie analitambua suala hili na kama analitambua nini *position* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dr. Ali Mohammed Shein ikiwa na muundo wa Umoja wa Kitaifa katika suala hilo tumeshirikishwa kiasi gani tuna maamuzi gani.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba wazanzibari wanachotaka ni mamlaka kamili. Siku ya kuchangia Afisi ya Makamo wa Pili nilisema kwa urefu hapa ni kiasi gani kukosa mamlaka ya kusimamia mambo ya nje, uhusiano wa kimataifa ulivyotukosesha *sovereignty* na kutufanya hata yale mambo yasiyokuwa ya muungano tukitoka nje ya Jamhuri ya Muungano inakuwa ya Muungano. Kwa hivyo wazanzibari wanataka mamlaka kamili. Tunahitaji kuiona Zanzibar ambayo inaweza kujisimamia wenyewe iwe na Serikali yake kamili, Rais wake awe na uwezo wa kuingia Umoja wa Mataifa kuiwakilisha Zanzibar ahutubie Umoja wa Kimataifa akiwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tunataka Zanzibar ambayo ina sarafu yake na Benki Kuu yake, tunahitaji kuwa na Zanzibar ina Waziri wake wa mambo ya nje, tunahitaji kuiona Zanzibar ina mamlaka yake kamili Mhe. Naibu Spika, na hayo ndio madai ya Wazanzibari. Sasa nasema haya tukiyapeleka kivyama Mheshimiwa tutafanya makosa. Nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, katika hili serikali bado itafakari tena vipi inaweza kuwaunganisha wazanzibari kudai yale wanayotaka. Kwa sababu kuna hatari tukienda katika vyama tukatoka hapa tukawa tumegawanyika kama ilivyokuwa kawaida yetu.

Mhe. Naibu Spika, moja katika makosa makubwa tunayoyafanya sisi ni hayo. Sisi tukitaka kuliendea hili tunagawanywa tunakubali kugawanyika, lakini wenzetu wanapoikabili Zanzibar wanaweka upande tofauti zao za vyama, tofauti za kila kitu. Mimi naamini Mhe. Naibu Spika, kwamba siku zote wenzetu wanayo ajenda ya Tanganyika dhidi ya Zanzibar. Lakini Wazanzibari hatuna ajenda ya Zanzibar kwa Tanganyika tunakwenda tukiwa tumegawanyika gawanyika.

Na Mhe. Naibu Spika, kutaka kulithibitishia hili nitatoa mfano mmoja. Mwaka 1994 kulikuwa na azimio lile la kuundwa kwa Serikali ya Tanganyika katika mfumo wa Muungano. Lilipokuwa linafutwa na *hansard* watu wakaangalie maana inapatikana hata katika mtandao. Aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati ule Mhe. Samuel Sitta alipopeleka azimio la kufuta azimio lile akasema tunaondoa azimio la kuanzisha serikali ya Tanganyika na badala yake tunathibitisha kwamba hatua tutakazochukua ni kuendelea na mfumo wa serikali mbili ambao utatupeleka hatimae katika serikali moja. Hii

ni azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano mwaka 1994 na halijafutwa mpaka leo, ndio kusema bado muelekeo wa wenzetu uko pale pale. Tutajinasibu sana hapa kwamba sisi tutalinda lakini wenzetu wana ajenda na katika ajenda hii ikija haitizami vyama nilikuwa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninalisisitiza sana hili. Na katika hili Mhe. Naibu Spika, niiombe Wizara. Wizara hii ndio tuliyoibebesha jukumu la kusimamia haki za Zanzibar katika huu utaratibu wa kuandika Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano, niwaombe sana katika hili kukwepa kugawanyika tumeteua makamishna kumi na tano kawateua Rais wa Zanzibar kwa niaba yetu ndio sheria inavyosema wametangazwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano hawa wanaiwakilisha Zanzibar Mhe. Naibu Spika, inawezekana wameteuliwa na kupendekezwa makundi tofauti, naomba sana Wizara iwasimamie kuwaunganisha hawa kwamba wapo pale kwa ajili ya Zanzibar na kusimamia watu wa Zanzibar na watu wake. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema tunahitaji kujua tunachokitaka nini katika *process* hii. Mimi ninajua Wazanzibari wanakijua wanachokitaka katika *process* hii. Na ninaamini watakitaka na mimi naamini sisi kama Wawakilishi wa wananchi tutawasimamia katika kuheshimu maamuzi yatakayotolewa na wazanzibari katika utoaji huu wa maoni. Mimi naamini wenzangu wote kwa sababu tumekuja hapa tumechaguliwa na wazanzibari hawatofanya kosa la kuwadharau wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika hili, utaratibu huu wa kutoa maoni unaongozwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba sura ya 83 toleo la mwaka 2012. Tuliletewa sheria hii hapa kwa mujibu wa ibara 132 ya Katiba ya Zanzibar, lakini tumesikia si mara moja, si mara mbili si mara tatu kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano amethibitisha kwamba bado upo uwezekano wa sheria hii kuendelea kufanyiwa marekebisho. Nakumbuka tulitoa maoni yetu sote kuna mengi yalichukuliwa lakini yapo machache yaliyokuwa hayajarekebishwa. Naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri haya ayachukue kama maoni yangu na ninaamini katika haya nawasemea Wazanzibari katika kuendelea kurekebishwa sheria hii kama wanavyoendelea kuahidi viongozi wengi wa Jamhuri ya Muungano maeneo haya ayatizame tena.

Kwanza ikitokea fursa ya marekebisho wakiangalie tena kifungu cha tisa cha sheria hii. Mimi kwa tafsiri yangu kifungu hiki kinakwenda kinyume na Katiba zetu mbili. Kwa sababu kifungu hiki kifungu cha 9(2) kimeweka maeneo fulani ambayo wananchi wametakiwa haya wasiyaguse, haidhuru katika utoaji wa maoni wameyagusa na hatimaye Mwenyekiti wa Tume kasema kwamba yote mawili watayapokea lakini sheria bado inakataza. Lakini kifungu cha 18 cha katiba zetu zote mbili Mhe. Naibu Spika, kinahakikisha uhuru wa maoni, kwa hivyo sioni sababu ya kuwafunga wananchi kwamba kuna maeneo ambayo wanatakiwa wasiyaguse. Hili ni kama indhari tu.

Katika kifungu cha 17 katika kifungu kidogo cha sheria hii kuna zile sheria ambazo zimetajwa kama ni rejea *reference*, kuna na sheria zilikuwa hazimo tukazikazania sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi zikaingizwa ndio sheria za Zanzibar. Nilikuwa naomba sana Wajumbe wa Zanzibar waliokuwa katika Tume wahakikishe wanasimamia kwamba humu mna mafundisho muhimu wayazingatie yale. Sheria zile zilizotungwa na Baraza la Mapinduzi mara baada ya mapinduzi.

Na kifungu chengine Mhe. Naibu Spika, ni kifungu cha 31(2) ambacho kimetaka kura ya maoni kule mwisho kabisa kwa *process* hii baada ya kupigwa itasimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kura zitahesabiwa Zanzibar lakini matokeo yanapelekwa yakatangazwe kuumeni. Mhe. Naibu Spika, mimi sioni sababu hiyo, haya masuala ya uchaguzi na kura ya maoni si suala la Muungano kila mtu ana yake. Mimi nasema tukifanya marekebisho Mhe. Waziri aangalie haja bado kwamba maoni yatakayotolewa Zanzibar matokeo yake yatangazwe Tume ya Uchaguzi hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa wito wangu kwa wazanzibari niwaombe tena wazanzibari kwamba nchi yetu imefika pahala muhimu sana katika historia yake. Viongozi wetu wengi wa Zanzibar wamesumbuka na wamepata matatizo kwa sababu ya kusimamia haki za Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, katika miaka ya mwanzo ya Mapinduzi Mhe. Abdulazizi Twala aliyekuwa Waziri wa Fedha wa Zanzibar alifika kuandikiana barua kali kali na aliyekuwa Waziri wa Fedha wa Tanganyika katika kusimamia haki za Zanzibar.

Mzee Karume mwaka 1971 waasisi wa Mapinduzi walitwambia aliongoza Baraza la Mapinduzi kwenda kudai haki za msingi za Zanzibar katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano akisema ikiwa hayakubaliwi hayo basi kaeni nayo mpaka mtakapokuwa tayari mtakuja kutujibu, mpaka leo hawakujibiwa. Mzee Jumbe kamalizia kuondolewa Dodoma kwa sababu ya kusimamia haki za Zanzibar. Aliyekuwa Waziri Kiongozi Maalim Seif yamemfika hayo hayo katika kusimamia haki za Zanzibar. Dr. Salmin alipokuja hapa alikumbwa na vikwazo katika kusimamia haki za Zanzibar. Hata Rais Aman Karume kaitwa kila majina Rais mstaafu kwa sababu ya kuleta marekebisho ya kumi ya Katiba yanayosimamia haki za Zanzibar. Sitoona ajabu kwamba Dr. Ali Mohammed Shein Rais wetu na viongozi wa Serikali hii wakatiwa midomoni na sisi kwa sababu ya kusimamia haki ya Zanzibar. Ninachowaomba viongozi hawa tusirudi nyuma tusimamie haki za Zanzibar. Wananchi wa Zanzibar wametuamini sisi hivi sasa wametulia baada ya kutoa wito mara nyingi sana kwamba watulie watuamini sisi.

Ninachosema wananchi wametuamini viongozi wao kwa sababu ya kauli tulizowapa tusije tukaiangusha imani hiyo ya wananchi Mhe. Naibu Spika. Narejea kusema kwamba katika Muungano huu sisi si watumwa wa muungano ni wabia wa muungano. Watanganyika waumiliki muungano huu ikawa sisi tunangoja fadhila yao, tuna haki sawa sawa ya kuamua nini tunachokitaka. Sasa sisi kama viongozi kuanzia Rais, Baraza la Mapinduzi, Baraza la Wawakilishi msimamo mmoja na wananchi wetu katika kusimamia kile Zanzibar wanachokitaka nacho si chengine ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar yenye mamlaka kamili kitaifa na kimataifa, halafu itakuwa na mashirikiano na Jamhuri ya Tanganyika kupitia Muungano wa mkataba.

Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na baada ya hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante ndugu Wajumbe kwa michangio yenu lakini bado tuna wachangiaji wengi, orodha ilikuwa na wachangiaji 24 wamechangia 4 bado 20. Kwa hivyo tuje mapema jioni ili tuendelee na michango hiyo.

Naakhirisha kikao hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tunapochangia twende kwenye *point* tusirejee, tutatumia dakika 20 kwa kila mchangiaji kwa sababu kuna watu 24.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria, hotuba ya bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha jioni hii ya leo na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa jioni hii ya leo. Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na kitabu chake kizuri, lakini pamoja na mazuri yaliyomo lazima na sisi tutie nyama zetu kwa sababu bila ya kutia nyongeza hotuba haitoboreka.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nizungumze kuhusiana na Ofisi ya Mufti. Tunashukuru sana ofisi hii ya Mufti kwa kutekeleza kazi zake na kuratibu

vizuri, lakini namuomba Mhe. Waziri katika ofisi hii kama ilivyo kawaida wanaratibu na kutekeleza mambo ya kidini lakini kuna mambo mawili matatu lazima wayaangalie na kuyapatia ufumbuzi kama vile migororo ya misikiti. Kunakuwa na migogoro ya miskiti mara kwa mara na ofisi yake inatakiwa iangalie ili kuipatia ufumbuzi migogoro hii ya misikini na migogoro ya kidini.

Mhe. Naibu Spika, siku nyingi kunakuwa na migogoro katika masuala ya uandamaji wa mwezi, kuna wengine wanafungua mwezi 29 wengine mwezi 30. Kwa hivyo, kuna haja ya ofisi hii ya Mufti kukaa kitako na maulamaa au wanavyuoni, ingawa wanakaa lakini kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala hili ili tusipate mwanya katika dini yetu hii.

Suala jengine tunaiomba ofisi hii kuangalia hawa walimu wa Madrasa, kila mara tunazungumza suala hili kwamba wawaangalie angalau kupatiwa sabuni. Kwa sababu kazi wanayoifanya ni kazi nzito sawasawa na walimu wanaosomesha skuli, kama wanavyopata kazi walimu wa skuli basi na walimu wa madrasa wana kazi nzito. Kwa hivyo, Serikali wangeangalia wakawaona hawa na wao wanastahiki kusaidiwa hata sabuni, japo si mishahara lakini angalau sabuni.

Jengine ni suala la kuwashajihisha Waislamu wenye uwezo kutoa zaka na kuona kwamba hizi zaka zinawafikia wale walengwa Mhe. Naibu Spika. Ni vizuri sana Waislamu kutekeleza ibada hii ya zaka lakini ikafika kwa wale waliokusudiwa. Kwa hivyo, Ofisi ya Mufti ina wajibu wa kusimamia na kuwaelimisha wakaona kwamba kuna wajibu wa kufikiwa na hii zaka. Pia misaada katika mwenzi huu mtukufu wa Ramadhan kuwaelimisha Waislamu ili kujua au kuwakumbusha kwa sababu sisi tunaambiwa tukumbushe, wanajua lakini wakumbushwe ili wapate kutekeleza katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani tunaoelekea.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kuzungumza ni kwamba pamoja na kuangalia haki za binadamu lakini kuna na haki na mila za miji. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tunakotokea huko nyuma mwezi wa Ramadhani ilikuwa si ruhusa mtu kula ovyo ikawa kila mmoja mtu anamuona katika nchi yetu ya Zanzibar, lakini sasa hivi Mheshimiwa limekuwa ni suala la kawaida tu. Mtu anakaa anakula tena pengine mtu yule ni Muislamu lakini anakula bila ya kujificha, mahoteli hayafungwi yanafunguliwa kikamilifu na ilikuwa zamani mikahawa midogo mdogo inafungwa kwa sababu ya kuutukuza mwezi wa Ramadhani lakini sasa watu wanakula ovyo, mikawaha haifungwi, hoteli hazifungwi kwa nini tufanye hivi. Mhe. Naibu Spika, lazima tuheshimu mila zetu na tuheshimu Mwezi Mtukugu wa Ramadhani. Pamoja na kuwa Serikali inasema haina dini lakini asilimia 90 ya Wazanzibari ni Waisilamu kwa hivyo lazima heshima ya Kiislamu iheshimiwe na itukuzwe.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nataka niitukuze sana hii Wakfu na Mali ya Amana kwa kazi zake nzuri inazozifanya kusimamia vizuri kazi zake, nampongeza sana huyu Sheikh Abdallah kwa kazi zake nzuri namuomba Mwenyezi Mungu amuwezeshe ili aendelee kusimamia vizuri kazi zake.

Suala jengine ni suala la vizazi na vifo. Mhe. Naibu Spika, suala hili limekuwa kikwazo sana, Mhe. Waziri alisema kwamba keshafanya marekebisho ya hivi vyeti vya kuzaliwa ili watoto wapate vyeti, lakini katika marekebisho yake bado ni vikwazo kabisa. Sasa naomba Mhe. Waziri atapokuja atueleze katika uratibu wake hasa kwa upande wa Pemba. Pamoja na kwamba amesema wameunda kikosi cha kusimamia lakini atueleze kikosi hicho kimesimamia vipi, watu wamepata vyeti kiasi gani na tatizo ni nini hasa hawa Wakuu wa Wilaya. Baada ya vyeti kuandikishwa Wakuu wa Wilaya inakuwa ni vikwazo vikubwa sana kuvisaini vyeti vile na kufika kwa walengwa na watu hupelekea kulalamika sana kuhusu vyeti vya kuzaliwa, kwa nini iwe hivi.

Mhe. Naibu Spika, cheti cha kuzaliwa sasa hivi imekuwa ni kigezo kikubwa, kwa sababu huwezi kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kama huna cheti cha kuzaliwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili suala aliangalia kwa umakini mkubwa kabisa, kwa sababu kuna wazee ambao wamekosa kuandikishwa na kutopata vitambulisho vya Mzanzibari kwa sababu ya vyeti vya kuzaliwa.

Nilizungumza hapa suala hili kwenye Ofisi ya Rais, Mzee ana miaka 70 au 80 atakipata vipi cheti cha kuzaliwa na urasimu mkubwa. Kwa sababu huko nyuma unakotoka mpaka mtu atoke Pemba aje Unguja na halafu sasa hicho chetu cha kuzaliwa ni zaidi ya shilingi 40,000 sasa mzee ana miaka 80 umtoe Pemba aje huku kutafuta cheti cha kuzaliwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili alione kama ni urasimu mkubwa na tunawapa tabu watu wetu, mtu anakuwa ni Mzanzibari halisi katika nchi yake anapata tabu kama mgeni katika nchi yake, kwa nini tuwafanyie watu hivi, tuacheni itikadi za kisiasa tuwape watu haki zao, itikadi zetu hebu tuziacheni pembeni ili kila mmoja apate haki yake. Mzanzibari mwenye haki ya kupata cheti cha kuzaliwa urasimu uondoke kama wazee wetu lazima wawe na vyetu ndio wapate vitambulisho ili wapate haki zao.

Mhe. Naibu Spika, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Mzanzibari sasa hivi sio cha kupigia kura, mtu hawezi kupata kazi kama hana kitambulisho cha Mzanzibari na kitambulisho cha Mzanzibari hukipati kama huna cheti cha kuzaliwa. Kwa hivyo, huu urasimu uondoke tuone kama ni haki Wazanzibari

wapewe vyeti vya kuzaliwa bila ya vikwazo, bila ya urasimu mkubwa ili kila mmoja apate haki yake tusiwanyime haki zao watu.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze kwenye marekebisho ya Katiba. Mhe. Naibu Spika, suala hili tushalizungumza kwa urefu sana lakini mimi nawashangaa sana Wazanzibari, Wazanzibari fursa hii tunasema mara kumi fursa hii tuliyoipata hatuipati tena kwa muda wa miaka mia, hii ni fursa tumepewa na Mwenyezi Mungu katutunuku Wazanzibari sasa fursa hii bila ya kuitumia vizuri hatutafaulu, kila saa tunapiga kelele humu tunasema jamani tuacheni itikadi za kisiasa kwa sababu Zanzibar tumefikia mahali hatujui tunachokifanya, hatuna maamuzi, hatujulikani kimataifa, hatujulikani popote.

Leo kuna watu redio zinapiga kelele huko kwamba watu wanakwenda wakiwashawishi watu kwa shilingi 10,000 jamani tunaelekea wapi, tumesema kwamba Wazanzibari waachwe huru leo wanakwenda watu kuwapa pesa na mabarua wende wakapeleke, jamani tunafanya mchezo, tunafanya masikhara, tunacheza na shilingi ndani ya choo, shilingi ikitumbukia ndani ya shimo la choo haipatikani tena. Kwa hivyo, na hii fursa tuliyopewa na Mwenyezi Mungu tunaichezea tutakuja kujuta.

Mhe. Naibu Spika, kusema kweli suala hili leo Wazanzibari badala ya kukaa tukaacha tafauti zetu sisi tumefika hadi maamuzi yote mpaka tuamuliwe, leo kuna nchi hizi mbili zimejiunga na Afrika Mashariki zilizoingia kijuu juu Burundi na Rwanda, wameingia juzi tu hivi sasa ni wanachama wa Afrika Mashariki sisi Wazanzibari hapa tulikuwa tangu nyuma ni wanachama hatujulikani. Jamani sisi hamjui tumepoteza hadhi ya nchi hii, Wazanzibari tumepoteza hadhi ya nchi yetu leo tumepewa fursa ya kutetea, ya kusema kuna watu wanafanya masihara wanakwenda wakiwababaisha Wazanzibari.

Halafu suala jengine Mhe. Naibu Spika, namwambia Mhe. Waziri yeye katuahidi na amesema kwenye kitabu hiki kwamba watasimamia na watalinda haki za Wazanzibari kutokana na maamuzi watakayotoa kwenye maamuzi yao ya Tume. Sasa hivi hiyo Tume inaanza kuboronga, kwa sababu kuna baadhi ya majimbo hivi sasa kwenye ratiba zao wameweka siku moja tu, haya siku moja jimbo hilo watatoa maoni vipi, kwa nini waweke siku moja sehemu nyengine wakae siku nne, tano, kumi mwengine waweke siku moja, hivyo kweli siku moja Wazanzibari wenye jimbo lile zima wataweza kutoa maoni yao? Sasa nakuomba Mhe. Waziri hili nalo ulisimamia kama wanataka kukusanya maoni sio siku moja tume zilizopita zote hazipiti kwa siku moja kwa nini majimbo mengine wakae siku moja na mengine wakae siku nyingi kwa nini wasiweke usawa. Mhe. Waziri tunataka na hili ulisimamie ili Wazanzibari wapate haki ya kutoa maoni katika tume hii, fursa pekee ni kutoa

maoni hakuna njia nyengine ya mkato haya siku moja watatoa maoni watu wangapi kwa jimbo lile.

Mhe. Waziri hili tunataka utusimamie leo hii Mwenyezi Mungu akikupa uwezo uanze kupeleka ripoti kwamba haiwezekani kwenye majimbo mengine wakae siku tatu au nne na majimbo mengine wakae siku moja.

Halafu suala jengine Mhe. Naibu Spika, tunataka hizi ratiba za majimbo tupewe tuweze kuzielewa tuwaambie watu wetu mapema ili na wao wapate kutoa maoni yao. Lakini ratiba zisiwe hivi kwa sababu wengine hawasilikilizi redio kwa kutangazia kwenye redio tu haiwi, lakini tuwaambie mapema. Vile vile na hawa viongozi wengine wanaokwenda wakisimamia kuna viongozi wanakwenda wakifanya vurugu kwa nini wasiiache tume ikafanya kazi yake, hawa viongozi wanaojipeleka wanakwenda kusimamia nini. Mhe. Naibu Spika, hii ni haki ya Wazanzibari waachiwe waseme wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawaambia Wazanzibari, nawaambia ndugu zangu mimi ninayepiga kelele hapa sipigi kelele kwa sababu nataka urais sisi tunawapigia kelele viongozi wetu wa Zanzibari na maslahi ya nchi yetu na watoto wetu wajao, jamani sisi hapa ni mas-uli tumepewa fursa hii na Mwenyezi Mungu tutakwenda kuulizwa kutokana na fursa hii tuliyopewa msifanye masihara. Halafu mimi naona vingozi wetu wa Serikali sijui niseme wana kigugumizi au wana woga jamani woga ni adui wa haki, sisi kutetea nchi yetu na maslahi ya nchi yetu si dhambi kwa nini tunafanya hivyo.

Alisema hapa Mhe. Ismail Jussa na mimi usemi huu niliusema ulipopita na leo nasema tena, ukiowa mke ndugu ukimuonea huruma hamzai, wewe ukiwa utaona haya hamzai na mke ndugu. Jamani sisi hapa wenzetu tumeungana na wenzetu lakini kuna mambo ambayo ni ya Muungano hebu na tuambiwe hiyo faida kwa sababu usiangalie faida mbili tu tuangalie na hasara, lazima uangalie faida na hasara, lakini nyinyi mnaangalia faida tu mnasema kwenye Muungano tunapata faida hii na hii hasara je, hasara yetu ni kwamba sisi tumepoteza utaifa wetu Wazanzibari hatujulikani popote, Wazanzibari tukiondoka hapa tukifika Chumbe ndio mwisho wetu.

Nawaomba jamani wazee wangu, ndugu zangu sisi ni mas-uul tutakwenda kuulizwa na Mwenyezi Mungujinsi tulivyowasaidia Wazanzibari, kwa hivyo tuunganeni tuwe kitu kimoja, tutoe maoni kwa maslahi ya Wazanzibari tusitoe maoni kwa maslahi yake mtu binafsi, tutoe kwa maslahi ya taifa tuelekeze mbele maslahi ya taifa Wazanzibari nchi yenu ni Zanzibar ikiondoka Zanzibar hamna nchi nyengine, mtu atakapokwenda kujigamba popote pale, majigambo yake yote ni hii Zanzibar. Kwa hivyo, wazee wangu, ndugu zangu

Wazanzibari tusimameni kitu kimoja tusifanye masihara kila mtu akienda akasema lake kwa maslahi yake binafsi tuseme kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono yote hayo.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa jioni hii ya leo na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya bajeit hii ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kuwashukuru wizara husika ikiongozwa na waziri wake lakini pia na watendaji wote kwa ujumla. Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika dhana za maelekezo ambayo tulikuwa tukipata kwa Mhe. Rais wetu mstaafu Dr. Salmin Amour Juma alipokuwa akizungumzia suala zima linalohusiana na sheria.

Dr. Salmin katika wakati wa uongozi wake mara nyingi sana alikuwa akihimiza sheria, sheria, sheria; maelekezo yale ya Dr. Salmin tulidhihirika ufanisi na utekelezaji wake katika utawala wa Dr. Amani Abeid Amani Karume pale alipounda Wizara inayohusiana na masuala ya Katiba, Sheria na Utawala Bora. Lengo na madhumuni ya kufanya kazi hii ilikuwa anatimiza yale malengo ya sheria pamoja na utekelezaji wake. Lakini kwa bahati nzuri zaidi wakati ule wa Dr. Amani Karume kuanzishwa kwa wizara ile aliyekuwa msimamizi mkuu alikuwa kwa sasa ndiye Rais wetu wa Zanzibari, Dr. Ali Mohamed Shein na alipofika yeye kuchukua madaraka ya kuongoza nchi kwa vile alikuwa akiielewa Wizara hii akafikia pahala akaamua sasa kuipunguzia baadhi ya mzigo wizara ile na kuifanya kwamba iwe Wizara ya Katiba na Sheria na Utawala ukapelekwa katika maeneo ya utumishi kule. Ni jambo zuri na jambo la msingi na inaonekana ana muono wa kimaendeleo zaidi na katika utendaji wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari kwa sasa hususan wananchi wanakwenda na wamefika pahala wamepoteza matumaini, wamepoteza matumaini kutokana na kwamba wanaona haki zao baadhi ya nyakati na baadhi ya maeneo wanakosa kuzipata kwa mujihu wa utaratibu ambao wanahisi wao wenyewe unafaa.

Mhe. Naibu Spika, kimbilio la wananchi wetu katika masuala ya kutafuta haki zao ni katika Mahakama zetu Mhe. Naibu Spika, kinachostaajabisha, kinachoshtusha pamoja na kushangaza ni kuona kwamba wananchi hawa sasa wanapoteza imani katika Mahakama kutokana na rushwa kutawala sana katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chetu hiki cha bajeti ambacho kimekuja kusomwa hapa mimi nianze na ukurasa wa 56 kifungu cha 127. Tumeona hapa Mhe. Waziri alipokuja kutuelezea kwamba wizara itaendelea kupambana na tatizo la ucheleweshaji wa kesi katika Mahakama zetu na kuhakikisha matatizo ya wananchi katika usimamizi na ufuatiliaji wa haki zao yanapungua kwa kiasi kikubwa. Hadi sasa hivi Mhe. Naibu Spika, kuna watu wengi, wana matatizo mengi na kesi zao sasa hivi zinapigwa *date* tu miezi, wiki mpaka mwaka bila ya kupata ufumbuzi wa uhakika kutokana na kesi zao ambazo zinaendelea katika Mahakama hizi, ukiachilia Mahakama za kushughulikia kesi za kawaida lakini hata Mahakama za Ardhi vile vile. Kuna kesi nyingi ambazo hazina ufafanuzi wala uamuzi mpaka dakika hii.

Lakini kama hapo haitoshi Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya kesi ambazo zinatolewa maamuzi na zinashindwa kutekelezwa. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa hebu atusaidie na atuongoze zaidi kwa hizi kesi ambazo zinakuwa zimefikiwa maamuzi na ikawa utekelezaji wake bado unasuasua wananchi wafanye nini, waende wapi, wajibu wao ni nini katika masuala kama haya. Mhe. Waziri utapokuja hapa tutaomba utusaidie katika eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka kwenda ni kifungu cha 104 maeneo ya Wakfu na Mali ya Amana. Eneo hili ni eneo ambalo linagusa maisha ya watu moja kwa moja kabisa, katika kipengele hiki cha Wakfu na Mali ya Amana hapa tunapata safari za Hija ambazo ni mwaka jana tu palitokea matatizo hadi kuna baadhi ya watu wakakosa zile safari za kwenda Hija kutokana na zile taasisi walizokuwa wakizitumia hazina uhakika katika kupanga safari za watu kuweza kwenda safari nzito kama hii.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nimeona katika kitabu chake hiki ambacho ametuletea leo hapa kwamba kuna utaratibu maalum ambao umepangwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaratibu suala hili kwa umakini zaidi na kuhakikisha kuwa safari zile na walengwa ambao wanakwenda, wanakwenda katika misingi ambayo ni ya kitaaluma na misingi ambayo itakuwa inaeleweka zaidi.

Maelekezo na maombi yangu kwa Mhe. Waziri ni kwamba safari hii ni nzito sana kwa hivyo ahakikishe haya makundi yanayoshughulikia masuala ya hawa watu wanaokwenda Makka wayahakiki na wayape masharti maalum na watakapoona kwamba masharti yale hayatimizwi basi kuweko na adhabu maalum ziweze kuchukuliwa juu ya taasisi hizi ambazo zinashughulika na watu hawa kuwasifirisha ikiwa ni pamoja na kuwapangia safari leo, kesho, keshokutwa na mtondogoo. Utaratibu huu tunamuomba Mhe. Waziri ausimamie vizuri ili hawa watu wanaokwenda kuhiji wasipate usumbufu ambao unaendelea kuwepo siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumzia ambapo katika kitabu chetu hiki tumeona kwamba kumezungumziwa kwa kina ni suala la Zaka na Sadaka. Pamoja na kwamba wizara inapanga mikakati mizuri ya kuweza kupanga namna gani ya kuweza kuwafikia wale walengwa kuwapa hizi sadaka na zaka, lakini kwa kipindi hiki hata jana tulipokuwa kule shamba Marumbi tulishuhudia baadhi ya watu wakiwa wanatoka wanakwenda kule katika utaratibu ambao hata haueleweki kwenda kutoa hizi sadaka katika maeneo ambayo wananchi hali zao ziko duni.

Kusema kweli utaratibu unaotumika haupendezi kwa kifupi, ni vizuri wale watu wanapokuwa wanakwenda katika taasisi zile wafuate taratibu hizo ambazo Mhe. Waziri anataka kuja kuzitayarisha na kuzileta kwa watu na masuala haya yafanywe kwa haraka inavyowezekanaili hizi sadaka zinazokuja zije katika taratibu zinazostahiki.

Mhe. Naibu Spika, katika Kitengo hiki cha Wakfu na Mali ya Amana tuna tatizo kubwa ambao linatukabili katika misikiti yetu. Misikiti mingi sasa hivi imekuwa ina migogoro ya watu kugombana, kuzozana na watu kugombania uimamu katika misikiti. Namuomba Mhe. Waziri atapokuja hapa tutengenezewe utaratibu utakaofaa, utaokuwa mzuri, wa uhakika kuondoa migogoro katika misikiti yetu ambayo tunaendelea nayo kusali siku hadi siku katika maeneo yetu.

Jengine ambalo nataka kulizungumzia ni utaratibu wa upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri atapokuja hapa Mhe. Naibu Spika, atufahamishe ni utaratibu gani unaopaswa na unaostahiki kutumika ndani ya taasisi yake namna ya kuweza kuvipata vile vyeti vya vifo au vya uzawa katika Manispaa yetu ya Zanzibar na maeneo yote kwa ujumla wake.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la muundo wa Mahakama. Mhe. Naibu Spika, Tanzania tuna muundo wa Mahakama ambao umejengeka katika utaratibu ufuatao. Tuna Mahakama Kuu ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Tanzania, lakini tuna na Mahakama ya Rufaa. Mahakama ya Tanzania inaongozwa na Jaji Kiongozi, Mahakama ya Zanzibar inaongozwa na Jaji Mkuu, lakini Mahakama ya Rufaa inaongozwa na Jaji Mkuu kabisa tuseme kwamba jina lake anaitwa Mhe. Mwinyichande, lakini sijui katika masuala ya kimahakama tunamwita vipi zaidi, lakini huo ndio utaratibu ambao upo. Katika Mahakama ya Rufaa ambayo ndio kiunganishi baina ya Zanzibar na upande wa pili wa Muungano ni kwamba Mahakama ile ina wafanyakazi 16 katika wafanyakazi hao ambao wako katika Mahakama hii ni mfanyakazi mmoja tu ambaye ametokea upande wa Zanzibar.

Sasa katika hili Mhe. Naibu Spika, ninataka kusema hapa ni kwamba kutokana na uwakilishi mdogo uliokuwemo ndani ya Mahakama ya Rufaa, sasa mimi ninashindwa kufahamu jee hatuna watu wenye sifa kama zile kuweza kwenda kufanyakazi pale, au tuna matatizo gani yanayopelekea hata ikabidi hata katika Mahakama ya Rufaa Majaji 16 tuna Jaji mmoja tu ndani ya mahakama ile. Matokeo yake sasa inapelekea kwa sababu Jaji tuliyenaye ni mmoja tu, tunakosa kupata uwakilishi katika Mahakama ya Afrika ya Mashariki.

Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa Mhe. Naibu Spika, nitamuomba aje atuelezee ni sababu zipi zinazopelekea hata ikawa Zanzibar haina uwakilishi mzuri katika Mahakama ya Rufaa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni suala la buku letu hili kubwa. Katika buku kubwa hili ukurasa wa 51 nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe ufafanuzi juu ya ongezeko kubwa la fedha ambalo lipo katika ukurasa wa 51 *bullet* 142237.

Jengine ukenda kwenye ukurasa wa 550 katika kitengo cha 211108 vile vile ningependa kupata ufafanuzi juu ya ongezeko kubwa la fedha vile vile. Lakini pia *bullet* 211110 katika ukurasa huo huo wa 530. Tukiendelea mbele ukurasa huo huo wa 530 kuna *bullet* 220101 naomba kupata maelezo vile vile.

Na ukurasa wa 537 *bullet* 211108 naomba kupata maelezo vile vile na ukurasa wa 538.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa anasema unakwenda *speed* hapati kurekodi, hebu rudia.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Tunaanza wapi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Ukurasa wa 530

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ukurasa wa 330 bullet 211108. Ukurasa huo huo 330 tena 211110. Tunaendelea 220101 tumemaliza ukurasa huo.

Ukurasa wa pili ni 537 *bullet* 211108. Ukurasa wa 538 ni *bullet* 220509. Ukurasa wa 539 211110. Ukurasa tena wa 539 *bullet* 22020201. Ukurasa nambari 540 *bullet* 220407. Ukurasa wa 544 *bullet* 220506.

Sasa namalizia kwa suala zima la Katiba. Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Una dakika 2.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tuna tume hapa ambayo imetoka Tanzania kwa ajili ya kukusanya maoni ya Katiba. Lakini Mhe. Naibu Spika, sisi kama viongozi tukiwemo humu kama wawakilishi na wenzetu kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuna haki na wajibu wa kuwafahamisha wananchi wetu kitu gani wanachotakiwa kuchangia katika Katiba hii.

Sote tumekuwa tunaimba tu nyimbo ya Katiba. Kuna maoni ya Katiba huko yanatakiwa yaende yakatolewe, lakini mwananchi wa kawaida hajui kitu gani ambacho anataka kwenda kuchangia katika Katiba ile.

Sasa ningeliomba kupitia nafasi hii na fursa hii ambayo tumeipata hao wananchi wetu hao, tuwafahamishe kwamba kwa upande wa Zanzibar wanatakiwa waende wakasome sura ya nne ya Katiba yetu, kuanzia ibara ya 102 na kuendelea chini ili waweze kujua mambo ambayo yanayoihusu Zanzibar ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa mimi ninafikiria Mhe. Waziri atakapokuja hapa tunamuomba achukue fursa hii, awaelekeze wananchi pamoja na Wajumbe humu ndani ni namna gani wanapaswa kuifanya kazi hii ya kikatiba, ili wananchi wawe na uelewa juu ya mchango ambao watakuwa wanautoa katika suala zima, zito, ambalo ni nafasi ya pekee kwa Wazanzibari kuweza kuondokana na matatizo na kadhia tuliyonayo katika mambo yanayotusumbua siku hadi siku.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni nitaunga mkono hoja baada ya kwisha kupata maelekezo ya kina kwa mambo ambayo ninataka ufafanuzi wake.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza kuzungumzia katika Afisi ya Mrajis ya Vizazi na Vifo. Mhe. Naibu Spika, kwanza afisi hii ninayoizungumza ni afisi mpya. Afisi hii imetenganishwa na ile afisi ya zamani iliyokuwa ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Kwa hivyo hivi sasa tuna afisi mpya ambayo inafanya kazi peke yake. Dhamira ya afisi hii ni kuongeza ufanisi katika kazi zao na kupunguza kero za wananchi. Hiyo ni moja katika dhamira kubwa katika Afisi ya Vizazi na Vifo na wananchi kuweza kupata huduma za uhakika.

Lakini matarajio yake au yaliyopatikana ni kwamba hiyo haki haipatikani kikamilifu katika hii afisi mpya ya vizazi na vifo. Hali halisi iliyojitokeza ni kwamba usumbufu ndio unaonekana. Kwa hivyo sivyo watu walivyotegemea na sisi sivyo tulivyotarajia kwamba hali itakuwa ni nzuri, isipokuwa dhiki ndio inayoendelea zaidi.

Tuangalie huduma ambazo zinazotolewa vijijini kwa kuleta ufanisi. Suala hili ni gumu sana kwa vijiji vyote takriban ni usumbufu mkubwa, mwananchi anapotaka kupeleka shughuli zake kwa anayehusika, baada ya kutoa ada na kupeleka shughuli zake Wilayani, zinachukua muda mrefu, pengine itafika miezi mitatu ambayo inatakiwa cheti kile kipelekwe hakijafika bado. Kwa hivyo huo ni usumbufu vile vile.

Tuseme kwa ufupi kuwa huduma hizi zinatolewa na Afisi za Mkoa pamoja na Wilaya. Usumbufu huu bado unaendelea kwa wananchi juu ya suala zima la upatikanaji wa vyeti. Vyeti vya kuzaliwa inakuwa ni usumbufu, na vyeti vya vizazi na vifo vinakuwa ni usumbufu vile vile.

Lakini tuseme kwa ufupi kwamba, kwa sababu afisi hii haina udhibiti wa watendaji, wale watendaji ambao watakiwa wafanye shughuli hizi wanashindwa hawa kufanya kazi zao vizuri. Kwa hivyo hiyo wizara yenyewe au idara yenyewe inashindwa kuwadhibiti watu hawa katika shughuli zao.

Haya mambo haya katika mikoa na wilaya. Sasa idara hii imeshindwa kabisa kuweza kuwadhibiti watendaji ndio maana inapatikana usumbufu wa aina hii. Kwa hivyo mara nyingi watu hawa ambao wanaofanya kazi katika afisi za wilaya na mikoa wanapewa shughuli nyengine ambazo sio walizotengewa na idara, wanafanya kazi za ziada. Kwa hivyo kuwachelewesha watu katika kupata huduma zao.

Ushauri wangu hivi sasa ninasema kwamba kama wizara inataka ifanikiwe katika shughuli hizi basi iajiri wafanyakazi wa kudumu katika wilaya na mikoa, hapa shughuli zitakwenda barabara. Lakini kama wataachiwa watu wale wale ambao wanaendeleza shughuli hizi kutoa huduma kwa wananchi, hizo huduma kwa wananchi hazitopatikana, kwa sababu idara haina udhibiti wa watu hawa, watu hawa wanadhibitiwa na mikoa na wilaya. Kwa hivyo hilo nitamuachia Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutueleza vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi nizungumzie masuala mengine ya maandalizi ya Katiba mpya. Mhe. Naibu Spika, siku zote hapa tunazungumza ndani ya Baraza letu tukufu kwamba ni jambo la msingi na muhimu, siku zote tunapiga kelele kwamba suala la elimu kwa wananchi ni suala muhimu sana, siku zote tunasema maneno haya. Lakini baada ya kuzungumza hapa sivyo inavyotendwa huko nje.

Angalia kwamba siku zote nchi inapokabiliwa na jambo la kitaifa, kama hili la mchakato mzima wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunategemea kwamba wizara au serikali au kwa taifa kwa jumla iweze kulishughulikia kwa wananchi wake. Hao wananchi ni watu ambao hawafahamu Katiba ya Muungano, Katiba ya Zanzibar na wala hawajui nini kinachotakiwa, wanasikia watu wanakuwa wa tume wakaeleze nini. Kwa nini tufanye kitu kama hiki kisichoeleweka.

Ninakumbuka tulipokuwa tukitaka kufanya GNU hapa hapa tulifanya kamati ya watu sita, na tukakubaliana sote kwa pamoja hapa, twende hivi. Lakini hivi sasa inaonekana suala hili ukilizungumza hapa katika Baraza na kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri, anasema hilo si letu sisi serikali wala halihusiani na wizara yangu. Lakini hawa wananchi ni suala la kitaifa na ni suala kubwa.

Kwa hivyo tunakuwa tunawababaisha wananchi na hawajui vya kufanya. Tume inakuja kila mtu anazungumza anavyopenda yeye, matakwa ya kitaifa hayawezi kupatikana ikiwa kila mmoja anazungumza analolitaka yeye, hatupo kitu kimoja. Kwa hivyo tunasema hao wananchi angalau wajue jinsi gani ya kuikabili hii tume, na kuwa tayari kutoa mchango wao katika suala zima la Katiba mpya.

Mhe. Naibu Spika, kuwaelimisha wananchi kitaifa ni haki ya wananchi. Hili hili taifa ni haki yake kuwaelimisha wananchi hawa. Pia ni jambo la msingi kwani wananchi hukhitalifiana kifikra, kimawazo na hata katika kuchanganua mambo. Sasa ikiwa watu hawa katika haya niliyoyazungumza angalau hawakuelimishwa hili suala ni gumu, na nina wasi wasi kwamba, hatujui kwamba wananchi watakwenda kuzungumza kitu gani. Kila mtu atazungumza lake na matokeo itakuwa hasara kwa taifa hili.

Kwa hivyo, elimu ni kitu muhimu na elimu bado haikutolewa, wanakuja watu wameshaingia katika nchi, tume imefika lakini wananchi hawajui wanafanya nini. Mimi ninazunguka mote munazungumza nini, wanasema sisi hatujui chochote cha kwenda kuzungumza. Kila mtu ana wasi wasi. Kwa hivyo elimu hii haikutolewa kabla na tume imeshaingia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi ninataka nizungumzie suala la pili ambalo ni la Muungano. Mimi ninataka nitoe hapa tahadhari ya mambo. Muungano hivi sasa una umri wa miaka 48. Zanzibar imeendelea kumeguliwa sehemu ya madaraka yake na kuingizwa ndani ya Muungano. Hilo tukitaka tusitake hiyo ndio hali halisi ilivyokuwa.

Haya yamefanyika bila ya kuzingatia misingi ya ulimwengu, hiyo ni hali halisi. Kwa hivyo misingi hiyo ni katika kuheshimu utu na haki za watu walioungana. Pia misingi hiyo iheshimu mawazo ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, imechukuliwa Katiba ya Tanganyika na kufanywa Katiba ya Muungano. Kwa hatua hiyo ndiyo iliyoifanya Zanzibar kupokonywa uwezo wake, madaraka yake. Zanzibar haina mamlaka, haina madaraka.

Kama nchi imepokonywa madaraka yake, uwezo wake na mamlaka yake, ina maana nchi hii Zanzibar haina *sovereignity*. Kwa hivyo kama haina *sovereignity* ina maana nchi hii haina uwezo wa kufanya jambo lolote. Mimi niulize tu kwamba nchi tunayo au hatuna. Jibu nchi tunayo, watu tunao hatuna, jibu watu tunao, jee serikali tunayo, ndio serikali tunayo, basi iangalie ni aina gani ya serikali tuliyonayo, iangalie kwenye uwezo wake na madaraka yake na mamlaka yake kwenye nchi hii. Jee ina uwezo wa kufanya kitu. Kwa hivyo ninaweza nikasema ni serikali butu, haina uwezo wa kufanya kitu chochote.

Kwa hali hii inavyoendelea tukitizama kwa haki za binadamu au za kimataifa, tunasema kwamba ilivyokuwa imepokonywa *sovereignity* yake, hivyo *International treaty* imevunjwa, yaani mkataba wenyewe umevunjwa. Zanzibar imekuwa *unpower* na imekuwa *un active partner* ni watu tu kama watu walioungana, kwa sababu tumepokonywa *sovereignity* yetu.

Kwa namna hiyo katika Muungano huu na inasema hakuna kifungu chochote chenye uwezo wa kupunguza au kuongeza yale mambo ambayo Mheshimiwa aliyetangulia mbele ya haki, mambo 11 aliyoyaweka yale hakuna mtu katika suala lile ambaye anaweza kupunguza au kuongeza. Angalia leo hali ilivyo. Ni mambo mangapi ya muungano hivi sasa kutoka 11 na tupo mambo mangapi. Hii ina maana kwa sababu hatuna *sovereignity*, hatuna kitu chochote na ndio maana yakafanywa hivi sasa zaidi ya mambo ishirini na mbili naa. Hayo ni kwa sababu ya hivyo.

Kwa hivyo utaona bado muungano. Kwa nini tuseme kutoka 11 yakawa ni 21, ni kwamba Waziri yeyote anaweza kutoa mswada wa sheria akaupeleka Bungeni, halafu ikapigwa kura, ndani ya Bunge ikipigwa kura *two third majority*, ni *two third majority* ya watu wote, sio CCM na CUF wakae

upande. Hapo ndio ilipokuwa *two third majority* ilivyo. Isipokuwa leo ndio tumekubaliana mambo ya Zanzibar yatakuwa ya Zanzibar na mambo ya Bara yatakuwa ni ya Bara.

Lakini hapo awali ndio tumeshanyang'anywa madaraka yetu. Sasa mimi ninasema katika suala hili kama wananchi hatukuwaeleza vizuri hali halisi ya suala hili, kwenye Zanzibar tunataka serikali yetu ya Zanzibar, serikali ambayo itakuwa na mamlaka kamili, serikali itakuwa na maamuzi kamili, serikali itakuwa na uwezo kamili wa kufanya mambo yake ya ndani.

Kwa sababu hivi sasa niliposema ni serikali butu ni pale serikali ambayo haina mamlaka hayo. Kwa hivyo ikiwa haina *sovereignity* haya yote hayawezi kufanyika. Serikali tunayo, watu tunao lakini hali ni mbaya. Kwa hivyo tunataka mambo yetu. Serikali yenye mamlaka kamili na inayoweza kutoa maamuzi ya ndani. Kama tukisema kwa mfano tunataka bendera yetu wenyewe, wimbo wa taifa wenyewe, kila kitu wenyewe na Rais awe na maamuzi. Lakini hivi sasa atakuwa hana maamuzi.

Tunasema Zanzibar tunataka iwe na uwezo wa kuweza kuwa na mambo yake ya nje. Sisi Zanzibar hatujawa nayo. Sasa ikiwa watu hawa tunawapeleka kwenye tume wakazungumze wanakwenda kuzungumza kitu gani, maoni haya yatakuwa ni ya kiasi gani. Uwezo wa wananchi wetu tunajua wa kujieleza ni mdogo sana, kwa sababu watu wengi hawajui kinachoendelea katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar. Kwa hivyo hili ni suala muhimu ninalosema ijapokuwa sasa wizara imejitoa na kusema wao sio kazi yao, serikali imejitoa haya si kazi yao.

Lakini tunasema hili suala ni muhimu. Wananchi wanahitaji kupewa elimu juu ya suala hili, watu wamefika matokeo yake ndio yale. Sisi viongozi ndio tunaanza kuchafua mazingira ya tume hii. Tunapeleka vikaratasi vichochoroni, kwa nini tufanye hivyo. Kama kweli tupo kitu kimoja hatuwi kitu kimoja, tunapeleka vikaratasi vya nini na mna chochote, faida yake nini, unafanya nini, unajenga unabomoa.

Kwa hivyo mimi ninasema hii hali sio nzuri, ni lazima tukae tutafakari tuone hali halisi. Matoke yake utayaona yatakavyokwenda, kila mtu atazungumza vyake kama hatukuwa na msimamo mmoja. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi ningelimuomba Mhe. Waziri pamoja na kauli yake aliyoiandika katika Katiba kwamba yeye hahusiki na masuala haya, serikali haihusiki basi sijui wananchi hawa ni wa nani, ikiwa serikali haihusiki.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo ninataka nizungumzie kitu chengine cha tatu ambacho.

Mhe. Naibu Spika: Cha mwisho hicho.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ndio kitakuwa cha mwisho.

Mhe. Naibu Spika, ninakuja katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Katika tume hii moja ya majukumu yake, ni kuzifanya sheria za Zanzibar kuzifanyia marekebisho. Vile vile kutoa mapendekezo.

Lakini tunaona kwamba katika tume hii inaendelea vizuri na inajitahidi katika kutoa mapendekezo na kuboresha, lakini bado tunawaambia kuna sheria nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho katika tume hii. Kwa hivyo ninaomba tume hii iendelee na kazi yake ya kurekebisha sheria.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ningekuomba nimalizie ambalo litakuwa ni la mwisho ni suala zima la mikataba ya kimataifa. Hili suala Mhe. Naibu Spika, unipe nafasi niweze kulizungumza japo kwa kidogo.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 1989 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha kwa kauli moja mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto ambayo unaitwa *United Nations Convetion on the rights of the Child*, ni haki hizo. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhika na kupokea mikataba hii ya mwaka huo, iliridhia katika mwaka 1991.

Halafu katika mwaka 1990 kabla ya hapo Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika ulipitisha mkataba wa Afrika, kwa kuteua haki na maslahi ya mtoto. Sasa Mhe. Naibu Spika, haya ni mambo mawili, ni mikataba miwili ambayo yote inazungumzia juu ya haki za mtoto. Mikataba hii inasema kwamba inazitaka nchi wanachama zilizoridhia, maana yake sisi Tanzania tumeridhia, kwa hivyo hiyo mikataba miwili iliyoteuliwa na sisi tupo katika umoja huo, kwa hivyo ilitakiwa nchi ya Tanzania iridhirie kwenye mkataba huu.

Mkataba uliridhiwa na wanatakiwa wahakikishe kwamba zinaweka mikataba madhubuti ya kisera, kisheria au kimipango, ili kuhakikisha vipengele katika mikataba hiyo imetekelezwa na nchi wanachama.

Mimi ninachotaka kutanabahisha Baraza tuelewe kwamba, iwapo Tanzania itaridhia kwenye mikataba hii na haikuweka masharti yoyote, maana yake hapa kitu muhimu ni masharti, ikiwa hii Tanzania haikuweka masharti ya aina yoyote juu ya vipengele ambavyo vilivyotolewa katika mkataba huo, hii ni hatari vipengele hivi ambapo wanataka wao vipengele hivi vitumike, vipi vitumike na vipi visitumike.

Lakini kwa kuwa mkataba umeshakubalika na umeshatolewa, ina maana sisi tuna *accept without any adequate ground* ninaweza kusema hivyo. Tume-*accept* mambo *without any adequate ground*, bila ya sababu zozote za msingi tunakubali tu, *blind* kwamba sisi katika nchi hii kwenye ulimwengu kila nchi ina mambo yake.

Zanzibar ina mila zake, ina desturi zake. Tanzania Bara ni nchi ambayo ina mamlaka yake, ina *culture*, ina vipaumbele na haki za namna kwa namna, na hatuwezi kuchukua nchi ya Tanzania Bara tukasema sawa sawa na Zanzibar. Sisi Zanzibar tupo tofauti na wao kila mmoja na *culture* yake.

Sasa ikiwa hii mikataba inaingia Tanzania na ina-*accept without any adequate ground*, bila ya kujua kile unachokifanya, kwamba macho hawana. Matokeo yake sisi tunapata mambo ya ajabu ajabu, kwamba tunapata vipengele vya sheria ambavyo katika nchi yetu haviwezi vikatumika.

Sasa ninasema masharti yalikuwa lazima yawemo hakukuwa na *reservation*, kuifanya Tanzania Bara na Zanzibar kwenye hivi vipengele. Kwa hivyo sisi tumepokea, masharti hatukuweka.

Kwa hivyo Zanzibar ina maadili yake, mila zake, desturi, ina maslahi yake kwa watoto wake, itakuwaje sisi tufuate tu mambo kama haya. Sasa mimi ninavyomuomba Mhe. Waziri kwenye suala hili awe *very careful* wakati tunaleta suala lile kwenye Baraza la Wawakilishi tuje tulizungumze ambalo tunazungumza kitu *blind*.

Mimi ningemuomba mikataba yote ambayo inayotoka nje Mhe. Waziri kabla ya mikataba ile haijaweza kufanya kazi ndani ya Zanzibar kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mhe Naibu Spika: Malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Namalizia. Madukhuli hapa. Wazee wanataka madukhuli hao, inshaalla madukhuli mutapata si muda mrefu. *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, niendelea kuwapa watu wengine na mimi ninashukuru.(*Makofi*).

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuzungumza machache kuhusiana na Wizara hii ya Katiba na Sheria. Ninamshukuru Allah kwa kutupa uzima uhai na *taufiq* ya kuzungumza humu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa ujumla kwa kuandaa kitabu chenye kueleweka na uwasilishaji mzuri wa Mhe. Waziri. Pili, katika nchi iko mihimili ya uchumi, uendeshaji na kihuduma. Lakini huu muhimili wa Katiba na Sheria umeipita yote, kwa sabahu muhimili huu wa Katiba na Sheria ni wa nchi ambao unaongoza mambo yote matatu tuliyosema. Kwa hivyo, mimi nafikiria kwamba moja katika wizara muhimu sana ambayo inatoa muelekeo wa nchi na inakokwenda ni wizara hii, kwa sababu ndani yake munapatikana katiba inayoongoza nchi, sheria inayoelekeza watu waende vipi, serikali iende vipi na mambo kadhaa.

Kwa hivyo, mimi nafikiria kwamba ingefaa katika mgawanyo wa bajeti ingefikiriwa sana na ikaongezewa bajeti yake, kwa sababu ya kazi nzito waliyonayo. Hilo la mwanzo.

La pili Mhe. Naibu Spika, tuje katika mambo yanayofuata. Kwanza mahakama ambayo maamuzi yake tunaambiwa yako kwenye *decision* ya hakimu mwenyewe, katika vifungu au vile ngazi tofauti ikiwa ni mahakma ya mwanzo, ya wilaya, ya mkoa au Mahakama Kuu. Lakini mimi nauliza kwamba kwa sababu wao wenyewe wataalamu wanatuambia kwamba *justice delayed,* yaani hukumu iliyocheleweshwa au haki iliyocheleweshwa ni haki iliyokataliwa. Je, katika uendeshaji wa mahakama ndani ya nchi yetu na katika umoja huu wa Jumuia za Madola kama zinavyoendeshwa, hakuna utaratibu ambao ungepaswa kutumiwa kuziharakisha kesi au kuona kwamba kesi zinapatiwa maamuzi katika kipindi fulani na ikiwa hazikupatiwa maamuzi maana yake kuna kosa. Hili ni swali nauliza, kwa sababu mambo ya mahakama yana vipengele vyake.

Je, huyu anayeitwa Jaji Mkuu wa nchi anao uwezo wa kufuatilia malalamiko ya ucheleweshwaji wa kesi na kuweza yeye mwenyewe ni jinsi gani anavyoweza kuziingilia na kuweza kuhukumiwa upesi. Hili ni swali ambalo naliuliza. Kwa sababu mara nyingi unapouliza kama kesi zinachelewa, majibu ya moja kwa moja unaambiwa yako katika *decision* ya hakimu mwenyewe. Lakini huyo hakimu kawekewa na mkuu wake, ambaye hapa anakuwa *proclaimed* kwamba ni Jaji Mkuu wa Zanzibar. Nauliza mamlaka yake na utendaji wake kazi usingeweza kusaidia kwamba kuharakisha kesi zisikae muda mrefu. Halafu kama alivyotangulia kusema, suala moja sitaki nirudie sana kwamba kuna utaratibu huu wa kupeleka Majaji Pemba, lakini kumekosekana nini hata Jaji Mkaazi hata ikawa bado hajapatikana kule, hakuna hawa wataalamu au vipi. Nasikia huko nyuma kidogo ilikuwa nyumba za Pemba nyingi hazina *grade* ya kuishi Jaji Mkaazi, lakini nafikiria sasa hivi watu wamejitahidi sana kujenga na nyumba zipo.

Kwa hivyo, namuuliza Mhe. Waziri ni kitu gani kilichozuia kwamba kuharakisha ule uendeshaji wa kesi kupelekwa Jaji Mkaazi Pemba, ili wale wenye haki wakaweza kupata haki zao na wale ambao hawana wakajijua na mapema. Kesi zikienda sana zinawagharimu wote na yule ambaye ana haki yake ndio anazidi kupata ile dhuluma kwa sababu yule aliyekuwa anakwenda naye kesi kama anajua kwamba hii sio haki yake na anataka kusuluhisha na mapema, basi angesuluhisha.

Jambo la pili nije kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria. Nashukuru sana na naipongeza Wizara kwa kukiunda hiki kitengo yaani Tume ya Kurekebisha Sheria. Lakini Mhe. Naibu Spika, utaratibu wao kama ulivyoelezwa humu, kwa fikra yangu naona bado zipo kasoro kidogo. Sheria zimetungwa kwa ajili ya wananchi kutozivunja zile sheria na kuona kwamba utaratibu ni huu. Siku hizi wanaitwa wadau. Mimi nauliza katika utaratibu wa Tume hii ya kurekebisha sheria, kuna utaratibu gani wa kukutana na wadau.

Kwa mfano, Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko mengi yanatokana na wadau katika sekta tofauti, inawezekana malalamiko yale yalioko ni kwa sababu ya sheria hafifu iliopo au iliyokuwa haikidhi haja ya wakati ule. Sasa nafikiri Tume hii ingekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau.

Kwa mfano, tuna wafanyakazi serikalini, kuna wale wanaoendesha sekta binafsi, kuna shughuli za viwanda hapa, sheria zinazosimamia viwanda au biashara, kuna shughuli za wakulima, kuna hili tatizo ambalo tunalizungumza kila siku la ardhi. Je, haya malalamiko yalioko pengine sheria ina mapungufu.

Kwa mfano, Mhe. Naibu Spika, sisi katika Kamati yetu ulipokwenda tukaulizia kuhusu uhaulishaji wa mali isiyohamishika ikiwemo hii ya ardhi, tukapewa ule utaratibu wake, kwa ghafla utaona kwamba kuna matatizo. Kwa sababu unaambiwa mtu anaweza akauziwa, akishauziwa keshapokea pesa yule aliyeuza ndio tena wanafanya utaratibu wa uhaulishaji. Sasa ikiwa kuna matatizo, matatizo yanakwenda wakati yule mtu keshapokea pesa za kuuziwa. Je, utaratibu huu ni mzuri kutokana na sheria ndio nikasema kwamba Tume hii ingefanya kazi nzuri zaidi kama ingekutana na wadau mbali mbali na kuona michango yao. Sasa wao wanaweza wakapima kwamba haya ni matatizo ya kiuendeshaji au haya ni matatizo ya upungufu katika sheria. Kwa hivyo, badala ya kujikita kuvutana viongozi wa serikali tu na wizarani, basi wapanue wigo wa kukutana na wadau mbali mbali na kuona kwamba je, matatizo yaliopo ni ya kisheria au ni ya kiuendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwa kweli Kamisheni hii inajieleza wazi. Kwanza mimi napenda kusema kwamba sasa hivi kuna vyombo vingi vya kiteknolojia vya kudhibiti takwimu

au *data* tulizonazo, tayari tuna vijana wengi walio na utaalamu huo wa kuweza kuvitumia hivyo vyombo, kama kompyuta na programu nyingi sana zipo za kutengeneza ukaweza kuweka data zako kwa mujibu wa ile hali unayotaka.

Je, kamisheni imeshaingia katika hali hii ya kuweka kumbukumbu ya mali zote walizonazo za Wakfu kwa Unguja na Pemba, tayari zimeshafanyika au mchakato huu uko wa kuzitambua mali tofauti zilioko, mipaka yake na mambo yake, kama ni nyumba kama ni mashamba. Kwa sababu mimi nilipewa taarifa siku moja nikaambiwa kwamba kuna baadhi ya nyumba ni za zamani sana, kwa hivyo kuna wajanja wanajaribu kuzungumza huku na kuzivunja zile nyumba na kujenga nyumba nyengine za kibiashara zaidi. Lakini je, ile ardhi ilioko pale hata kama utaivunja ile nyumba, lakini ile ardhi bado ni ya Wakfu. Je, huyu aliyepewa ruhsa ya kuvunja ile nyumba akajenga nyengine, kapewa mkataba gani, au ndio imeshapita. Yeye keshafanya makosa yake, lakini makosa yale aliyofanya yeye yasifanye ile nyumba isiwe ya Wakfu bado, lakini kama hatuna kumbukumbu nzuri, basi wataendelea wajanja hawa kutuchukua mmoja baada ya mmoja, kwa sababu nyumba nyingi za Wakfu ni nyumba kongwe. Sasa kitu muhimu ni kuwa na utaratibu wa *data* maalum ambazo akianza tu mtu anajua kwamba hapa ni hivi pameshapita ujanja.

Mhe. Naibu Spika, la pili katika Wakfu ni kwamba kuna maeneo katika nchi huwa yana hali ngumu ama watu wake wako katika hali ngumu, au watoto wake wako katika hali ngumu. Ikitokezea misaada inayokuja kupitia kwa Kamisheni ya Wakfu, kuna utaratibu gani wa kuwaangalia hawa watu walioko katika hali ngumu au katika mazingira magumu ya maisha.

Mhe. Naibu Spika, tuna mashirika mengi ya kufanya safari za Hijja na Kamisheni ndio wasimamizi wakuu wa haya mashirika yaliyosajiliwa hapa, lakini kwa wale waliokwenda kule kuna tofauti ya makaazi katika mabanda ya Minna kwa nchi tofauti, ukiuliza utaambiwa aah! Mabanda hayo katika hali hii kwa sababu nchi zao yana watu wao wanayashughulikia, kwa hivyo wanapata ushughulikiaji na nchi zao. Sasa kwa sababu mashirika yanayoongoza sasa hivi kwa kupeleka Mahujaji kwa Tanzania ni ya hapa Zanzibar. Je, haujafika wakati wa kuwa na Mwakilishi wa Zanzibar aliyekuwa katika Ofisi ya Ubalozi wa Saudia anayeshughulikia mambo haya. Naomba Waziri aje atueleze kwamba je suala hili likoje. Kwa sababu kama kuna Mwakilishi wetu katika ofisi ya ubalozi, tusitegemee yule balozi tu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, Zanzibar inaongoza kwa mashirika yanayopeleka Mahujaji, lakini katika Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania kuwe na Mwakilishi kutoka Zanzibar, lakini anawakilisha kwa Tanzania, anayewashughulikia

Mahujaji kule. Kwa hivyo yeye atapata fursa ya moja kwa moja kwenda kuyashughulikia yale mabanda na shughuli nyengine ambazo zitafanyika. Lakini tukipeleka mtu ambaye hayuko *concerned* na hapa itakuwa hana uwezo huo, anakwenda kama ile *pass time* tu, nahisi ziko katika ofisi za ubalozi, wakati mwengine tunawaambia wanaitwa A.T.H.E, wengine wanakuja hapa ofisi za ubalozi wanaleta watu wao wanaita *education* A.T.H.E, sijui *cultural* A.T.H.E na nyenginezo. Sasa na sisi tupeleke A.T.H.E wetu, kwa sababu watu wetu wanakwenda kila mwaka *Alhamdulillah* wanakwenda kule. Sasa kwa nini twende kwenye mabanda ambayo hayakukaa vizuri, wakati sisi uwezo tunao. Kwa hivyo, tunaomba sana suala hilo ulishughulikie na uje utupe mwelekeo. Pia tunaiomba serikali hii ya awamu ya saba iangalie upya suala hili na kuona kwamba huduma ile inaendelezwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika Ofisi ya Mufti. Nashukuru sana kusikia kwamba idara hii inasajili madrasa. Mhe. Naibu Spika, hizi madrasa zinafanya kazi kubwa ya kuwalea hawa watoto na sasa hivi nyingi zao zimetafuta misaada mbali mbali, ili kuhakikisha yale majengo yao yako katika viwango vya kusoma wale watoto, sio vile tulivyosoma sisi majengo ya kuvutiwa paa kwenye upenu. Kwa hivyo, kutokana na hali hiyo na ugumu wa maisha, naomba sana Ofisi ya Mufti ifanye utaratibu, tunasoma humu kwenye bajeti ya serikali misaada kutoka nje ni asilimia 80 au 90 ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Kwa hivyo, sio vibaya na sisi kutafuta hayo maeneo tukawaombea ruzuku hao walimu ambao wanasomesha katika hizi madrasa, hata kama hawakupata kwa kila mwezi, lakini kila baada ya kipindi wakapata ruzuku fulani, kwa sababu wameshasajiliwa itawapa moyo na itawapa muelekeo wa kulea watoto wetu. Pia kuna nchi zinajitolea kutoa misahafu, juzuu na vitabu vyengine vidogo vidogo. Mimi nafikiri ni kazi ya ofisi hii, kuhakikisha kwamba wanatumia fursa zile ili vijana wetu katika madrasa mbali mbali waweze kupata fursa hizo. Kwa hivyo, tunaiomba ofisi hii ichangamke ili tuweze kuvuna na sisi matunda hayo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwanza nampongeza sana Mhe. Mwanasheria wetu anavyojitahidi kutukwamulia mambo yetu humu katika Baraza ya kisheria. Mimi nilikuwa na swali moja tu, katika maofisi mengi siku hizi kuna wanasheria ambao wanawakilisha zile ofisi zao. Nilikuwa nataka nijue, je kuna uhusiano gani kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wanasheria hawa ambao wamo katika maofisi, je wanapata maelekezo, wako masuuli. Maana yake Wizara ya Fedha, Uchumi

na Mipango ya Maendeleo, imewachukua wahasibu wote wanakuwa masuuli kwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Je, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni hivyo hivyo, au wale wanakuwa *independent* wanafanya kwa mujibu wa vile anavyoona yeye tu kule.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuona kwamba ipo haja ya kuwazindua Wazanzibari, kuwaeleza kwamba kuna mchakato wa marekebisho ya Katiba. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nawaomba sana Wazanzibari watumie fursa hii kujikwamua katika huu mkwamo tuliokwama, tusitumie fursa hii kujenga misimamo ambayo ni ya kiushindani. Huyu anasema hivi na mimi nataka kusema hivi. Lakini serikali imekiri tokea mwanzo kwamba itaheshimu na itasimamia watu watoe maoni yao. Je, kama kuna watu ambao wamekwenda kinyume na hivyo na kuwalazimisha watu kutoa maoni yao wanayoyataka, serikali itachukua hatua gani kwa watu hawa. Kwa sababu kuna wengine wanaandika mabarua kupeleka kwenye Tume, sisi tumesema kwamba wananchi wako huru kutoa maoni yao, lakini kama wakitokezea watu kama hao, mimi nafikiri wasinyamaziwe kimya, waitwe na waulizwe wana madhumuni gani. Au na wao wameshapewa kidogo. Kwa sababu unapofanya *acting* haiwezekani iwe hivi hivi tu, kama na wewe hujapenyezewa mfukoni. Sasa kama wameshapenyezewa mfukoni, basi wasiwahadae Wazanzibari, wana haki yao na wana maoni yao. Ushirikiano katika dunia ni muhimu sana, lakini ushirikiano unaolinda haki ya mtu mmoja, unaolinda heshima ya mtu ndio ushirikiano utakapokuwa mzuri. Lakini ikiwa mtu anakudharau, anakukejeli na kukufanyia kila aina ya mambo ambayo hayalingani katika ushirikiano wenu, ushirikiano huo utakwenda vipi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, kuna watu wanafanya kazi iliyokuwa sio yao humu. Mhe. Naibu Spika, hajanionesha saa, unanionesha wewe. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana tutizame tulikotoka, tutizame nchi yetu inapokwenda. Sisi hapa tunaambiwa hatuna kauli popote pale. Hawa wana michezo wenzetu walijitahidi, tutaingia katika FIFA. Wameingia wapi, jambo dogo tu hawakuweza kujitolea wao, wakasema kwamba aah! Hawa waingizeni ni ndugu zetu, jambo dogo tu la michezo, je hayo mambo makubwa, aah! Wazanzibari nyinyi. Vyama hivi ni vya kupita, kwa sababu hapa kilikuwepo Afro Shirazi, kikaondoka kikaja CCM na hii CCM itaondoka na CUF itaondoka, lakini Zanzibar ipo. Twendeni tuilinde Zanzibar kwa kizazi chetu kinachokuja. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kwanza nitaanza *Audhubillah Minna Shaitwan Rajjim, Bismillahi Rah-maan Rah-hiim,* Mwenyezi Mungu niongoze katika kujadili na kusaidia hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpe pole ndugu yangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary, nimpe pole sana kwa wizara hii, maana hawa ndio wanaotuongoza. Niseme tu kwamba Mhe. Abubakar Khamis nitakukumbusha nyuma, kwa sababu umepewa wizara ambayo ndio dira na muongozo wa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, wizara hii kila kitu chake ni nyeti, ukija kwenye katiba kama una nchi haina katiba basi haijakamilika nchi. Ukija kwenye nchi kama haina sheria basi nchi haijakamilika. Lakini makubwa mengine zaidi yamehusisha na dini na sisi Wazanzibari asilimia 99 ni Waislamu, ndio maana nikakupa pole ni mambo nyeti katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka nimkumbushe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Abubakar Khamis, huko nyuma na mpaka sasa hivi tuna Chama cha CCM na Chama cha CUF. Huko nyuma ilikuwa CUF hata ikisema nini basi CCM inampinga, na CCM hata ikisema neno gani kuitetea serikali basi CUF inapinga kwa asilimia 100. Mimi na wewe ndugu yangu Mhe. Abubakar Khamis tulikuwa tunangoja, ukisema wewe na mimi nakujibu, na ulikuwa mkali mno kipindi kile. Maana yake nimesema nitakukumbusha ya nyuma. Ulikuwa mkali mno na ulikuwa unaijejea Serikali ya Mapinduzi na ulikuwa una kitabu cha katiba na sheria wewe ndio nambari moja. Lakini Mwenyezi Mungu amepitisha rehma zake, ametuletea Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Serikali ambayo haina CCM, wala haina CUF katika jukwaa hili tunalozungumza. CCM wakati wa uchaguzi atakwenda na CCM yake na CUF atakuwa na chama chake wakati akienda kwenye uchaguzi.

Kwa hivyo, ndio nikakuambia nakupa pole ndugu yake Mhe. Abubakar Khamis. Serikali hii imo mikononi mwako, ukiiyumbisha wewe kwenye mambo ya Katiba na Sheria basi utakuwa umeiyumbisha nchi Mhe. Abubakar Khamis. Lakini kwa imani yangu kubwa niliyokuwa nayo juu yako, kwa sababu wewe ni mzalendo wa nchi hii na unaionea uchungu nchi hii, basi utaipeleka nchi hii kwa utaratibu wa sheria na katiba.

Nakusaidia sasa Mhe. Ababakar Khamis. Humu tunatetea maslahi ya wananchi na maendeleo ya wananchi, kwa sababu wao ndio waliotuteua wakatuleta humu, iwe kwenye jimbo, iwe kina mama sisi, sisi ndio wazazi, sisi ndio walezi na sisi ndio tunajua shida katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamezungumzia kuhusu maoni ya Katiba. Mimi nilizungumza katika wizara mbili, sitaki nirejee. Mhe. Ismail Jussa amesema vizuri na Wajumbe wengine wamezungumza vizuri. Mimi sasa nataka kuichangia hii wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, tuna Kitengo cha Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Abubakar hiki ni kitengo muhimu sana. Kwanza uje unieleze ni sheria ngapi zimepitwa na wakati, ni sheria zipi na zipi, kwa sababu sisi kwa kutunga sheria ni mahodari kweli kweli, lakini namna ya kuzitumia sheria hatuwajibiki ipasavyo. Sasa ni sheria zipi tumezirudia rudia, maana yake sisi kutunga sheria ni mahodari, lakini nina hakika kuna sheria nyengine tumezirudia rudia.

Mhe. Abubakar Khamis nakuomba sana kakae na watu wako, uje utueleze ni sheria ngapi na ni sheria zipi ambazo zimepitwa na wakati. Kwa sababu sasa hivi tunakwenda kwenye karne ya sayansi na teknolojia.

Nije katika kitengo cha Mufti na bwana Kadhi. Kwanza nitoe pongezi kwa uteuzi wa Mufti na Naibu Mufti wake, pia nimpongeze Katibu wa Mufti na kitengo kile kwa jumla. *(Makofi)*

Kwa kweli mimi naomba sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kitengo hichi ni muhimu sana, kwa sababu ni kitengo ambacho kwa upande mwengine kitakuongoza, kwani hapa umeona hali ya hewa na wala sitaki niirudie Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mufti, Naibu Mufti na Katibu lazima wabadilike, na kubadilika kwao ni wewe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kwani nina hakika kitengo hichi kiko katika mambo magumu na wala sijui kama Mufti anayo gari, na taarifa niliyoipata anayo gari iliyoombwa huko nyuma *shaghala baghala* kwa ajili ya Kitengo cha UKIMWI. *(Makofi)*

Lakini Katibu alifanya kila aina na kupatikana gari nyengine, sasa sijui na nauliza serikali imempatia gari Mufti kama ni serikali. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anipe jawabu. *(Makofi)*

Vile vile suala jengine ni kuhusu upungufu wa wataalamu katika Kitengo hichi, nimesoma hii hotuba ya bajeti, lakini kuna matatizo kidogo. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba awasaidie sana kitengo hichi.

Sasa naomba nizungumze na Mashekhe wangu ambao nimewataja pamoja na Makadhi kwa jumla na mtanisamehe, kwa sababu hapa niko katika utetezi. Kwa hivyo, mtu lake akilifanya zuri mpe na akilifanya baya mkosoe na mwenye kukukosoa anakupenda. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sisi kama wanawake kuna madhambi yanafanyika kama vile ndoa za ovyo ovyo na talaka zinatolewa ovyo, mtu anakwenda na akishatoa shilingi 100,000/= au 200,000/= basi talaka anaipata. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nakuombeni sana kwa sababu hakuna kitu alichokichukia Mwenyezi Mungu kama talaka. Lakini sisemi Makadhi wote, isipokuwa ni baadhi na Kariakoo mtindo huo upo. Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana kwamba twende kwenye mstari ulionyooka katika dini yetu ya Kiislamu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu wafadhili wetu wa Misikiti. Kwa kweli tunashukuru sana wafadhili wetu wa Misikiti. Lakini hebu tuone na kule vijijini Misikiti tusiijenge mijini tu, na vijijini tuende kwa sababu kule ndiko kwenye wananchi ambao ni *twaa*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwani ni vijiji vichache tu ndio utaona kuna misikiti ambayo imefanyiwa na wafadhili. Mhe. Waziri nakuomba sana na wenyewe wanatusikia wako nyuma. Kwa hiyo, naomba tufanye kila aina na tuwape wananchi wetu huduma sawa katika mambo haya. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Vyeti vya Kuzaliwa, na huko ndio kuna uvundo. Mhe. Naibu Spika, kwanza kuna vyeti *fake* naomba kumpa taarifa Mhe. Waziri kama yeye hana habari, basi sisi tunamwambia, na pia tunaisubiri na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huko mbele. *(Makofi)*

Mhe. Waziri hivi sasa tuko katika *science* na *technology*, bado sisi tunachukua peni na kuandika kwenye karatasi na ndio maana vikatokezea vyeti *fake* vya kuzaliwa. Kutokana na hali hiyo, tunaomba sana na Mhe. Waziri tunakuomba sana Mwenyezi Mungu amekupa ujuzi wa aina yake, hebu utumie huu ujuzi ili upate mustakbali mwema kwa wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Suala la ucheleweshaji wa vyeti halisemeki na wala sijui kuna maradhi gani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba maradhi haya hakuna wa kuyatibu isipokuwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwa kweli maswali mengi yaliulizwa hapa na hata juzi

kwenye Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria lolote litakalotekea kwenye Kamisheni hii, basi ujue Mwenyezi Mungu anakuhukumu wewe, kwa sababu hukutenda haki na kwa nini hukutenda haki, watu wako hukuwasimamia ipasavyo. *(Makofi)*

Kwa kweli mtu yeyote Mwenyezi Mungu anamuamrisha mtawala na kuamrisha mteue Abubakar Khamis Bakary kuwa ndiye awe Waziri wa Katiba na Sheria, imetoka kwa Mwenyezi Mungu na kumuamrisha Rais. *(Makofi)*

Sasa wewe ujue kesho utakwenda kuulizwa uliifanya vipi kazi yako vizuri? na wala tusione huu ni mchezo wa hapa duniani jamani, leo hii ni mara ya pili nazungumza suala hilo, kwamba huu ni mchezo lakini Mwenyezi Mungu anakwenda kukuhukumu wewe na wala hamuhukumu Rais na Mhe. Abubakar Khamis Bakary uko katika *dilema* kwa Wizara hii ya Katiba na Sheria. Kwa hivyo, nakuomba sana na ninavyokujua utatekeleza wajibu wako ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimesema mengi, lakini naomba sana Mhe. Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa wenzangu, kwamba sisi ndio watungaji sheria, basi tuwe na sisi sheria zile tunazisimamia ipasavyo, sio sisi tukiuke sheria. Kwa hivyo, tukienda hivyo tutakuwa tunakwenda kinyume na maadili yaliyotuleta humu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimesikia michango ya watu wengi sana wakati walipokuwa wakichangia, lakini la mwisho niombe watu wote ambao wenye Vitengo vya dini ikiwa ni Mufti, Kadhi, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, mambo ya Hijja nakuombeni sana wazee wangu, kwamba mutumie vyeo vyenu kwa mujibu wa taratibu zinazotuongoza kwenye dini yetu. *(Makofi)*

Kwa kweli nyinyi ndio ambao mnaotoa mawaidha, mnaotuelekeza, pia mnatupa mambo ambayo ya kutupeleka aidha peponi, lakini sisemi wote na ninakuombeni munisamehe huko nyuma, baadhi yenu munatupotoshea watoto wetu. *(Makofi)*

Kwa mfano, vyuoni hivi sasa tunaogopa kuwapeleka watoto wetu, imekuwa kama mchezo wa kawaida, kwa sababu hapa tupo kwenye sheria na mimi nitasema wazi wazi. Kwa kweli imekuwa kama ni mchezo si mwanamke wala mwanamme, wale mnaowaacha vyuoni ndio wanaojifanya walimu wakuu kutuharibia watoto wetu, kama hilo hamna basi sisi tunakwambieni, kwa sababu sisi ndio wenye watoto pamoja na wajukuu na tunayaona. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, mimi nasema yeyote anayekwenda kinyume Mwenyezi Mungu alipe rada ambayo haimithiliki, maana nimesoma *Agh'udhubillahi Minashaitwani Rajjim na Bismillahi* na siku ya leo Mwenyezi Mungu atusaidie. Lakini hatutokubali vijana wetu wanaume kufanywa mabibi na wanawake kupotoshwa, upotosho ambao Mwenyezi Mungu hakukubaliana nao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimesema niyaseme haya na iwe hii ndio kama kusema kwangu ni hitimisho na niombe kheri katika wizara hii. Lakini nakwambia tena Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kazi kubwa unayo, ukiiendesha kombo nchi hii, basi unaiendesha wewe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, nafikiri umenielewa vizuri kwa nini nikasema hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo na wala sizuii fungu hata moja, isipokuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa tunampa Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, afuatie Mhe. Mussa Ali Hassan na baadaye Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Mansoor Yussuf Himid) ajiandae kumalizia, dakika 20 tu kila mtu na tujali muda.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wageni waliohudhuria huko juu. Nachukua fursa hii kukushukuru tena Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuipongeza Hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa hotuba zao zote mbili nzuri, zenye hekima, busara na usikivu kabisa. *(Makofi)*

Vile vile nichukue fursa hii kuzipongeza taasisi zetu hizi ambazo ziko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi zote za Mufti, Kadhi Mkuu, Idara ya Mrajis Mkuu, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pamoja na sehemu zote zinazohusika. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatakia kheri na pia nitahakikisha nitakuwa karibu nao wizara hii na taasisi hizi kwa faida ya Wazanzibari na Watanzania kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ofisi hizi zinataka zisukumwe, na kusukumwa kwa ofisi hizi ni sisi Wazanzibari kwanza tunatakiwa kuzisaidia ofisi hizi ambazo ziko chini ya mamlaka ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama vile Mufti, Kadhi

Mkuu pamoja na sehemu nyengine zinazohusika, ili ziweze kufanya kazi zao ipasavyo. Kwa kweli naamini wakati mwengine shida yao ni zana za kufanyia kazi. *(Makofi)*

Lakini mimi sina pingamizi nao, tena nawaombea kila la kheri kwa kazi yao ngumu, kwa sababu kazi walizokuwa nazo ni dhamana kubwa katika sehemu zote hizo, basi sote mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Uzini nawaombea kila la kheri katika kazi zao, ili waweze kuendelea kwenye maadili mazuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili nije katika suala zima la marekebisho ya Katiba, ambalo liko kwenye volume 125 na 126 ukurasa wa 54 na 55, ambazo zinazohusu ofisi mbili ambazo ni mihimili Wizara ya Katiba na Sheria, kwa maana Mhe. Waziri mwenyewe mzee wangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ambaye pia ni kaka yangu Mhe. Othman Masoud Othman. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni yetu na *we are all in transit*, tuendapo ni padogo sana. Mimi naamini ofisi hizi, imani yangu na imani ya wenzangu nina hakika, basi watusaidie kuweza kufanya marekebisho au kuelezea hali halisi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, leo nataka kuelezea machache fursa hii niliyoipata nikiwa kama Mzanzibari, ni machache lakini nataka kuwaelezea hali ya Wazanzibari tulivyo ndani ya Muungano. Mhe. Naibu Spika, tarehe 18 kesho kutwa Jumatano panapo uhai na uzima *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu natimia miaka 50 siku yangu ya kuzaliwa. *(Makofi)*

Lakini Muungano wetu huu ni Muungano wa kihistoria, yaani ni Muungano wa faida zote mbili, maana ya Zanzibar na Tanganyika tukaita Tanzania. Muungano wetu huu tulivyoambiwa kulikuwa na mambo 11, lakini leo tunaambiwa kuna mambo 22 na tujaalie hayo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, sisi kama nchi Zanzibar tulipaswa tuone ule Mkataba wa Muungano wa sehemu ya Tanganyika na Zanzibar na tukaita Tanzania, ili vizazi vyetu, watoto wetu pamoja na wajukuu zetu waje kuelewa maana ya historia ya Muungano, tena Muungano huu ni wa Marais wetu kwa nchi zote mbili na walifanya kwa maslahi ya pande zote mbili. *(Makofi)*

Jambo la kusikitisha Mhe. Naibu Spika, mpaka leo huo mkataba hatuuoni na wala hatuelewi huu muundo wa Muungano nani anasimamia. Kwa kweli kama nilivyosema kwamba kuna mambo 11 na leo tunaambiwa 22. Lakini

nataka nilihakikishie Baraza hili Mhe. Naibu Spika, haya 11 hakuna saini ya Viongozi Wakuu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tunafanya maslahi mazuri katika umoja wetu, na maana ya Muungano kuna vitu vimeungana au viungo vimeungana. Mhe. Naibu Spika, kwa faida yetu sisi na ninataka kusema na kuihakikishia dunia kwamba Wazanzibari ni watu wastahamilivu, watulivu, wastaarabu pamoja na kukinai. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, chini ya Mfumo wa Chama kimoja Wabunge wetu wa Zanzibar kule Dodoma walifukuzwa na kuambiwa tokeni, kwa sababu mnakuja kuchukua posho, tupo ndani ya Muungano narejea historia. *(Makofi)*

Vile vile tulikaa na kuambiwa mwelekeo ni serikali moja tuko ndani ya Muungano, nchi zimeungana na wenzetu hawa walituambia tupo kwenye serikali moja. Mhe. Naibu Spika, mimi niliwaambia wakati ule labda mutawale minazi, mikarafuu na miembe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, haikutosha hapo pia tuliambiwa Zanzibar si nchi na ikawa zahama kubwa sana. Sasa naomba tupate ufafanuzi serikali zote mbili Rais wa Jamhuri ya Muungano ameunda Tume ya kukaa Wanasheria ya pande zote mbili kujadili hatua hii ya Tume ya kuhusu Zanzibar si nchi. Kwa kweli ilikuwa ni kiini macho mpaka leo hatujui vikao vingapi na taarifa iko wapi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itueleze hapa kwamba hii Tume au Kamati imekaa mara ngapi kati ya Mwanasheria Mkuu wa Bara na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, ili waje watueleze tulivyoambiwa kwenye Vyombo vya Sheria Dodoma kuwa Zanzibar si nchi.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwaambie Wazanzibari humu ndani pamoja na dunia nzima, wenzetu walikuja kuuliza na haya yote yapo. Kwa kweli wenzetu walikuja kuuliza uhalali wa Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Sherehe zetu za Mapinduzi kuingia mwisho pale Uwanja wa Amani. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, wenzetu Bara walikuwa wanataka mpaka kufuta Mapinduzi matukufu ya Zanzibar Rais wetu anapoingia Uwanja wa Amani, tena kwa maandishi kwamba uhalali wa Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nini anaingia mwisho, kwa nini asiingie mwanzo kwa sababu kuna Rais wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Jamani tumeunganisha nchi mbili na Rais ya Jamhuri ni Rais wa Jamhuri ya watu milioni 30, na Rais wa Zanzibar ni Rais wa watu milioni 1, na wote wako sawa ndani ya Muungano, ndani ya Muungano wetu hakuna bwana wala hakuna kiongozi ambaye yuko juu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini haikutosha hapo Mhe. Naibu Spika, wenzetu waliuliza uhalali wa kupigiwa Rais wanaokuja Zanzibar mizinga 21 pia walitaka kuondosha hii. Sasa Mhe. Naibu Spika haya yote ninayozungumza mimi na kwa bahati nzuri Wazanzibari tulikaa kikao na tulisema mkiondosha mizinga tunawaleta Askari wa KMKM wapige risasi 21. Kwa hivyo, tukimpokea Rais wa nje hapa Zanzibar kwa mizinga hamutaki basi tutapiga risasi 21. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika mazingira kama haya leo tunaambiwa Idara ya Anga imo ndani ya Muungano, yaani kila jambo na wenzetu wakitaka suala lolote kufanya *amendment* kuhusu Katiba wao ruhsa, sisi tukitaka kujitanua katika masuala yoyote lazima tukatake kibali, ndipo pale niliposema kwamba cheti cha ndoa tunachukua Dodoma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tumeingia kwenye mchakato wa Katiba na huyu Muungano mgonjwa unampeleka hospitali ana njaa, maana unampeleka hospitali huyu Muungano tayari mgonjwa ana njaa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, naona ni vyema tungelikaa kwanza na kuyamaliza matatizo yetu ambayo yapo na halafu tukaja kwenye huu mchakato, kwa sababu matatizo mengi hatukuyaweza kuyamaliza na tulikuwa tunapeana ma-kalenda, kila kiongozi anapokuja tunapeana ma-kalenda, Rais wa Muungano anakwambia miezi 6 tu tutaondosha Muungano, na sisi Wazanzibari tunapewa Maandamano ya Kumpongeza. *(Makofi)*

Sasa ninachotaka kusema mimi Mhe. Naibu Spika, kwa hali tuliyokuwa nayo kuhusu suala zima la Muungano halina sura ya Muungano, kwa sababu hata hiyo *Cabinet* ya Muungano inayokaa Bara, ambapo Mawaziri wetu wa Zanzibar wanashiriki na wale hawana mamlaka ya kuzungumza mambo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hata Mhe. Rais wetu wa Zanzibar anaingia kwenye Baraza la Mawaziri ambalo linaongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano tujaalie alipinge jambo pale, basi labda ajiuzulu lakini haliwezi kukubalika kwa sababu pale kuna *vote* ya kura. *(Makofi)*

Sasa ukitizama kwa jumla Mhe. Naibu Spika, matatizo yote haya tunapozungumza Muungano, lakini matatizo yapo katika huu utendaji mzima

wa huu Muungano wetu, kwa sababu sisi tumetoa nchi yetu, kama vile tulikuwa na mabalozi wetu, kiti chetu cha Umoja wa Mataifa tena ni mambo mengi kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kazi tuliyokuwa nayo mbele yetu ni ngumu sana. Kwa kweli huu mchakato wa Katiba, unakuja kuambiwa usizungumze Muungano, zungumza Katiba na hii ni Katiba gani? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika mazingira tuliyonayo tungelikaa kitako pamoja na Wabunge wetu wanaobweka kule Bara wa Tanganyika, tuwalete Zanzibar na tuwafundishe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar idhamini Wabunge na tuwalete na tuwafundishe nini maana ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, haya matokeo yote haya. Kwa mfano, kuna mmoja juzi katika masuala ya Zanzibar si nchi tena Kiongozi Mkuu Mstaafu wa Chama, alisema Wimbo wa Taifa wa Zanzibar sasa ni wimbo wa Taarab, na hilo ni tusi la mwisho. Sasa Zanzibar tukizungumza jambo dogo tunaambiwa tunataka kuvunja Muungano, maana "*mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu*". *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, huko tunakokwenda *huwezi kuutafuta mwezi bila ya nyota*, na wala *huwezi kujenga nyumba ndani ya mawingu*. Kwa hivyo, ninachokiomba Mhe. Naibu Spika kwa maslahi ya Zanzibar, pamoja na hali tunayokwenda nayo hayo, nilisema Wazanzibari kesho tusistaajabu tukaambiwa Zanzibar mnaongozwa na mikoa mitano na jeshi linakuwepo Zanzibar ndio basi Zanzibar haipo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nilisema hapa kwamba walikuwa wakiuliza uhalali wa Rais wa Zanzibar Mapinduzi Matukufu pale Uwanja wa Amani tarehe 12 na walitaka Rais wa Jamhuri aingie mwisho hii nchi yako, kwa sababu kuna utaratibu tumeunganisha nchi mbili huru. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninachotaka kusema wamekaa na kuuliza kwa nini tunapiga mizinga Waziri wa Katiba na Sheria wa Bara alitamka wazi kwamba Zanzibar imevunja Katiba kwa kupiga mizinga 21, tumenyamaza kimya sote. Mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, tunajukumu lakini uongozi ni dhamana, uongozi ni halbadiri. Tunapochukua dhamana ya mambo kama haya lazima tuelezwe ukweli katika tatizo lenyewe la Muungano. Maana kuna vitu hivi, tuliambiwa Zanzibar si nchi, kesho tutakuja kuambiwa aah kwa sababu kuna mchakato wa Katiba ile Zanzibar si nchi Tume imeundwa ishakufa. Alah! hili suala mbali. Mshatwambia ndani ya Bunge Zanzibar si nchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa hali hii nina uchungu na nchi, naipenda nchi yangu, naupenda Muungano wangu lakini Muungano uliokuwa na usawa wa kuheshimiana. Muungano ambao hauna bwana ndani ya Muungano. Kwa hivyo katika mazingara kama yote hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri niwaombe kwa heshima na taadhima, Waziri wa Sheria na Katiba, Afisi ya Mwanasheria Mkuu, waone kwamba mtiririko mzima huu niliouzungumza, akufukuzae hakwambii toka. Hali hii tunayokwenda nayo tupate ufafanuzi. Maana Katiba yetu tunayo, humu ndani ya Baraza tumewakilishwa na Katiba yetu na ndiyo inayomfanya Rais wa Zanzibar aingie madarakani ndio atuongoze sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini Katiba hii na uhuru tuliokuwa nao unaendaje katika hali halisi ilivyo na katika muundo mzima ulivyo wa Katiba yetu.

Mhe. Naibu Spika, natoa tahadhari haya mambo tena yalikuwepo tena kwa maandishi, sema sisi tulikuwa masugu tu. Tulikuwa tunafanya mambo mengine kimabavu tu. Ninachohofia mimi kesho tutakuja kuambiwa tuna Mikoa mitano ndio basi, Zanzibar Mkoa tu. Ninachoanza kusema kwamba Wazungu wanasema *"You make somebody once stupid, but you cannot make all stupid, enough is enough.*

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema sasa, kwamba jamani twendeni katika mashirikiano, twendeni katika kudumisha, lakini tunataka utaratibu wetu, Rais wetu, viongozi wetu. Katika masuala mazima ya Muungano, Wazari wa Katiba, Afisi ya Mwanasheria, suala la Anga mtusaidie ili iwepo na maelewano mazuri kati yetu na Bara katika mazingira ya kuheshimiana, katika mazingira ya kuvumiliana na katika mazingira ya kujadiliana.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Uzini naiombea kheri Wizara ya Sheria na Katiba, naiunga mkono asilimia 100 na zaidi ya 100. Lakini vile vile naomba katika madhila kama haya umebeba majukumu ili mje kutusaidia kutupa ufafanuzi wa mambo haya, ili tuendenao huu Muungano wetu katika njia inayoeleweka, inayofahamika, tupate manufaa kwa pande zote mbili. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa kuwaza kunipa nafasi hiyo kuchangia Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2012.

Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na nashukuru sana Mhe. Naibu Spika kwa kuweza kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba na pia kumpa hongera sana kwa kuweza

kuiongoza Wizara hii ngumu katika kipindi cha Serikali ya Ummoja wa Kitaifa.

Kwanza nichangie ukurasa wa 11 kuhusu Mahakama zetu juu ya uhai wake na uzima wake. Mahakama zetu za Mkoa wa Kusini hivi sasa zipo katika hali duni. Naomba Mhe. Waziri ahakikishe anazisaidia sana katika matumizi yake ili ziwe Mahakama za kisasa. Tunajua kwa vile ni Mji wa pili kwa Unguja kwa ukubwa kwa hivyo ijengwe Mahakama kama ile ya Vuga.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ahakikishe wafanyakazi wa Mahakama wanapata nyumba za kuishi kwa wale waliokuwepo mashamba kwa sababu kuchanganyika na raia si vizuri ni lazima wawe na *cottage* zao ambazo zinalindwa kwa wakati wote.
Mhe. Naibu Spika, vile vile Majaji wetu wanahitaji wapatiwe usafiri ili kila mmoja awe na usafiri wake, haipendesi Jaji anakutwa njiani tena usiku akiwa anatembea na vespa. Hii kwa Majaji sio jambo zuri. Tunashauri watu wetu wahakikishiwe kwamba wanapata vipando pamoja na nyumba ili wawe na maisha ya kisasa kama zilivyo Mahakama zetu za hapa mjini ambazo ni za kisasa.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa nambari 54 kuhusu marekebisho ya Katiba. Marekebisho ya Katiba ni wajibu wetu sisi Wawakilishi kuweza kuzungumza, lakini haitupasi kuweza kuwasemea wananchi wetu. Kwa sababu Katiba imetoa nafasi kwa kila mwananchi aweze kujisemea mwenyewe lipi analiunga mkono na lipi analitaka katika Katiba.

Mimi sipaswi kuwasemea wananchi wangu wa Jimbo la Koani wafanye nini, isipokuwa mimi niwasisitize tu kwamba wafike kutoa nasaha zao pamoja na kutoa maoni yao. Mimi sielewi maoni gani wanataka, lakini naunga mkono maoni yote wanayozungumza wananchi wangu wa jimbo la Koani.

Mhe. Naibu Spika, nichangie zaidi kuhusu suala la Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba, kuhusu Afisi yake inayohusika na shughuli za usajili. Kwa mujibu wa sheria zinazoongoza aina mbali za usajili kama Afisi ya Msajili ndiyo yenye mamlaka ya kusajili, naamini kwamba sheria wanazo za kuzifuta taasisi za Jumuiya zote ambazo zinakwenda kinyume na malengo yaliyoweka na ile taasisi husika. Sheria Nambari 6 ya Usajili ya mwaka 1995 kifungu cha 13 kinaambatanisha hayo niliyoyasema. Mhe. Waziri kuweza kuzifuta taasisi zinazofanya shughuli zake kinyume na malengo yaliyoainishwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Jumuiya ya UAMSHO hivi sasa inafanya kinyume na malengo ya usajili. Maelezo yangu hayo naomba nipatiwe jibu kwa nini Mhe. Waziri kwa mamlaka uliyonayo unashindwa kufuta shughuli zote

zinazofanywa na Jumuiya hii ya UAMSHO au na wewe Mheshimiwa unahusika na Jumuiya hii. Mheshimiwa naomba unipe jibu au nitazuia Kifungu cha Afisi ya Mrajisi Mkuu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mzanzibari halisi na Mzanzibari mwenye uchungu wa nchi hii na Muungano naujuwa wa Tanzania. Mimi niliapa kwa vitabu hivi viwili navyo ni Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Tanzania. Nashangaa sana anapokuja mwananchi yoyote akasema kwamba Katiba ya Zanzibar haifai na haijui chochote. Mimi najua Katiba ya Zanzibar ndiyo iliyonipatia kazi mimi na nikaweza kuingia humu ndani. Katiba ya Tanzania ndiyo inayoniongoza kuweza kuongoza jimbo na mimi nikawa naeleweka kwamba mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Koani Zanzibar na kiongozi wa Tanzania na popote ninaposhuka naeleweka huyu ni kiongozi wa Tanzania.

Sasa mtu kusema Muungano hauna faida hilo suala si kweli. Mimi ni Mzanzibari tena ni Mtanzania tena nina uchungu wa Zanzibar hii na Tanzania hii kwa sababu maalum. Katika Tanzania hii nimepata tabu sana, katika Zanzibar hii nimepata tabu sana, hasa ilipoingiliwa Tanzania ikavamiwa na maadui wa Tanzania. Sisi Wazanzibari ndio wakwanza tukaweza kuingia mipakani kuweza kuikomboa Tanzania pamoja na Wazanzibari wengine.

Ni vigumu kusema mtu haelewi neno Muungano, Muungano ambaye haelewi labda huyo si Mtanzania. Kwa sababu pengine wamo wengine wana uraia mbali mbali. Utakuta mtu hana uraia halisi wa Zanzibar lakini ana uraia aina tatu, anachagua tu uraia anao upenda ndio anaoutaka. Hata mitaani utamkuta mtu anasema yeye anagombania Zanzibar lakini ukitangaza anakwambia mtu huyu alikuwa jeshi wa nchi nyengine. Mtu huyo hawezi kuwa mwanajeshi wanchi ile kama hakuwa raia wa nchi ile.

Mimi naweza kusema ni Mzanzibari kwa sababu mimi nilikuwa katika jeshi la Wananchi wa Tanzania. Naweza kusema kwamba mimi ni Mzanzibari halisi. Mimi ni Mtanzania. Kwa hayo Mhe. Naibu Spika, nisiwe na wakati mwingi wa kuhoji. Nasema naiunga mkono hoja hii mia kwa mia pamoja na wanachi wangu wa jimbo la Koani. Ahsante sana.

Mhe. Mansoor Yussuf Himid: Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha au kuniwezesha mimi na nyinyi wenzangu Wajumbe wa Baraza hili tukufu la Wazanzibari kuwa hai na kuwa na pumzi ya kufanya shughuli hizi adhimu za usimamizi wa shughuli za Wazanzibari na mustakbali wanchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja na namtakia kila la kheria Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Wataalamu wa Wizara yake. Naungana na

Mhe. Asha Bakari kukubaliana naye juu ya unyeti na umuhimu wa Wizara hii katika mustakbali wanchi yetu na udumishaji wa misingi ya utawala bora na ya Katiba.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja nilikuwa nataka kuchangia mada moja tu ambayo imeelezwa na Mhe. Waziri kwenye kitabu cha hotuba yake, hilo ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na mustakbali wa nchi yetu ndani ya utaratibu ambao unaendelea hivi sasa. Nitagusia michango ya wajumbe watatu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na hatimaye ndugu yangu, kaka angu, Mhe. Mohamedraza Hassanali.

Mhe. Mohammedraza mimi namuhusudu sana, na namuheshimu sana, tangu nimeanza kumtambua miaka 20 iliyopita. Nikiongozi mmoja mkweli, mwenye msimamo wa dhati usioyumba na amekuwa tayari kuitetea na kuisemea Zanzibar wakati watu walikuwa hawathubutu kusema, hii ni miaka 20 nyuma. Kwa sababu akiwa mshauri wa aliyekuwa Raisi wetu mpendwa Dokta Salmin Amour Juma. Ni awamu ambayo kwa kweli ilichukua maamuzi ya kijasiri sana. Hata haya mafuta na gesi asilia ambayo tunayazungumza leo kwa kinywa kipana lakini ulikuwa utawala wa Dokta Salmin ambao ndio ulioweka misingi madhubuti ya utetezi na ulinzi wa maslahi ya Wazanzibari na kuna mengine nitayazungumza.

Namuheshimu sana Mhe. Raza kwa maana tangu miaka ile hadi hii leo msimamo wake juu ya Zanzibar ndani ya Muungano huu hautateteruka na umekuja kuimarika. Pia namuheshimu kwa ujasiri wake. Namtakia kila la kheri na *Ishaallah* Mwenyezi Mungu atampa uwezo na upeo mkubwa zaidi wa kuitetea Zanzibar na Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, *awwalan* kwa maana la mwanzo, nataka kulizungumza maana ya neno "JAMHURI" nini maana yake. Ukichukua makamusi ya Kiengereza nimeyapitia matatu, moja *Chambers /Thesaurus* la pili *Oxford* la tatu *Macmillan* Yote ninayo kwangu. Yote hayo yanakupa tafsiri moja tu, nayo ni kama hii ifuatayo:

Jamhuri ni mfumo wa utawala unaongozwa na Rais na Wawakilishi wanaochaguliwa na watu. Inaendelea kusema kwamba Mfalme na Malkia hawachaguliwi wanajichagua. Nimeanza kutoa taafsiri ya maana ya Jamhuri kwa sababu kuna maneno yameshaanza kwa baadhi yetu. Yanasemwa kwamba tunaotaka mabadiliko katika mfumo wa Muungano kwamba tunataka bwana Sultani arudi.

Nataka niwambie Wazanzibari msikubali kudanganywa. Ni aibu kwa wale waumini wa *Afro Shirazi Party* baada ya karibu miaka 48 ya Mapinduzi yetu

tunashindwa kujiamini na hata leo tunakubali kwamba atarudi mfalme hapa, atapitia kwa mlango upi. Kwa maana ndio hofu tunaowajenga wazee wetu huko kuwaondosha kwenye mambo ya msingi ya utetezi wa nchi yetu na kutaka kuanza kuwatia hofu kwamba hapa atarudi Mfalme.

Katiba hii ya Zanzibar hairuhusu kwa njia yoyote ile, mtu asiyechaguliwa kushika nafasi ya uongozi ndani ya nchi yetu. Huyo mfalme anamjua nani hapa, nilisoma makala moja katika gazeti Mhe. Naibu Spika, muandishi akawa anauliza kwamba ukipiga kura ya maoni leo ukawauliza wananchi wa Zanzibar baina ya Jemshid na Marehemu Mzee Karume nani wanamjua zaidi, mpaka mtoto mdogo atakwambia Marehemu bwana Abeid Karume. Sasa Bwana Abeid akiwa mfalme yeye ndiyo Mfalme wetu.

Lakini hapa Zanzibar hakuna njia yoyote ile ya kurudi Mfalme. Kwa maana Wazanzibari hatupendi wala hatutaki kutawaliwa. Ndio maana Januari 12 mwaka 1964 tukawaondosha wakoloni wawili hapa. Miongoni mwa nchi chache tuliofanya hivyo, tumemuondosha Muingereza na Mfalme aliyetoka Oman kwa mpigo mmoja. Kwa sababu hatupendi kutawaliwa. Ndio maana kwenye utaratibu wote huu, mnaouita mchakato wa Muungano kelele zimekuwa nyingi kwa sababu Wazanzibar hatupendi kutawaliwa. Haimo ndani ya damu yetu, wala mazoea yetu, wala muelekeo wetu. Ndio maana Januari 12 tukamfukuza aliyetaka kutawala.

Nataka kuwahakikishia Wazanzibari hatukubali kurudi katu Mfalme mwengine. Utaratibu aliyotuachia Marehemu Mzee Karume na tarehe 13 aliitangazia " Kwamba sasa Zanzibar ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar" Jamhuri kwa maana ya *Republic* na sisi tunafanya *Republican System of Government* kwa maana ya utaratibu unaotokana na Jamhuri kwa utaratibu ule niliouleza mwanzo, Rais anachaguliwa, Wawakilishi wanachaguliwa, Wabunge na hata hao waliochaguliwa humu ndani wamechaguliwa na watu waliochaguliwa na watu. Kwa maana wana uhalali, vyengine vyovyote Wazanzibar wa leo hawakubali.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana katika hili maneno yamekuwa mengi kwa sababu hatuna mazowea ya kutawaliwa. Wengine tuliokuwa waumini wa *Afro Shirazi* na Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, maana yake sote tuna uhalali nayo hayo. Si lazima mtu atoke Kaskazini ya Unguja wala Kusini ya Unguja hata sisi wa Mjini yetu haya. Wangine wazee wetu walikuwa ndani jikoni katika upikaji na sio upikaji, tuutekelezeje pia.

Maana ya Mapinduzi tafsiri yangu mimi jambo la kwanza la Mapinduzi tujitawale, tulikuwa tunatawaliwa. Ni jambo la faraja kwa jamii ya Wazanzibari ni kwamba Mapinduzi yale yalikuwa ya aina pekee. Kwa maana

ilikuwa ni *Peoples' Revolution* ni Mapinduzi yaliyosimamiwa na watu wenyewe. *Afro Shirazi Party* ilikuwa muongozaji na Mapinduzi kama hayo duniani, nafikiri sisi ndio tunaoongoza na pengine Cuba lakini walichukua muda mwingi sana na China. Lakini yale yaliyochukua muda mfupi kukubalika na wengi na yakafanyika ndani ya siku moja ni Zanzibar peke yake. Walikubali umma ule na watu wale kutundika roho zao, kwa sababu walitaka kujitawala.

Mhe. Mwenyekiti ukishakujitawala baada ya hapo ndio unaweka misingi ya yale aliyoyatangazia. Bwana Abeid tarehe 8 Machi 1964 Maisara pale, ndio akaweka sasa malengo ya baada ya kupata kujitawala. Akaweka misingi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, elimu bure, maji safi na salama bure, ardhi kila mtu yake sasa na mengine mengi ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti la msingi miongoni mwa yale sote tukiwa sawa, hakuna bwana hakuna aliyekuwa mkubwa juu ya mwenziwe, ndani ya Jamuhuri ya Watu wa Zanzibar, sote sawa. Na kawambia wenziwe kaoweni sasa wa Malindi kawatafuteni wa Shangani, wa Malindi Jongiani, mama angu mmoja Fatma Mohammed Salim Jinja akaolewa na Marehemu Yussuf Himid nikapatikana mie wa mwanzo.

Hii ndiyo maana ya Mapinduzi kujenga jamii ya Wazanzibar ikiwa moja, watu wasiobaguana kwa rangi, anapotoka mtu, na kutukuka kwake kwa ubini wake. Hii ndio misingi sahihi ya Mapinduzi yetu. Siamini hata kidogo marehemu Mzee Karume na wenziwe walioongoza Mapinduzi yale halafu tutawaliwe na mtu mwengine. Nimesema huko nyuma, nitaendelea kusema mpaka kufa kwangu.

Mhe. Naibu Spika, kura za maoni hizi zimeletwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Bara yupo Dokta Jakaya Mrisho Kikwete Zanzibar yuko Dokta Ali Mohammed Shein, Serikali inayotawala ni ya Chama cha Mapinduzi na Bara ni ya Chama cha Mapinduzi. Viongozi wetu hawa walijua kwamba unapopeleka au unapomwaga mtama kwenye kuku wengi yatasemwa mengi. Unaposema sasa tuweni mawazo yenu, tuweni maoni yetu, tazuka mengi na wote hawa wanajua. Hawa ni watu wazima na walijua haya na wanajua kwamba ukishasema semeni, yatasemwa mengi. Na wengine wenziwao tutatofautiana na wao kwa mawazo.

Mhe. Naibu Spika, sijamsikia hata mmoja wao kusema usiseme hili. Sijamsiki Dokta Jakaya Mrisho Kikwete wala sijamsikia Dokta Ali Mohammed Shein kumkataza mtu yoyote kwamba usiseme hli na mimi natizama Maraisi wangu. Wametwambia kasemeni mnayoyataka lakini wote wawili wametwambia

zingatieni busara, zingatieni hekima, zingatieni sheria za nchi. Na mimi kwa hilo nakubaliana nao.

Jaji Warioba aliyekabidhiwa Tume ametwambia hata kama huutaki huo Muungano nenda kaseme. Na mimi nawambia Wazanzibari kama hawautaki waende wakaseme na wanaotaka mkataba akina sisi tutasema. Mwakilishi mimi nitasema tu na nitawashawishi wengine wakubaliane na yale ninayoyaona, kwa sababu ndio kazi yangu.

Lakini nikiwa kiongozi ndani ya nchi ni wajibu wetu, wangu mimi na wetu sote kutizama mambo kwa upeo wan chi. Hata jambo kama hulipendi lakini ukiweka mizani ukatizama hatima ya nchi yetu na tuendako na umuhimu wa kuwa na mahusiano mema na jirani zetu wote, basi wale wanaoukataa Muungano miye nawasihi tusielekee huko, tunacho kitu mkononi kwa miaka 48 sasa, tuna umuhimu wa kuwa na mahusiano mazuri na ndugu zetu. Na jambo moja wengi wanalisahau, kwamba mahusiano baina ya watu wa pande hizi mbili yapo kabla ya Muungano kurasimishwa. Kabla ya Mwalim Nyerere kuchukua haya akayatia ndani ya katiba, ndani ya makaratasi, sisi tulikuwa na Muungano wetu wananchi wa pande hizi mbili. Na hakuna ubaya wa kuyaendeleza na kuyadumisha yale na mengine kwa maslahi ya nchi yetu. Lakini naendelea kusema Mhe. Naibu Spika, mfumo huu kwangu mimi *sebu*! (*makofi*)

Mhe. Naibu Spika, *sebu!* na ninaamini tunaweza kuwa na Muungano *fair and equitable*, Muungano uliokuwa wa haki na wenye heshima na fursa sawa kwa pande zote mbili za muungano wetu. Inawezekana sana, na ni jambo jepesi sana, na ninaamini faida itakayopatikana hapo itakuwa kubwa sana kwa pande zote mbili za muungano wetu.

Mhe. Naibu Spika, nilizungumza awamu ya tano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nimekuwa nikitafakari sana, awamu ya tano ilianzisha utaratibu hapa wa EPZ na EEZ, Mhe. Asha Bakari anatikisa kichwa kwa sababu alikuwa sehemu ya Serikali ile na kiongozi wetu wa muda mrefu, na yeye ameyapitia mengi na kusimamia mengi kwa maslahi ya nchi yetu. Lakini sasa tujiulize mpango ule mpaka sasa hivi umeishia wapi.

Sisi ni wa mwanzo Afrika Mashariki na Kati kuwa na mipango endelevu na yenye upeo mkubwa katika kuzingatia maslahi na ustawi wa kiuchumi wa Wazanzibari, lakini sasa sisi tuko mkiani, nikiwa Waziri wa Ardhi miaka ile nilikuwa ninajua kule Fumba zimetengwa hekta 900, lakini mpaka hii leo kuna komba, ngedere na wanyama wengine, sasa tujiulize kwa nini haji muwekezaji hata mmoja pale Mhe. Naibu Spika? Narejea maneno ya Mhe. Mshimba tuache kuwadanganya watu.

Mhe. Naibu Spika, haji muwekezaji kwa sababu hatumiliki uchumi wetu wala mfumo wetu wa kodi hatuumiliki sisi. Kwa sababu muwekezaji Mhe. Naibu Spika, hasa kwa mazingira ya dunia ya leo ambapo pesa haipo tena, uchumi wa dunia umeathirika pakubwa, hawezi kuja na milioni zake dola mia akawekeza kwenye kiwanda pale bila ya kuwa na utaratibu ulio wazi, ajue anapoleta mali ghafi, wenzetu wamefanikiwa wawekezaji wanawaekea miundo mbinu, anamwambia wewe lete mali ghafi ya aina yoyote hapa *free of charge* hamna kodi. Ukitengeneza ukitoa wengine asilimia mbili, wengine asilimia nne, lakini faida yake ikifunga meli inalipa, mkipakua mizigo kwenye meli mnalipwa, gari zitakuwa hazitafuti kazi, kazi zinatafuta gari, vijana watapata kazi na taaluma mpya. Leo tunawadanganya vijana kazi hamna, anakuja kumfata Mwakilishi, mimi vijana wangu wote wanataka kwenda ZAT kwa Mhe. Raza.

Ninamshukuru sana wengi kawachukua, lakini Mhe. Raza atawachukua wangapi? Kila asubuhi vijana wanakuja kwangu niwapeleke ZAT nishawapeleka karibu ya 50 na anawasaidia, wanakwenda wanapata *course* wakirudi na vyeti vyao wanavuka vizingiti, ninamshukuru sana kwa uzalendo wake, mimi jimboni kwangu kanisaidia. Lakini atawachukua wangapi ZAT mmoja. Vijana wetu wanasoma vizuri mpaka *form six* fursa ya kwenda Chuo Kikuu hawana, wanatujia Wawakilishi anataka kijana kwenda Chuo Kikuu mwaka wa mwanzo milioni nne. Wewe una wako watatu ndani na kwa desturi zetu sisi Mhe. Naibu Spika, wazanzibari familia sasa wanakutizama wewe, umalize wa kwako, wa ndugu yako, wa shangazi yako, wa mjomba wako, wa jimboni basi hizi pesa za fomu huwezi kumpa milioni nne utamdanganya tu. Wanaosoma wapo wenye diploma jimboni kwangu hawana kazi, vikosi watakwenda wangapi? Maalim Haroun atawabeba wangapi? Lakini tukifika pahali tukiwa wakweli wa dhati, na tukasimamia maslahi ya nchi yetu, tukasema tunapiga mstari uchumi tuumiliki wenyewe, ndio nikasema yale maana ya mapinduzi kujitawala ni kujiamulia.

Vijana tunao kwa maelfu, tunaendelea kuwadanganya wanaosoma vizuri wakajisaidia wakasoma vizuri wote wanakwenda nje. Tulitaka kujiunga na OIC yakawa mengi Mhe. Raza ametwambia hapa anazo data zote, mwenye kutaka kumuuliza akamuulize. Kuna nchi zilizokuwa na asilimia kubwa za wakristo wapo kwenye OIC na wanafaidika kwa mabilioni, sasa jamani tuwe wakweli viongozi tujiulize ikija bilioni moja tu Zanzibar tuko wapi, wasituletee hayo mabilioni mengi ya dola, tupewe dola bilioni moja tu hapa tuko mbali. Tunazungumzia FIFA jaribuni kwenda kujiunga na chama cha *netball* tu nyie, si mnazungumza FIFA, mimi nasema kajiungeni na hicho chama cha *netball* muone hapa.

Sasa jamani hii ndiyo dhamira ya Muungano, huu ndio muelekeo wetu? Na jengine Mhe. Naibu Spika, kwa haya tujifundishe kustahamiliana, kwa sababu haya niliyozungumza hapa ni mawazo yangu mimi, haya hayamlazimu Maalim Haroun, yeye ana ya kwake na ni haki yake na anaweza kutofautiana na mimi, na mimi nikiwa na akili nitaendelea kumuheshimu huyu kama mzee wangu na kaka yangu, kwa sababu si lazima awe na mawazo kama yangu. Na wengine wana haki kuwa na mawazo mengine, lakini nasaha zangu jamani tufike sasa kuanza kutukanana matusi ya nguoni? Ndio hayo aliyosema Mhe. Mshimba, huyu sie, huyu mpinzani, huyu hizbu, sisi wengine tushayazoea hizbu asili, wala sipati tabu mimi kwa sababu nafsi yangu ninaijua mimi wenyewe, ninakotoka ninakujua mimi mwenyewe, mapenzi yangu na heshima yangu kwa chama changu ninayajua mimi mwenyewe, wala simtegemei mwengine kunifundisha hayo wala kunielekeza kwa hayo.

Yeye nani hata anambie mimi, yeye kaingia kama nilivyoingia mie na wengine wameingia kama walivyoingia wengine. Zile zama za kutishana ziko wapi jamani? Zama hizi mtu hakubaliani na mawazo yako nenda kamrai, anakwambia hataki Muungano mwambie kwa nini baba, mueke kitako muelekeze, mvute, lakini hauvunjiki huu, tutakiona, Husni Mubarak yuko wapi mfalme wa Misri yuko wapi? yuko jela. Zen bin Ali yuko wapi? kakimbia nchi yake. Gaddafi wamemtoa kwenye tundu vijana wamempiga risasi. Zama zimeshabadilika Mhe. Naibu Spika, watu hawataki tena kusemewa, watajisemea wenyewe na ni haki yetu Wawakilishi kuwasemea, kuwaelekeza, kuwashauri (makofi).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abubakar kaambiwa yeye Waziri wa uamsho na kaambiwa aifute, mimi ninamwambia huna haki ya kuifuta Muamsho na utaifuta kwa misingi ipi? Sisi kazi yetu kulinda uhuru wa watu, na serikali hii inayoongozwa na Dr. Shein inalinda uhuru wa watu. Uhuru wa kujikusanya, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kuwa na fikra tena zinatofautiana, uhuru wa kudai na kupewa majibu, kwa hivyo huna haki ya kuwafuta, unawafuta kwa misingi ipi? Labda wakikiuka sheria za nchi, wakikiuka sheria za nchi wenzio tutakuunga mkono sio wao tu na mwengine yeyote yule, NGO na taasisi nyengine yeyote ikikiuka sheria za nchi baada ya kufata taratibu za kupewa onyo, karipio na maelekezo una haki ya kuwafuta, lakini si kuwafuta kwa sababu watu fulani hawayapendi yale wanayoyasema. (Makofi).

Sasa mimi ninayapenda wanayoyasema, wanasema tuachiwe tupumue. Mhe. Naibu Spika, wanasema tuachiwe tupumue na mimi nishawahi kusema kwa hili nakubaliana nao, haki yetu, wajibu wetu na tufike pahali tumue kwa misingi ya heshima, kwa kulinda misingi imara tuliyoachiwa na Afro Shirazi yetu na kulinda Muungano uliokuwa wa heshima. Lakini huu ulivyo sasa Mhe. Naibu Spika, nishasema na ninaendelea kusema na baadhi ya vielelezo

vyangu kwa nini sikubaliani na mfumo huu uliopo sasa, nimeeleza machache tu yapo mengi ninaweza nikakaa mpaka saa nane za usiku hapa.

Kuna waraka alioandika Mwanasheria Mkuu, mambo yasiyojibika kwenye muungano nikiuchukua ule masaa manne na maandiko mengine, kwa hivyo mfumo huu *sebu*! Muungano wa heshima unaolinda heshima na utaifa wa pande zote mbili na sisi tukakiona kiti chetu cha Umoja wa Mataifa, tukafaidika na taasisi za umoja wa kimataifa moja kwa moja, tukafaidika na misaada ya washirika wa maendeleo moja kwa moja. Sisi watu wazima tukaambiwa 4.5 1964 mpaka leo 4.5, na marehemu Mzee Karume kasema mwanamme hashikiwi pesa zake, mwanamme anazikamata mwenyewe. Lakini OIC, taasisi za Umoja wa Kimataifa, *netball*, CECAFA, Afrika Mashariki na Kati, tena siku Dr. atakwenda Umoja wa Mataifa, Mwenyezi Mungu kama kaniweka hai hata kama simo nitajilipia mwenyewe niende.

Naishia hapa ninakushukuru lakini huu *sebu*!

Mhe. Naibu Spika: Kwanza niwashukuru wale waliopata nafasi na Wizara ina wachangiaji wengi, tuna wachangiaji 30 washachangia 12 bado 18. Sasa ninawashauri wale wote ambao leo sikuwaita, kesho waje mapema wasitoketoke wapate nafasi na wao waseme waliyonayo.

Baada ya hayo ninaakhirisha kikao hadi kesho tarehe 17/07/2012 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.45 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 17/07/2012 saa 3.00 asubuhi)